# YALIYOMO

UTANGULIZI ..... vii
TAFSIRI: ..... vii
SURA YA KWANZA: ..... 1
1.0 UTANGULIZI: ..... 1
1.1 Jina la chama ..... 1
1.2 Anuani ya UBOMA ..... 1
1.4 Muundo wa chama ..... 1
1.5 Hadhi ya chama kisheria. ..... 1
1.6 Imani ya chama ..... 2
1.7 Dira ya chama ..... 2
1.8 Dhima ya chama. ..... 2
1.9 Lugha rasmi ya chama: ..... 2
1.10 Kauli mbiu: ..... 3
SURA YA PILI: ..... 3
2.0. MADHUMUNI YA CHAMA ..... 3
2.1. Madhumuni ya chama cha UBOMA yatakuwa yafuatayo: ..... 3
2.2 Huduma zitolewazo na chama kwa wanachama ni kama zifuatazo: ..... 5
a) I: UGONJWA ..... 6
b) II: KIFO ..... 6
c) III: BIMA YA AFYA NA YA CHOMBO ..... 6
d) IV: MIKOPO MBALIMBALI ..... 6
2.3. Wajibu wa kuthibitisha uhalali wa huduma: ..... 7
SURA YA TATU: ..... 7
3.0. UANACHAMA ..... 7
3.3. Sifa ya Mwanachama. ..... 7
3.4. Kama mwenye kuomba kuwa mwanaumoja alishakuwa mwanaumoja; ..... 8
3.5 Sifa Za Kujiunga Na Umoja Wa Bodaboda Mkoa Wa Arusha(UBOMA) ..... 8
Rufaa dhidi ya kukataliwa Uanachama ..... 9

Michango ya mwanachama. .......... 9
a) Kiingilio cha mwanachama.......... 10
b) Ada ya mwanachama .......... 10
c) Michango Maalumu .......... 10
Kadi za uanachama .......... 10
Daftari la kudumu .......... 10
Data base .......... 11
Mgawanyo wa ada ya uanachama. .......... 11
HAKI ZA MWANACHAMA AU MWANAUMOJA .......... 11
Mwanachama wa bodaboda Mkoa wa Arusha atakuwa na haki zifuatazo: .......... 11
WAJIBU WA MWANACHAMA NDANI YA CHAMA: .......... 12
Mwanachama atakuwa na wajibu ufuatao ndani ya umoja, .......... 12
Miiko ya wanachama .......... 13
UKOMO WA UANACHAMA: .......... 13
Mwanachama atakoma kuwa mwanachama iwapo: .......... 13
Kufukuzwa uanachama. .......... 14
Utaratibu wa kumfukuza mwanachama utakuwa kama ufuatao: .......... 14
Mwanachama kuhamia kata au wilaya nyingine ndani ya Mkoa. .......... 15
SURA YA NNE: .......... 16
4.0 VIKAO VYA CHAMA NGAZI YA KITUO: .......... 16
MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA KITUO: .......... 16
MAJUKUMU YA VIONGOZI WA KITUO: .......... 17
VIKAO VYA CHAMA NGAZI YA KATA: .......... 18
KAMATI KUU YA KATA. .......... 18
MAJUKUMU YA KAMATI KUU YA KATA: .......... 18
HALMASHAURI KUU YA KATA: .......... 19
MAJUKUMU YA HALMASHAURI KUU YA KATA: .......... 19
MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA KATA: .......... 19
Mkutano mkuu wa kata ni chombo cha maamuzi ya mwisho ndani ya kata .......... 19

VIKAO VYA CHAMA NGAZI YA WILAYA: 20
Kamati kuu ya wilaya: 21
MAJUKUMU YA KAMATI KUU YA WILAYA: 21
Kupanga kalenda ya vikao vyote vya chama ikiwa ni pamoja na: 22
HALMASHAURI KUU YA WILAYA: 22
MAJUKUMU YA HALMASHAURI YA WILAYA: 22
Halmashauri ya Umoja itakuwa na majukumu yafuatayo: 22
MKUTANO MKUU WA WILAYA: 23
MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA WILAYA: 24
VIKAO VYA UMOJA NGAZI YA MKOA: 25
MAJUKUMU YA KAMATI KUU YA MKOA: 25
HALMASHAURI KUU YA MKOA: 27
MAJUKUMU YA HALMASHAURI KUU YA MKOA: 27
MKUTANO MKUU WA MKOA: 28
MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA MKOA: 28
SURA YA TANO: 31
5.1. MUUNDO WA UONGOZI; 31
5.2. VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA KITUO: 31
5.3. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA KITUO: 31
5.4. MAJUKUMU YA MAKAMU MWENYEKITI WA KITUO: 32
5.5 MAJUKUMU YA KATIBU WA KITUO: 32
5.6 MAJUKUMU YA NAIBU KATIBU WA KITUO: 32
5.7 MAJUKUMU YA MWEKA HAZINA WA KITUO: 32
5.8 MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MKUU WA KITUO: 33
5.9 MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA KITUO: 33
5.10 VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA KATA: 34
5.11. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA KATA: 34
5.12. MAJUKUMU YA MAKAMU MWENYEKITI WA KATA: 34
5.13. MAJUKUMU YA KATIBU WA KATA: 34

5.14. MAJUKUMU YA NAIBU KATIBU WA KATA: ........ 35
5.15. MAJUKUMU YA MWEKA HAZINA WA KATA: ........ 35
5.14. MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MKUU WA KATA: ........ 36
5.15. MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA KATA: ........ 36
5.16 AFISA HABARI WA CHAMA NGAZI YA KATA: ........ 36
5.17 MAJUKUMU YA AFISA HABARI WA CHAMA: ........ 36
5.18. VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA WILAYA: ........ 36
5.19. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA WILAYA: ........ 37
5.20. MAJUKUMU YA MAKAMU MWENYEKITI WA WILAYA: ........ 37
5.21. MAJUKUMU YA KATIBU WA WILAYA: ........ 37
5.22. MAJUKUMU YA NAIBU KATIBU WA WILAYA: ........ 38
5.23. MAJUKUMU YA MWEKA HAZINA WA WILAYA: ........ 38
5.24. MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MKUU WA WILAYA: ........ 38
5.25. MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA WILAYA: ........ 39
5.26. AFISA HABARI WA CHAMA NGAZI YA WILAYA: ........ 39
5.27. MAJUKUMU YA AFISA HABARI WA CHAMA: ........ 39
5.28. VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA MKOA: ........ 39
5.29. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA MKOA: ........ 40
5.30. MAJUKUMU YA MAKAMU MWENYEKITI WA MKOA: ........ 40
5.31. MAJUKUMU YA KATIBU MKUU WA MKOA: ........ 40
5.32. MAJUKUMU YA NAIBU KATIBU MKUU WA MKOA: ........ 41
5.33. MAJUKUMU YA MWEKA HAZINA WA MKOA: ........ 41
5.34. MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MKUU WA MKOA: ........ 42
5.35. MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA MKOA: ........ 42
5.36. AFISA HABARI WA CHAMA NGAZI YA MKOA: ........ 42
5.37. MAJUKUMU YA AFISA HABARI WA CHAMA: ........ 42
5.38 KAMATI MBALIMBNALI ZA CHAMA KIKATIBA: ........ 42
5.39 KAMATI YA UCHAGUZI NGAZI KATA: ........ 43
5.40 KAMATI YA UCHAGUZI NGAZI WILAYA: ........ 43

5.41 KAMATI YA UCHAGUZI NGAZI YA MKOA: ........ 44
5.42. KAMATI YA FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO NGAZI YA KATA: ........ 44
5.43 KAMATI YA FEDHA UCHUMI NA MIPANGO NGAZI YA WILAYA: ........ 44
5.44 KAMATI YA FEDHA UCHUMI NA MIPANGO NGAZI YA MKOA: ........ 45
5.45 KAMATI YA NIDHAMU NA MAADILI YA CHAMA KATA: ........ 45
5.46 KAMATI YA NIDHAMU NA MAADILI YA CHAMA WILAYA: ........ 46
5.47 KAMATI YA NIDHAMU NA MAADILI YA CHAMA MKOA: ........ 47
5.48 KAMATI MAALUM YA CHAMA KATA: ........ 47
5.49 KAMATI MAALUMU YA CHAMA WILAYA: ........ 48
5.50 KAMATI MAALUMU YA CHAMA MKOA: ........ 48
5.51 KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII YA CHAMA KATA: ........ 49
5.52 KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII YA CHAMA WILAYA: ........ 49
5.53 KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII YA CHAMA MKOA: ........ 49
5.54 KAMATI YA RUFAA YA CHAMA MKOA: ........ 50
5.55 MAJUKUMU YA KAMATI YA RUFAA YA MKOA: ........ 50
5.56 BARAZA LA WAZEE CHAMA KWENYE KITUO: ........ 51
5.57 MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE: ........ 51
5.58 BARAZA LA WAZEE WA CHAMA KATA: ........ 52
5.59. MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE: ........ 53
5.60. BARAZA LA WAZEE WA CHAMA WILAYA: ........ 54
5.61. MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE: ........ 54
5.62. BARAZA LA WAZEE WA CHAMA MKOA: ........ 55
5.63 MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE: ........ 56
SURA YA SITA: ........ 57
UCHAGUZI WA VIONGOZI KWENYE UMOJA NA SIFA ZAKE: ........ 57
6.1 SIFA ZA KUWA KIONGOZI: ........ 57
6.2. UCHAGUZI WA VIONGOZI NDANI YA CHAMA (UBOMA): ........ 58
6.3. ADHABU MBALIMBALI ZA MWANACHAMA NDANI YA CHAMA: ........ 62
SURA YA SABA: ........ 63

7.0. MFUKO WA CHAMA. 63
7.1. MFUKO MKUU WA CHAMA: 63
7.2. UTUNZAJI WA FEDHA ZA CHAMA: 64
7.3. UKAGUZI WA FEDHA ZA CHAMA 65
7.4. UWAJIBIKAJI KWENYE MASWALA YA FEDHA; 65
7.5. UTARATIBU WA UTOAJI POSHO; 66
SURA YA NANE: 70
8.0. BODI YA WADHAMINI: 70
8.6. Sifa Za Kuwa Kwenye Bodi Ya Wadhamini. 70
8.6.2 Kazi za bodi ya wadhamini. 70
8.6.4 Haki za bodi ya wadhamini. 71
8.13. Ukomo wa Ujumbe wa bodi ya Wadhamini. 71
SURA YA TISA: 72
9.1. TARATIBU ZA AJIRA, UTUMISHI NA USIMAMIZI WA WATENDAJI 72
SURA YA KUMI: 74
10.0. MENGINEYO 74
10.1. Utaratibu wa Kutengeneza Kanuni 74
10.7. Taratibu za ada ya uwakala 74
10.12. Kipindi cha Mpito 74
10.18. TARATIBU ZA USHIRIKIANO NA VYAMA AU TAASISI NYINGINE: 75
10.25. Ushirikiano na Vyama rafiki au vyenye mlengo sawa 75
10.29. Utaratibu wa kuunganisha vyama 76
10.32. Uwakilishi kwenye mialiko mbalimbali 76
SURA YA KUMI NA MOJA: 76
11.0. MAREKEBISHO YA KATIBA: 76

# UTANGULIZI

Mnamo mwezi Machi 2009, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya marekebisho katika sheria ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973 na kupitisha azimio la kuruhusu pikipiki za magurudumu mawili na magurudumu matatu kuwa moja ya vyombo vya usafiri vilivyoruhusiwa kutoa huduma ya kubeba abiria kwa malipo au kwa kukodishwa.

Sisi Bodaboda wa mkoa Arusha tunaofanya kwa biashara ya usafirishaji wa abiria kwa pamoja, tumeamua kuanzisha umoja wetu ujulikanao kama (UBOMA) Mwezi January 2024. Umoja huu utaongozwa kwa mujibu wa Katiba hii kama nguzo na dira yetu. Madhumuni ya Umoja yatakuwa ni yale tuyaliyoorodheshwa kwenye ibara ya pili ya Katiba hii ambayo yanalenga kusaidiana na kushirikiana katika masuala ya kuisaidia jamii nzima ya Watanzania hasa wale waishio katika mazingira magumu pale mfuko wa Umoja utakapokuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

**KWA KUWA** sisi waendesha pikipiki za kibiashara (Bodaboda) ni Raia halisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunalo jukumu la kuelimisha wenzetu juu ya matumizi bora ya Usalama wa Barabarani na utii wa sheria bila shuruti.

**KWA HIYO BASI**, Sisi sote waendeshaji wa Pikipiki za kibiashara, wamiliki wa vyombo hivi, tunaazimia kushirikiana na wataalam na taasisi/wadau wengine wa maendeleo kwa pamoja na kuunda umoja wetu utakao hakikisha kuwa huduma ya usafiri wa Pikipiki za magurudumu mawili na matatu ndani ya mkoa wa Arusha, inatolewa kwa kufuata sheria za nchi na kupata haki zote tunazostahili barabarani kutokana na maudhui hayo.

Katiba hii ya UBOMA ya mwaka 2024 ndio itakayoongoza utekelezaji wa shughuli za chama Kimukoa, aidha katiba hii itaendelea kufanyiwa marekebisho na wanachama kupitia mkutano mkuu watakavyoona inafaa na kwa kuzingatia kanuni za katiba hii na sheria za Nchi. Wanachama, viongozi, maafisa na watendaji wote wa chama katika ngazi zote hawana budi kuheshimu katila hii pamoja na Sheria za Nchi.

## TAFSIRI:

Katika Katiba hii maneno yafuatayo yatakuwa na tafsiri iliyotolewa kisheria kama ilivyoainishwa chini ya ibara hii isipokuwa pale ambapo yatakuwa yameainishwa vinginevyo katika ibara nyinginezo. Iwapo pana sheria yoyote nchini inayohusiana nayo kwa maana yanakubalika na chama.

**Akidi**- Ni idadi ya wajumbe wanaotakiwa ili kikao kianze.

**Alama**- Alama ni ishara ya kitu Fulani, kutakuwepo na alama katika kila Pikipiki na dereva. Itakayoonyesha ishara ya kutambua Pikipiki za Magurudumu mawili na matatu pamoja na dereva kwa kila kituo.

**Namba**- Ni idadi ya vitu, kutakuwepo na namba maalum itakayowekwa kwa kila Pikipiki za magurudumu mawil na matatu itakayonyesha idadi ya Pikipiki katika kila kituo, namba hizo zitawekwa pia katika kila vazi la Dereva**, (reflector)**

**Ajali**- ni tukio la dharura la kusababisha kutokea majeraha, maumivu ama kifo kutokana na mgongano wa vitu viwili kama gari na Pikipiki, Pikipiki na Pikipiki, Pikipiki na mwenda kwa miguu, dereva wa Pikipiki na abiria wake au dereva wa Pikipiki kuanguka pekee yake itahesabika kama hiyo ni ajali.

**Bodi ya Wadhamini** - Kutakuwa na bodi ya wajumbe Chombo cha wadhamini wa Chama chenye wajumbe watatu.

**Nembo ya Chama** - Alama ya chama itakuwa na mchoro wa barabara, pikipiki yenye magurudumu mawili na matatu.

**Fomu ya uanachama**- Fomu itakuwa na taarifa zote muhimu zinazomhusu mwanachama na chombo anacho kilimili au kukuendesha na sehemu anayopaki (kituo chake)**.**

**Chama** -Ni Umoja wa madereva na wamiliki wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu, waliosajiliwa kufanya biashara za usafirishaji wa abiria.

**UBOMA**- Umoja wa Bodaboda mkoa wa Arusha - Taratibu zinazoitafsiri Katiba na kutoa mwongozo wa utekelezaji wake.

"**Kituo**" Ina maana ya sehemu ya parking ya pikipiki za magurudumu mawili na matatu kuanzia wanachama watano (05) na kuendelea kutokana na ukubwa wa kituo husika.

**"Viongozi wa bodaboda wa chama ngazi ya kituo"** ina maana viongozi wote waliochaguliwa na wanachama ngazi ya kituo.

**"Mkutano Mkuu wa kituo"** ina maana ya Chombo chenye maamuzi ya mwisho katika Chama kwa ngazi ya kituo kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

"**Bodaboda Kata"** ina maana ya muunganiko wa vituo vya bodaboda ndani ya kata husika.

“**Viongozi wa bodaboda wa chama ngazi ya kata**” ina maana ya viongozi wa kata waliochaguliwa kutoka baadhi ya viongozi wa vituo ndani ya kata ambao ndio chombo cha tatu chenye maamuzi katika kata.

“**Halmashauri ya bodaboda kata**” ina maana ya viongozi wote wa vituo ndani ya kata ambacho ndicho chombo cha pili chenye maamuzi katika kata husika.

“**Mkutano mkuu wa bodaboda kata**” ina maana ya wanachama wote wa bodaboda ndani ya kata ambacho ndicho chombo cha kwanza chenye maamuzi katika kata.

“**Bodaboda wilaya**” ina maana ya muunganiko wa bodaboda kata zote katika wilaya husika.

“**Viongozi wa bodaboda wa chama ngazi ya wilaya**” ina maana ya viongozi waliochaguliwa kutoka kwa baadhi ya viongozi wa kata ambao ndio chombo cha tatu chenye maamuzi katika wilaya husika.

“**Halmashauri ya bodaboda wilaya”** ina maana ya viongozi wote wa kata ndani ya wilaya ambacho ndicho chombo cha pili chenye maamuzi katika wilaya husika.

“**Mkutano mkuu wa bodaboda wilaya”** ina maana ya viongozi wote wa vituo ndani ya wilaya na ndicho chombo cha kwanza chenye maamuzi katika wilaya.

**“Bodaboda mkoa”** ina maana ya muunganiko wa bodaboda wilaya zote ndani ya mkoa.

“**Viongozi wa bodaboda wa chama ngazi ya mkoa**” ina maana ya viongozi waliochaguliwa kutoka kwa viongozi wa kata na wilaya ndani ya mkoa na ndicho kitakuwa chombo tatu chenye maamuzi ndani ya mkoa.

“**Halmashauri kuu ya bodaboda mkoa**” ina maana ya viongozi wote bodaboda wilaya zote ndani ya mkoa ambacho ndicho chombo cha pili chenye maamuzi katika mkoa.

“**Mkutano mkuu wa bodaboda ngazi ya mkoa”** ” ina maana ya Mkutano Mkuu wa Chama mkoa au Chombo/Kikao cha juu kabisa cha maamuzi katika Chama au kama inavyofafanuliwa na Katiba hii.

**Katiba-** Katiba ndio sheria mama za chama. Ni sheria itakayosimamia uendeshaji wa shughuli za umoja (UBOMA) Ambayo itatumika kusimamia na kuelekeza fikra, mitazamo na maono ya wanachama ili kufikia malengo na madhumuni ya uanzishwaji wa Umoja.

**Mwanachama hai"** ina maana ya mwanachama anayeshiriki katika shughuli mbalimbali za chama na kutoa michango kwa mujibu wa katiba na taratibu za chama

**Mwanachama** – Ni Dereva wa pikipiki ya magurudumu mawilli na matatu ambaye anafanya biashara ya usafirishaji wa abiria kutoka sehemu moja kwenda nyingine ndani ya mkoa wa Arusha.

**Shirikisho"** ina maana ya muungano wa vyama huru vya bodaboda.

"**Afisa wa Chama**" ina maana ya mtumishi mwajiriwa yeyote wa Chama aliyeajiriwa kutekeleza majukumu mbalimbali ya Chama kwa mujibu wa Kanuni za ajira ndani ya Chama.

**Uongozi**: Ni dhamana ambayo imekabidhiwa kwa baadhi ya Wanaumoja ili waongoze wanaumoja na Umoja kwa ujumla ilikufikia malengo ambayo wanaumoja wamejiwekea. Kama mme au mke, mmojawapo atachaguliwa kuwa kiongozi wa umoja, aliyechaguliwa Ndiye kiongozi na siyomwenzi wake. Ushirika unabakia kwenye uanachama na siyo majukumu aliyokabidhiwa mmoja wao kama kiongozi;

"**Kiongozi**" ina maana ya mwanachama yeyote katika Chama ambaye madaraka, mamlaka au nafasi yake katika shughuli za Chama ameipata kupitia uchaguzi au kuteuliwa kwa mujibu wa Katiba hii.

"**Viongozi wa Chama**" ina maana ya viongozi wote wa kuchaguliwa wa Chama au walioteuliwa kwa mujibu wa Katiba hii kushika nafasi mbalimbali katika ngazi ya kituo hadi mkoa na ambao hawatahesabika kama waajiriwa/ watumishi wa Chama.

**Mwenyekiti** - Kiongozi Mkuu wa Chama katika ngazi husika.

***Mwenyekiti Msaidiz***i - Kiongozi mkuu msaidizi wa Chama katika ngazi husika**.**

**Katibu Mkuu** - Mtendaji Mkuu wa shughuli za Chama katika ngazi ya husika.

**Naibu Katibu Mkuu** - Mtendaji Mkuu Msaidizi wa Chama***.***

**Mweka Hazina** - Mtunza Hazina wa Chama katika ngazi husika.

**Kiongozi wa Nidhamu (kamanda**) Ni msimamizi mkuu wa nidhamu ndani ya chama**.**

**Makubaliano au Mkataba"** ina maana ya maelewano yaliyofikiwa kati ya mwajiri na Mfanyakazi au Chama chake kwa niaba ya mwanachama/wanachama.

"**Mfanyakazi**" ina maana ya mwajiriwa au mtu yeyote aliyeingia katika Mkataba/Makubaliano na mwajiri ya kutumia taaluma kama nyezo na nguvu kazi yake kuzalisha mali au kutoa huduma kwa

malipo yanayothaminika kifedha kwa kila saa ya uzalishaji mali au huduma. **Mlezi:** Mtu yeyote yule mwaminifu, mkarimu, msikivu, mwenye upendo na meandeleo ya watu, atakayependekezwa na bodi ya wakurugenzi kutekeleza na kuwa Mlezi kama Mshauri wa Chama katika mambo yote yanayohusu maendeleo ya Chama.

**Mradi-** chama kinaweza kuwa na mradi wowote utakao buniwa kwa lengo la kukuingizia chama mapato.

***Mtalaamu***: Ina maana ya mfanya kazi wa hiari au wa kulipwa/Kuajiliwa mwenye ujuzi na kile alichoomba ama kuombwa kusaidia katika chama ambaye atakuwa ni mtendaji wa hiyari, katika chama kutoka katika sekta binafsi au serikali na anaweza kutoa ujuzi wake kama ushauri kwa chama bila kuvunja mashafti mengine ya Katiba hii.

"**Mtumishi**" ina maana ya mtu yeyote kwenye Chama, ambaye madaraka, mamlaka au nafasi aliyonayo katika shughuli za Chama ameipata kupitia fursa ya ajira ya kudumu au ya mkataba kulingana na masharti ya ajira aliyonayo.

**Mgogoro** - Kuwepo hali isiyokuwa ya maelewano kati ya mwanachama na mwanachama mwenzake au kati ya kiongozi na viongozi wenzake au kati ya mwanachama na kiongozi.

**Mgomo** - Kitendo chochote kinachotendwa na wanachama ambacho kitasababisha uzorotaji wa kazi kutokana na kutoelewana kati ya mwanachama na chama au kati ya mwanachama na kiongozi.

"**Mwajiri**" ina maana ya mtu binafsi, kampuni, shirika, taasisi ama serikali ambaye ameingia makubaliano/mkataba wa kazi na mtu ama watu fulani kwa madhumuni ya kumfanyia kazi na yeye kulipa ujira.

"**Serikali**" ina maana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Ngazi za uwakilishi**- kutakuwepo na wawakilishi wa chama katika ngazi ya Vituo, Kata,na Mkoa. Ngazi hizi zitachagua wajumbe wa kuhudhuria mkutano wa Kamati ya Utendaji wa Ki-Mkao. Ngazi ndiyo sehemu ya muundo wa chama kikatiba.

**Muundo wa Chama**- Kituo, kata, wilaya, mkoa.

**Ulemavu** - Ni kukosa au kushindwa kuwa na fursa ya kushiriki katika maisha ya kawaida ya kijamii sawa na watu wengine kwa sababu za kimaumbile, kiakili au sababu za kijamii.

**Wadau**-Ni makundi washiriki wa maendeleo katika tasnia ya usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya pikipiki za magurudumu mawili na matatu.

**ADA-** Ada ni kiasi cha fedha ambacho kila mwanachama anachangia kwenye mfuko mkuu wa umoja kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za umoja

# SURA YA KWANZA:

## 1.0 UTANGULIZI:

### 1.1 Jina la chama

Jina la chama ni **UMOJA WA BODABODA MKOA WA ARUSHA** (UBOMA).

### 1.2 Anuani ya UBOMA

Anuani ya chama ni:

UBOMA Makao Makuu

S.L.P 3013, ARUSHA

Simu: + 0621087351/0752947499

Fax:

Barua pepe **ubomarusha@gmail.com**

Toviti: www.uboma.org.tz

Mtaa: kaloleni magharibi.

Kata: kaloleni.

Manispaa ya Arusha jiji.

### 1.3 Makao makuu ya chama

Makao makuu ya chama yatakuwa Arusha au mahali pengine popote, katika mkoa wa Arusha kama itakavyoamuliwa na kamati kuu ya chama.

### 1.4 Muundo wa chama

Chama kitakuwa na ngazi nne za muundo wa kiuongozi ambazo ni: Kituo, Kata, Wilaya na Mkoa.

### 1.5 Hadhi ya chama kisheria.

UBOMA ni chama kilichosajiliwa wizara ya mambo ya ndani chini ya kifungu no………..ambavyo chama hiki siyo cha kiserikali, kisiasa, kabila wala dini hivyo kina haki ya kushitaki au kushitakiwa katika vyombo vya sheria ndani ya nchi kwa jina lake.

## 1.6 Imani ya chama

Chama cha UBOMA kinaamini kwamba:

(a) Binadamu wote duniani ni sawa.

(b)Kila mtu ana haki ya kufanya kazi na anastahili malipo kufuatana na kazi hiyo pamoja na kuheshimiwa kama binadamu katika mazingira salama.

(c) Wamiliki wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu za kibiashara ndio injini na uti wa mgongo wa maendeleo ya uchumi wa taifa letu.

(d)Nguvu ya wamiliki wa vyombo vya moto ndiyo chachu ya maendeleo ya taifa na ukombozi wao.

(e)Utengano wa aina yoyote kati ya wanachama ni alama dhaifu katika juhudi za kuimarisha mshikamano wa kuendeleza mapambano yao.

(f)Nguvu ya umoja inatokana na juhudi zao katika kukuza na kuimarisha umoja wao na baina ya vyama vyao.

## 1.7 Dira ya chama

Kuwa chama imara, chenye nguvu, cha kidemokrasia, kinachojitegemea, kinachounganisha na kutetea haki za madereva wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu ambao ni wamiliki kibiashara.

## 1.8 Dhima ya chama.

Ni kushirikisha wanachama katika maamuzi, kushinikiza kuwepo kwa sera za kuongeza na kupanua wigo na kuwaunganisha wanachama katika kuweka mazingira bora ya biashara na kutetea haki na maslahi na kuhakikisha wanapata elimu katika tasnia ya usafirishaji abiria.

## 1.9 Lugha rasmi ya chama:

1.9.1 Lugha rasmi zitakazotumika katika vikao, mikutano au shughuli zozote za Chama zitakuwa Lugha ya **Kiswahili** na **Kiingereza.**

1.9.2 Chama kitaruhusu kutumika kwa lugha nyingine tofauti na zilizotajwa hapo juu katika shughuli zake ikiwemo katika kutunza baadhi ya kumbukumbu endapo mazingira ya kutumia lugha hiyo yameridhiwa na wajumbe walio wengi watakaokuwa katika Kikao au Mkutano husika**.**

1.9.3 Bila kuathiri masharti mengine ndani ya Katiba hii, endapo katika Kikao au Mkutano wowote ataalikwa mgeni asiyefahamu lugha ya Kiswahili au Kiingereza, mgeni huyo ataruhusiwa kutumia lugha anayoifahamu na atakaribishwa Mkalimani atakayetoa tafsiri ya kile kitakachokuwa kinaongelewa.

**1.10 Kauli mbiu:**

***BODABODA USAFIRI SALAMA au BODABODA KAZI KAMA KAZI NYINGINE USIICHUKULIE POA.***

# SURA YA PILI:

## 2.0. MADHUMUNI YA CHAMA

### 2.1. Madhumuni ya chama cha UBOMA yatakuwa yafuatayo:

a) Kulinda na kutetea haki na maslahi ya wanachama na kuendeleza Juhudi za kuboresha hali za maisha yao wanapokuwa katika kazi zao.

b) Kusimamia, kuendeleza na kulinda maslahi ya watumiaji wa Pikipiki za magurudumu mawili na matatu ndani ya mkoa wa Arusha.

c) Watendaji wa UBOMA watahakikisha katika mamlaka husika za Serikali na umma kwa ujumla kuwa kuna vivutio vya kutosha na mazingira mazuri ya kufanya biashara ya usafirishaji abiria kwa kutumia pikipiki za magurudumu mawili na matatu.

d) Kuhakikisha madereva wote wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu kwa ajili ya kubeba abiria wanafuata na kuzingatia sheria za usalama barabarani.

e) Kuwa mdau mkubwa wa usalama barabarani katika kuhakikisha jitahada za serikali Kupunguza au kumaliza ajali za barabarani zinakuwa na mafanikio chanya kwa kushiriki katika kutoa elimu ya usalama barabarani kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa barabara. Kuwakutanisha madereva wa pikipiki za magurdumu mawili na matatu ambao ni wamiliki kibiashara ili kujadili maendeleo na matatizo yao katika matumizi ya Barabara na utoaji wa huduma zao na kutafuta mbinu ya kuzitatua changamoto za kisheria kwa kushirikiana na wasimaizi wa sheria.

f) Kujadili na kushauriana na wakuu wa mamlaka zinazosimamia kanuni na sheria za matumizi ya barabara kwa niaba ya madereva wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu ambao ni wamiliki kibiashara kufuatilia haki, maslahi na haki nyingine zinazohusiana na mazingira ya utoaji wa huduma ya usafiri wa Pikipiki ndani ya Mkoa Arusha. Kuishauri Serikali juu ya mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya utoaji wa

huduma hii ya usafiri wa Pikipiki za biashara za magurudumu mawili na matatu kama vile kuweka utaratibu wa maegesho, uongozi katika maegesho na serikali za mitaa.

g) Kuishauri Serikali namna iliyo bora ya kupambana na uhalifu wa kijinai kwa kutumia pikipiki za magurudumu mawili na matatu.
h) Kupokea maoni, malalamiko ya wanachama wa vituo vya pikipiki za magurudumu mawili na matatu ndani ya Mkoa na kuwasilisha maoni hayo katika ngazi husika ili kupata msaada unaohitajika.
i) Kusuluhisha na kutatua malalamiko au migogoro mbalimbali ya wanachama katika vituo, Kata, Wilaya, na Mkoa kwa wawakilishi wa chama kimkoa pamoja na kuweka bayana makubaliano yaani mikataba kati ya waendasha Pikipiki za magurudumu mawili na matatu na waajiri wao kwa wale watakaokuwa wameajiriwa kufanya kazi hiyo na watu binafsi na makundi yote katika jamii.
j) Kuandaa mikakati na mipango kazi itakayounganisha wadau wote kutekeleza mpango wa utoaji huduma bora na salama ya usafiri wa Abiria kwa njia ya Pikipiki za magurudumu mawili na matatu.
k) Kufanya utafiti na uchambuzi mbalimbali dhidi ya utoaji wa huduma ya usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu ili kuwa huduma bora na salama.
l) Kushauri na kutetea sera itakayolinda hadhi na heshima ya utoaji wa huduma hii ya usafirishaji kwa njia ya Pikipiki za magurudumu mawili na matatu. na kuhimiza huduma ya Afya ikiwa ni pamoja na kuwa na Bima ya Afya.
m) Kuhimiza, kuwahamasisha na kuwataka waendeshaji wa vyombo hivi vya magurudumu mawili na matatu kuhudhuria mafunzo ya aina yoyote ile itakayowasaidia katika maendeleo ya shughuli zao.
n) Kuhakikisha kuwa wasimamizi wa sheria za Barabarani na watumiaji wa usafiri wa Pikipiki za magurudumu mawili na matatu wanazingatia na kutekeleza vyema sheria na kanuni za nchi.
o) Chama hiki kitakuwa na wajibu wa kuomba tenda mbalimbali za ukusanyaji wa mapato ya serikali au taasisi binafsi kwa kadri tenda hizo zitakapo tangazwa ndani ya mkoa wa Arusha.
p) Kuanzisha taasisi ya mikopo kwa wanaumoja kwa ajili ya kukopeshana ndani ya mkoa wa Arusha.
q) Kujadiliana na taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali kwa ajili ya kuinua uwezo kiuchumi kwa Wanaumoja ili kupata mikopo mbalimbali kama:
    a. Pikipiki.
    b. Bajaji

c. Vipuri.
d. Fedha.
e. Viwanja.
f. Nyumba. n.k.

r) Kuhakikisha tunashirikiana na taasisi mbalimbali zitakazo kuwa tayari kushirikana na umoja wetu ili kutoa fursa kwa wanachama wetu.
s) Kuanzisha vituo vipya vya waendesha pikipiki za magurudumu mawili na matatu ndani ya mkoa wa Arusha kwa sehemu ambazo zitakuwa na uhitaji wa kufanya hivyo.
t) Kufuta vituo ambavyo havitaki kufuata sheria na taratibu na kanuni za serkali na maelekezo ya chama chetu.
u) Kuimarisha usafi wa mazingira kwenye vituo.
v) Kuelimisha abiria juu ya haki zake za msingi kabla ya kupanda pikipiki.
w) Kuanzisha michezo mbalimbali ndani ya mkoa wa Arusha.
x) Kuwa na mifumo wa mawasiliano kunanzia ngazi ya kituo, kata, wilaya na Mkoa na Kuimarisha mfumo wa utambuzi wa wanaumoja ndani ya Mkoa wa Arusha.
y) Umoja utashirikiana na serikali na taasisi binafsi katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

## 2.2 Huduma zitolewazo na chama kwa wanachama ni kama zifuatazo:

Wanafamilia wanaotambuliwa na kuhudumiwa kwa mujibu wa katiba hii

a. Mume na mke mmoja
b. Watoto wanne wa kuzaa au kuasili kwa mujibu wa sheria za nchi

- Wanafamilia watakaotambuliwa na kuhudumiwa ni sharti
  i. Wawe wamejazwa kwenye fomu ya tarifa ya mwanachama na wamewekwa kwenye mfumo wa data base ya umoja
  ii. Watoto wawe chini ya umri wa miaka 18 au kama motto ana umri wa Zaidi ya miaka 18 kivuli cha kitambulisho cha shule au chuo kiambatanishwe kwenye fomu ya kuomba huduma
  iii. Motto aliyefikisha umri wa miaka 18 hatahudumiwa hata kama ni mwanafunzi iwapo ana familia, amedailiwa chuoni kusoma shahada ya uzamili au uzamivu.

**a.** Kusaidiana katika shida mbalimbali ambazo zitakuwa ndani ya uwezo wa wanaumoja.
b. Mwanachama wetu atanufaika na huduma zifuatazo ndani ya umoja;
  i. Ugonjwa.
  ii. Kifo.
  iii. Bima ya afya na ya chombo.
  iv. Mikopo mbalimbali.

**a) I: UGONJWA**

c. Kumpatia mchango wa matibabu mwanachama ambaye amelazwa hosipitali kuanzia siku tatu (3) au zaidi.
d. Huduma ya kulazwa hospitali inaweza kutolewa kwa mwanachama ambaye hali ya Ugonjwa wake anaweza kuruhusiwa kutoka hosipitali au hata pengine asilazwe kabisa lakini kwa namna alivyougua ugonjwa ambao utamlazimu kuugulia nyumbani zaidi ya mwezi moja bila kupona.
e. Itakuwa kinyume cha katiba kutoa huduma hii kwa mwanachama aliyeugua akabakia nyumbani bila kwenda kupata matibabu hospitali.
f. Kumpatia mwanachama mgonjwa kiasi cha fedha kilichoainishwa kwenye kanuni za umoja ambaye kutokana na hali yake ya kiafya ameamua kwenda kuugulia eneo lililoko nje ya Arusha na kwa hiari yake kaamua kusitisha uwanachama wake kwa kuandika barua ya kujitoa kwenye umoja huduma hii haitatolewa mpaka:
(i) Awe ni mwanachama hai.
(ii) Awe amepoteza matumaini ya kupona.
(iii) Iwapo atapona na kurudi atalazimika kujiunga upya.

**b) II: KIFO**

**g.** Kiasi cha fedha kitatolewa na kamati kuu kwa mujibu wa katiba kwa kushirikiana na familia ya marehemu kulipia gharama za hospitali pamoja na shughuli zote za mazishi.
**h.** Baada ya msiba kutokea ndani ya kata husika uongonzi wa mkoa, wilaya, kata na kituo utasaidiana na familia ya marehemu kuratibu msiba kipindi chote cha msiba mpaka mwili utakapo zikwa.
i. Kwenye kituo kilichopoteza mwanachama kwa kukutwa na umauti kituo kinahimizwa kuhudhuria msiba kipindi chote cha maombolezo.

**c) III: BIMA YA AFYA NA YA CHOMBO**

**j.** Umoja utakuwa na utaratibu wa utoaji wa bima za afya.
k. Mwanachama atalipiwa bima ya chombo na chama kutoka kwenye ada yake kwa mujibu wa katiba na
l. Katiba na kwa kufuata viwango vilivyoanishwa kwenye kanuni za umoja.

**d) IV: MIKOPO MBALIMBALI**

m. Umoja utaweka utaratibu wa utowaji mikopo mbalimbali kwa wanachama ya kwa mujibu wa sheria za umoja na kwa kufuata kanuni za umoja.

### 2.3. Wajibu wa kuthibitisha uhalali wa huduma:

2.3.0 Uthibitisho wa huduma iliyotolewa kwa mwanachama yeyote aliyelipwa fedha ya huduma anawajibika kuwasilisha kwa mweka hazina vilelezo vifwatavyo:

- **a)** Kivuli cha cheti cha kifo(death certificate) kama huduma iliyotolewa ilihusu kifo.
- **b)** Barua ya afisa mtendaji wa kijiji kama msiba umetokea mazingira ambayo cheti cha kifo hakiwezi kupatikana.
- **c)** Fomu ya kuruhusiwa kutoka hosipitali (discharge summary) kama huduma iliyotolewa ilihusu kulazwa hosipitali.
- **d)** Vielelezo vingine kulingana na huduma iliyotolewa au uamuzi wa uongozi.
- **e)** Mwanachama au ndugu atakayeshidwa kuwasilisha vielelezo vya huduma ndani ya siku sitini (60) atalazimika kurudisha fedha aliyopewa kama huduma

## SURA YA TATU:

### 3.0. UANACHAMA

3.1. Chama cha UBOMA kitakuwa na aina mbili za wanachama kama ifuatavyo:

- a) Wanaumoja waanzilishi waliokutana kwa mara ya kwanza na kuanzisha umoja huu.
- b) Wanachama wanaoendelea kujiunga baada ya umoja kuanzishwa.

3.2. Wanachama waanzilishi na waliojiunga baadae wote watajulikana kama wanachama au wanaumoja kwa mujibu wa katiba hii.

### 3.3. Sifa ya Mwanachama.

Ili mtu yeyote apokelewe kwenye chama cha waendesha bodaboda mkoa wa Arusha sharti awe na sifa zifuatazo:

- a) Umri wa miaka 18 au Zaidi
- b) Awe na leseni ya udereva, latra, na viambatanisho vingine kwa mujibu wa sheria ya usafirishaji.
- c) Awe anafanya biashara ya kuendesha pikipiki ya magurudumu mawili au matatu ndani ya mkoa wa Arusha.
- d) Mwaminifu
- e) Mwenye akili timamu
- f) Sifa nyingine ni zile zilizoainishwa kwenye kanuni za umoja wa mkoa.

g) Ni kinyume cha masharti ya katiba hii Kwa mtu yeyote ambaye hajasajiliwa kupitia namba ya kituo na namba ya ubavuni kuendesha pikipiki ya magurudumu mawili au matatu kujiunga na umoja huu.

### 3.4. Kama mwenye kuomba kuwa mwanaumoja alishakuwa mwanaumoja;

a) Kabla ya kupokelewa atalipa madeni aliyoacha kabla ya kuondoka kwenye umoja.
b) Kama alifukuzwa kwa kukiuka taratibu za umoja au aliacha madeni, atakuwa kwenye kipindi cha majaribio kwa mwaka mmoja.
c) Mwanaumoja aliye kwenye kipindi cha majaribio hatapewa huduma yoyote.
d) Mwendesha bodaboda yeyote anaetoa huduma ya usafirishaji ndani ya jiji la Arusha lazima awe amesajiliwa ndani ya kituo/ofisi atakapofanyia kazi.
e) Taarifa zake lazima zifike ngazi ya kituo, kata, wilaya pamoja na halimashauri ya jiji la Arusha.

### 3.5 Sifa Za Kujiunga Na Umoja Wa Bodaboda Mkoa Wa Arusha(UBOMA)

Mtu mwenye kujiunga na umoja wa bodaboda atafuata taratibu zifuatazo:

a) Atakuja na barua ya utambulisho kutoka kwa afisa mtendaji wa kata
b) Mwenyekiti wa mtaa wake ikiwa imegongwa muhuri pamoja na passport size 3
c) Atajaza form inayopatikana kwa katibu wa kituo husika lakini pia baada ya kujaza form hiyo itaambatanishwa na vitu vifuatavyo:
d) COPY YA LESENI YA DEREVA.
e) COPY YA LATRA.
f) COPY YA BIMA NA STIKA YA NENDA KWA USALAMA BARABARANI.
g) HELMET MBILI (02) NGUMU.
h) Zitakaguliwa na mwenyekiti wa kituo husika mahali ambapo unataka kupaki.
i) Ataweka fedha ya kiingilio kwenye account ya Umoja Kama ilivyoainishwa kwenye kanuni.
j) Atapeleka form iliyojazwa na benki slip kwa katibu wa kituo.
k) Viongozi wa kituo watajadili na kujiridhisha kuwa imejazwa ipasavyo.
l) Katibu wa kituo ataweka maoni yake ya kituo.
m) Katibu wa kituo atapeleka form ya benki slip Kwa katibu wa kata husika na katibu wa kata husika atapeleka benki slip hiyo kwa katibu wa wilaya husika na katibu wa wilaya husika atapeleka kwa katibu wa mkoa.
n) Baada ya kupokea form katibu mkuu wa mkoa atajiridhisha kwa taarifa zifuatazo.
o) Form imejazwa kwa ukamilifu.
p) Taarifa zilizojazwa hazina mashaka.

q) Mwombaji ana sifa za kujiunga na umoja.
r) Iwapo katibu mkuu atajiridhisha kwamba form imejazwa ipasavyo ataifikisha kwenye kikao cha kamati kuu ili ijadiliwe.

3.5. Mtu yeyote atachukuliwa kuwa amepokelewa kwenye umoja baada ya:

a) Form yake ya maombi ya kujiunga na umoja kujadiliwa na kikao cha kamati kuu ngazi husika na kufikia uamuzi wa kumpokea.
b) Mwanachama anayejiunga kwenye umoja wa Bodaboda Mkoa wa Arusha atalipa kiingilio cha kiasi cha fedha kilichoainishwa kwenye kanuni za umoja na kukatiwa risiti ya uthibitisho wa malipo ambayo uthibitisho wake ni benki deposite slip iliyoambatanishwa kwenye form ya maombi ya kujiunga na umoja.

3.6. Mtu atachukuliwa kuwa mwanaumoja kuanzia tarehe ya stakabadhi ya malipo ya kiingilio.

3.7. Mtu yeyote ambaye fomu yake imekataliwa Kwa sababu ya kutoa taarifa za uongo au uanachama wake umekuwa batili Kwa sababu za uongo wakati wa kujaza fomu ya usajili hatarudishiwa fedha alizotoa kwenye umoja.

3.8. **CHAMA KIMEWEKA UTARATIBU WA KUSAJILI WANACHAMA WAPYA NA KUFUNGUA KITUO KIPYA KAMA IFUATAVYO:**

3.9. Katiba hii ya umoja wa waendesha Bodaboda mkoa wa Arusha inatambua kwamba wanaoruhusiwa kusajili wanachama wapya na kufungua vituo vipya ni:

a) Viongozi wa bodaboda kata.
b) Viongozi wa bodaboda Wilaya na mkoa endapo itahitajika kufanya hivyo.
c) Taarifa hizo za mwanachama mpya zifike ngazi ya Mkoa.

3.10. Viongozi waliotajwa hapo juu kikatiba ndio wenye mamlaka ya kupeleka wanachama wapya kwenye vituo na kufungua vituo vipya.

3.11. Ni kinyume cha katiba hii viongozi wa serikali au viongozi wa chama chochote cha siasa kujihusisha na ufunguzi wa vituo vyovyote au kupeleka mwanachama yoyote kwenye kituo.

## Rufaa dhidi ya kukataliwa Uanachama

Mwombaji asiyeridhika na uamuzi wa kituo anayo haki ya kujieleza mbele ya kamati ya rufaa ya Mkoa iwapo hataridhika, muombaji anaweza kukata rufaa katika kata na kwenye vikao vya juu Zaidi vya chama ambavyo vitatoa uamuzi wa mwisho.

## Michango ya mwanachama.

Michango ya chama itakusanywa kutoka kwa wanachama kama ifuatavyo:

**a) Kiingilio cha mwanachama.**

(i) Muombaji aliyekubaliwa uanachama atatakiwa kulipa kiingilio na kupewa kadi ya uanachama.

(ii) Kiingilio kitapangwa na mkutano mkuu wa chama Mkoa kwa mujibu wa katiba.

**b) Ada ya mwanachama**

Ada ya mwanachama italipwa, kila mwezi kwa viwango vitakavyowekwa na mkutano mkuu wa chama kwa mujibu wa katiba hii.

1. Utaratibu wa malipo ya ada za mwanachama yatafanywa kama ifuatavyo:

   (i) Ada inaweza kulipwa na mwanachama mwenyewe kituoni kwake kupitia mifumo mbalimbali ya malipo ya chama na kupewa stakabadhi yake ya malipo na kituo.

   (ii) Ada ya wanachama wa **UBOMA** inaweza kulipwa kwa mkupuo au mara mbili tu.

   (iii) Michango yote ya chama italipwa kupitia benki kwenye akaunti za chama.

   (iv) Ruzuku za kata na wilaya zitalipwa kutoka kwenye mfuko mkuu wa chama kwa viwango vitakavyopangwa na mkutano mkuu wa Mkoa ukizingatia uwiano wa wanachama ndani ya kata na wilaya.

**c) Michango Maalumu**

Kila inapobidi chama kitaagiza na wanachama watawajibika kutoa michango maalumu kama itakavyokubaliwa na vikao husika kwa manufaa ya wanachama.

## Kadi za uanachama

Kila mwanachama atapewa kadi ya chama itakayobandikwa picha yake na kujazwa:

(a) Jina lake.
(b) Anuani yake.
(c) Kazi yake.
(d) Tarehe ya kujiunga.
(e) Maelezo mengine muhimu.

## Daftari la kudumu

Kutakuwa na daftari la kudumu kwa madhumuni yafuatayo:

(a) Kuingiza maelezo yote ya wanachama yaliyomo katika kadi yake na kuhifadhi taarifa zote muhimu zinazohusu uhai wa mwanachama, ikiwa ni pamoja na michango aliyotoa.

(b) Ni wajibu wa viongozi ngazi zote za chama kutunza kumbukumbu zote muhimu zinazohusu uhai wa wanachama katika Daftari lake la kudumu.

## Data base

Chama kitakuwa mfumo wa data base mfumo huo utakuwa upo kwa ajiri ya uhifadhi wa taarifa zote za wanachama online

## Mgawanyo wa ada ya uanachama.

(a) Makao makuu ya chama, itarejesha ruzuku za uendeshaji katika ngazi za chama kama ifuatavyo:

(i) Kituo kitawekewa asilimia kumi na tano 15% kwenye akaunti ya kituo ya makusanyo yao.

(ii) Kata itawekewa asilimia ishilini 20% kwenye akaunti ya kata ya makusanyo yao.

(iii) Wilaya itawekewa asilimia ishirini na tano 25% kwenye akaunti ya wilaya ya makusanyo yao. Na

(iv) Mkoa utabaki na asilimia arobaini 40% kwenye akaunti ya chama.

## HAKI ZA MWANACHAMA AU MWANAUMOJA

**Mwanachama wa bodaboda Mkoa wa Arusha atakuwa na haki zifuatazo:**

a) Kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa umoja

b) Kupata taarifa ya mali au fedha za umoja.

c) Kupata taarifa za mapato na matumizi kwa mujibu wa katiba.

d) Kupata taarifa juu ya mwenendo wa taarifa za shughuli za umoja

e) Kupewa fursa ya kujitetea mbele ya kamati ya nidhamu na maadili ngazi ya kituo, kata na wilaya na mkoa.

f) Kama matatizo ni ya uongozi wa Mkoa rufaa yake itaishia kwenye bodi ya wadhamini ya chama kupitia kamati kuu na kamati ya usuluhishi.

g) Bodi ya wadhamini wanayo mamlaka ya kuonya, kusimamia na kushauri kamati zote ndani ya chama Mkoa na kuchukua hatua za kinidhamu kwa kiongozi yeyote yule pale panapo shindikana na kamati kuu italazimika kuitisha mkutano mkuu kwa ajili ya kutoa mapendekezo na maamuzi ya mwisho dhidi ya kiongozi husika ngazi ya Mkoa.

h) Kutetea maslahi na haki zake za chama kuhusiana na shughuli zake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na katiba hii.

i) Kushiriki na kufaidi matunda yote au mafanikio yatokanayo na ushiriki wake katika chama kwa ujumla.

j) Kupata haki ya kukata rufaa iwapo hakupata haki kutoka kwenye kamati ya nidhamu na maadili.
k) Kushiriki kwenye shughuli za umoja.
l) Kuhudumiwa wakati wa shida kwa huduma zilizoainishwa kwa mujibu wa katiba hii.

M).Kutoa mawazo Kwa uhuru bila kuzomewa, kutishiwa, kushurutishwa au kushawishiwa na mtu yeyote ilimradi havunji taratibu za umoja.

## WAJIBU WA MWANACHAMA NDANI YA CHAMA:

**Mwanachama atakuwa na wajibu ufuatao ndani ya umoja,**

a) Kuchagua na kuchaguliwa, kushika nafasi ya uongozi wa chama
b) Kujitetea na kutoa maelezo mbele ya kikao cha chama au chombo kinachohusika katika mashitaka yoyote yaliyotolewa dhidi yake.
c) Kupata taarifa ya fedha na mali za umoja mara moja kwa mwaka ngazi ya Mkoa wakati wa mkutano mkuu.
d) Kupata taarifa juu ya mwenendo wa shughuli za umoja.
e) Kupewa fursa ya kujitetea mbele ya kamati ya nidhamu na maadili ya kata, endapo hataridhika na maamuzi yaliyotolewa dhidi yake atakata rufaa kwa kamati ya nidhamu na maadili ngazi ya wilaya na endapo hataridhika na maamuzi yaliyotolewa dhidi yake atakata rufaa kwa kamati ya nidhamu na maadili ngazi ya Mkoa.
f) Kila mwanachama atakuwa na haki ya kupata huduma zilizoainishwa kwa mujibu wa katiba.
g) Kutoa mawazo kwa uhuru kwenye vikao bila kuzomewa, kutishiwa, kushurutishwa ama kushawishiwa na mtu yeyote ilimradi havunji taratibu za umoja.
h) Mwanachama wa umoja Mkoa wa Arusha atakuwa na wajibu ufuatao:
i) Kusoma na kuelewa katiba ya umoja.
j) Kulinda, kutetea na kuheshimu katiba.
k) Kulipa ada na michango mingine ndani ya muda uliowekwa.
l) Kuunga mkono na kusaidia kwa maneno na vitendo maendeleo ya umoja.
m) Kuhudhuria mikutano na vikao halali vilivyowekwa kikatiba pamoja na misiba
n) Shughuli nyingine za umoja zitakazoamriwa na vikao vya umoja.
o) Kuhudhuria mafunzo ama semina ya aina yoyote kadri zitakazotolewa taarifa na uongozi katika ngazi husika ili kujiendeleza na kupata maarifa mapya.
p) Kutoa misaada kwa wenzake na kushiriki shughuli za pamoja za wanachama.

q) Kutoa taarifa kwa uongozi kwa haraka iwezekanavyo kwa pale itakapohitajika msaada wa viongozi wa ngazi zote
r) Kutoa ushirikiano wa maswala yote yanayohusu usalama wa nchi ikiwa ni pamoja na kushiriki mikutano mbalimbali ya maendeleo ya wananchi na viongozi wa kiserikali.
s) Kutokujichukulia sheria mkononi pale tatizo litakapotokea watoe taarifa kwa ngazi husika mara moja.

**Miiko ya wanachama**

(a) Mwanachama wa **UBOMA** hatajihusisha au kushiriki kaika vikao au mikutano inayojadili hoja za kupingana na katiba, kanuni,au miongozo ya chama.
(b) Hatashiriki katika migomo au maandamano au hatua nyingine zozote za ushinikizaji ambazo hazikuandaliwa na chama.
(c) Hatatoa lugha chafu ya matusi kwa viongozi wa chama, au kwa wanachama wenzake.
(d) Hatatoa kauli za uwongo popote pale.

## UKOMO WA UANACHAMA:

**Mwanachama atakoma kuwa mwanachama iwapo:**

i. Atafariki.
ii. Ataugua ugonjwa wa akili
iii. Atafungwa jela kwa makosa ya jinai.
iv. Atafukuzwa uanachama kwa mujibu wa kifungu 3.25 cha katiba hii.
v. Kufukuzwa kwa sababu mbalimbali kama vile:
vi. Kujiondoa kwa hiari yake mwenyewe kwa kuandikia kamati kuu ya chama barua.
vii. Kuondolewa au kufukuzwa uanachama na mkutano mkuu kwenye ngazi husika.
viii. Kutohudhuria mikutano mitatu (3) kwa mfululizo bila taarifa yoyote kuanzia ngazi ya kituo, kata na Wilaya hadi Mkoa
ix. Kutokutoa ada kwa muda wa miezi mitatu mfululizo kwa makusudi.
x. kubainika kuwa ni mwizi.
xi. Ubakaji/ulawiti.
xii. Uuzaji na utumiaji wa madawa ya kulevya ndani kituo.

(a) Mwanachama ambaye kazi yake ya kufanya biashara ya bodaboda imekoma atatarifu kituo chake cha kazi ambapo viongozi wa kituo wataliondoa jina lake kwenye orodha ya wanachama na kutia muhuri kwenye kadi yake kuthibitisha kuwa alitimiza masharti yaliyomo katika katiba na kutunukiwa cheti maalum cha chama na kamati kuu ya Mkoa.

(b) Mtu yeyote ambaye uanachama wake umekoma hatakuwa na haki wala wajibu wowote katika chama.

**Kufukuzwa uanachama.**

(a) Mwanachama yeyote anaweza kufukuzwa katika chama iwapo mamlaka husika itathibitisha kwamba,

(i) Amejipatia uanachama kwa njia ya udanganyifu.

(ii) Amekosa uaminifu, amefuja na/au kupoteza Mali na fedha za chama.

(iii) Ana uanachama wa chama kingine tofauti na **UBOMA.**

(iv) Amefanya vitendo vinavyopinga katiba ya chama au maamuzi ya mkutano mkuu.

(v) Amekosa uzalendo, utii na amekisaliti chama katika migogoro ya kazi.

(vi) Akikaidi kutekeleza uamuzi wa kamati ya nidhamu na maadili au uamuzi wa kamati ya rufaa kwa zaidi ya miezi mitatu.

(vii) Endapo akikaa bila kulipa ada ya umoja au kituo kwa muda wa miezi mitatu.

**Utaratibu wa kumfukuza mwanachama utakuwa kama ufuatao:**

01. Uongozi wa kituo baada ya majadiliano na mwanachama mtuhumiwa, watatoa maelezo kwa maandishi kwa uongozi wa bodaboda kata wakipendekeza adhabu, hatua zinazositahili kuchukuliwa dhidi ya mtuhumiwa.

02. Uongozi wa kata utajadili tuhuma dhidi ya mwanachama husika na ukiamua kumfukuza uanachama ndani ya kituo hicho utapeleka taarifa kwa maandishi kwa uongozi wa chama ngazi ya wilaya na nakala kwenda Mkoa wakipendekeza kufukuzwa uanachama mtuhumiwa huyo.

03. Kamati kuu ya chama Mkoa itazipitia tuhuma zilizopokelewa na ukikubali mapendekezo yaliyotolewa na kata na wilaya utawasilisha jina la mwanachama mtuhumiwa kwa uamuzi wa mwisho.

04. Mwanachama anayependekezwa kufukuzwa kwenye chama anayo haki ya kujulishwa tuhuma zinazomkabili, kukata rufaa, kutoa na kusikilizwa utetezi wake katika ngazi zote husika hadi uamuzi wa mwisho utakapotolewa.

**Vile vile utaratibu wa kumusimamisha kazi mwanachama mwenye utovu wa nidhamu ndani ya kituo chake utakuwa kama ifuatavyo:**

01. Uongozi wa kituo baada ya majadiliano na mwanachama mtuhumiwa, watatoa maelezo kwa maandishi kwa uongozi wa bodaboda kata wakipendekeza adhabu, hatua zinazositahili kuchukuliwa dhidi ya mtuhumiwa.
02. Uongozi wa kata utajadili tuhuma dhidi ya mwanachama husika na uongozi wa kata unaweza kuamua kumpa adhabu. ndogondogo mwanachama huyo au ukaamua kumusimamisha kazi kwa muda mpaka atakapojirekebisha au pengine ukaamua kumpiga faini kwa mujibu wa katiba ya chama.
03. Baada ya maamuzi hayo kwa mwanachama uongozi wa kata utatoa taarifa kwenye kituo cha mwanachama huyo kwa maamuzi yaliyoafikiwa.
04. Mwanachama anayependekezwa kusimamishwa kazi kwenye kituo ndani ya chama anayo haki ya kujulishwa tuhuma zinazomkabili, kukata rufaa, kutoa na kusikilizwa utetezi wake katika ngazi zote husika hadi uamuzi wa mwisho utakapotolewa.

**Mwanachama kuhamia kata au wilaya nyingine ndani ya Mkoa.**

Mwanachama anaweza kuhamia kata nyingine au wilaya iwapo:

(a) Amehamishia makazi yake ya kudumu katika kata hiyo au wilaya hiyo na hataki kuendelea kufanya kazi alipokuwa akifanyia mwanzo.

(b) Kuna sababu za umbali kutoka kwenye kituo chake cha kazi na kwenda nyumbani kwake.

(c) Uongozi wa kituo husika mwanachama anachotoka utampa barua ya utambulisho inayoonyesha taarifa halisi za mwanachama huyo ikiwepo michango mbalimbali ya chama na kutoa idhini kwa mwanachama huyo kupokelewe kwenye kituo kingine huko anakohamia na kufuata utaratibu wa kituo kipya cha kazi.

(d) Mwanachama anayehamia kituo kingine kwasababu zilizoanishwa kwenye kifungu cha katiba 3.26 (a na b) hatalipishwa kiingilio huko anakohamia kwani alikuwa mwanachama cha msingi awe ni mwanachama hai kwa mujibu wa katiba hii.

(e) Endapo atakuta kituo hicho kina mfuko kwa mujibu wa katiba hii atalazimika kuchanga fedha hiyo ili aweze kueendana na wanachama wengine ndani ya kituo hicho lakini pia atapewa muda wa kulipa kidogokidogo kutokana na mfuko huo.

(f) Mwanachama huyo atakapokuwa amemaliza fedha hiyo ya mfuko wa kituo atakuwa na haki ya kuhudumiwa kwa mujibu wa katiba hii.

# SURA YA NNE:

## 4.0 VIKAO VYA CHAMA NGAZI YA KITUO:

4.1. Kikao cha mwanzo kabisa cha **UBOMA** kitakuwa ni kikao cha kituo.

4.2. Hapa ndipo kila mwanachama atadhihirisha uanachama wake kwa vitendo wajibu wake wa uanachama.

a. Wajumbe wa mkutano mkuu wa kituo watakuwa ni wanachama wote wa kituo Husika**.**
b. Viongozi wote ndani ya kituo.
c. Vikao vya kituo vitafanyika mara sita (06) kwa mwaka.
d. Vitafanyika mwezi wa February, April, Juni, August, October, December na vitafanyika mwisho wa kila mwezi.

## MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA KITUO:

i. Kiunganishi cha wanaumoja walioko kwenye Kituo mpaka Mkoa kwa kuhimiza mahudhurio katika vikao mbalimbali vya umoja.
ii. Kuchagua viongozi wa kituo.
iii. Kuhimiza ulipaji wa michango mbalimbali na ada za umoja
iv. Kuainisha kero mbalimbali katika umoja na wanaumoja hasa kuhusiana na mwenendo wa uendeshaji na usimamizi wa maswala ya umoja.
v. Kutafakari juu ya uongozi wa umoja ndani ya vituo, kata, wilaya husika ili kama kuna maoni ya kuboresha yawakilishwe kwa katibu mkuu wa umoja ngazi ya Mkoa kwa maandishi.
vi. Kutambua wanachama wapya walioingia kwenye vituo ndani ya kituo husika.
vii. Kwa kushirikiana na kamati kuu ya kata,wilaya, Mkoa na kusimamia nidhamu ya wanaumoja kwenye kata husika
viii. Kuhimiza wanaumoja kwenye kituo kwa mujibu wa katiba hii, kuhudhuria vikao vya umoja na matukio mbalimbali ya umoja ikiwa ni pamoja na matukio ya kiserikali na taasisi nyingine.
ix. Kuhakikisha kuwa wanachama walioko kwenye kata hawafanyi jambo lolote linalopingana na katiba ya umoja na kanuni, maamuzi na maelekezo ya kamati kuu, halmashauri kuu, mkutano mkuu au viongozi wakuu wa umoja.
x. Kujadili mwenendo na tabia ya mwanachama katika kituo husika.

**MAJUKUMU YA VIONGOZI WA KITUO:**

i. Viongozi wa kituo watawajibika kuitisha vikao kwa wanachama wao ili kuwapatia mrejesho na miongozo ya kikatiba kutoka kwenye vikao vya kata, wilaya na Mkoa.
ii. Viongozi wa vituo watawajibika kukusanya michango ya kikatiba kwa wanachama wao.
iii. Viongozi wa kituo watawajibika kusimamia amani kwa wanachama wao ndani ya kituo chao.

4.3. Viongozi wa kituo watawajibika kujua taarifa za kila mwanachama kwenye kituo chao ikiwa ni pamoja na:

i. Barua ya utambulisho kutoka kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa eneo analotokea.
ii. Kuwa na leseni ya udereva.
iii. Awe na akili timamu.
iv. Awe na umri usiopungua miaka 18 na kuendelea.
v. Awe na afya bora na asiwe anatumia kilevi chochote kama pombe, bangi, mirungi, sigara, pindi awapo eneo la kazi.
vi. Taarifa za mwanachama mpya ziende ngazi ya kituo anachoenda kufanyia kazi, kata kilipo kituo, kisha wilaya na endapo itabainika mwanachama mpya ameingia bila taarifa kupita ngazi ya kata ama wilaya uongozi wa kituo husika utawajibika.
vii. Kudhibiti kelele za exosit ( Tramper) na taa zenye mwanga mkali (Sport light).
viii. Ni marufuku mwanachama yeyote ndani ya kituo kuharibu mfumo wowote wa pikipiki, kuitoa kutoka kwenye uhalisia wake na kuibadirisha anavyotaka yeye.
ix. Kuhakikisha kuwa mwanachama hatoi lugha za matusi kwa abiria, mwanachama mwenzake au kwa majirani walioko karibu na kituo
x. Ni marufuku kwa kituo chochote kupokea fedha mkononi za mwanachama mpya/faini na michango yoyote inayotambulika kikatiba.
xi. Ni lazima kila kituo kuwa na akaunti ya benki.
xii. Ni lazima wanachama wasomewe taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi mitatu kwenye kituo husika.
xiii. Ni marufuku kwa mwanachama kuendesha pikipiki akiwa hana helmet (kofia ngumu) na kiakisi mwanga (reflector) chenye namba ya uanachama wake.
xiv. Ni lazima mwendesha bodaboda kuwa msafi wa mwili, mavazi, chombo anachoendesha, mazingira anakofanyia kazi.
xv. Ni lazima wanachama kushiriki shughuli mbalimbali za kiserikali na za kijamii pale itakapohitajika kufanya hivyo.
xvi. Ni marufuku kuweka plate namba isiyotambulika kiserikali, kuikunja, kuichora au kufuta baadhi ya namba ambazo zimewekwa kwenye plate namba hiyo.

xvii. Ni marufuku kupiga norinda na kuinua pikipiki juu ndani ya kituo cha kazi.

## VIKAO VYA CHAMA NGAZI YA KATA:

4.4. Kutakuwa na vikao vya bodaboda katika kila kata na wajumbe wake watakuwa ni:

a) Kamati kuu ya kata ( Viongozi wote wa kata wa kuchaguliwa).
b) Halmashauri kuu ya kata ( Viongozi wote wa vituo wa kuchaguliwa).
c) Mkutano mkuu wa kata (Wanachama wote wa vituo ndani ya kata).

## KAMATI KUU YA KATA.

a) Kamati kuu ya kata itakaa vikao vyake mara tatu (03) kwa mwaka kama ifuatavyo; Mwezi wa Marchi, julai, Novemba, na vitafanyika mwisho wa kila mwezi.
b) Wajumbe wa kamati hiyo wanaweza kufanya vikao vya dharura wakati wowote endapo itahitajika kufanya hivyo.

## MAJUKUMU YA KAMATI KUU YA KATA:

i. Kuhakikisha kunakuwepo umoja na mshikamano wa wanachama wote ndani ya kata husika.
ii. Kusimamia maendeleo na kutoa miongozo ya kiutendaji kwenye vituo ndani ya kata husika.
iii. Kusimamia utekelezaji wa kanuni, katiba na kuhakikisha ustawi wa umoja kwa ujumla.
iv. Kuratibu shughuli za kila siku za umoja ndani ya kata.
v. Kupokea wanachama wapya wanaojiunga kwenye vituo ndani ya kata husika.
vi. Kusimamia mapato na matumizi kwenye vituo ndani ya kata.
vii. Kusimamia nidhamu kwa wanachama ndani ya vituo vya kata husika katika utaratibu tuliojiwekea.
viii. Kuhamasisha ulipaji wa ada na michango mbalimbali kwa wanachama ndani ya kata.
ix. Kutoa taarifa kwa wanachama ndani ya kata husika ilimradi taarifa hizo haziathiri malengo na madhumuni ya umoja.
x. Kumwongezea majukumu madogomadogo kiongozi yeyote kwa jinsi itakavyoona inafaa ili akaimu nafasi ya kiongozi ambayo iko wazi au mwenye kuishikilia ana udhuru unaomfanya asiweze kutekeleza majukumu yake. Baada ya kumwongezea majukumu kiongozi kamati kuu itawajulisha wanachama ndani ya kituo husika.
xi. Kusimamia uchaguzi wa vituo vyote ndani ya kata husika.
xii. Kufanya ziara kwenye vituo ndani ya kata kwa ajili kuimarisha umoja kwa kusikiliza kero mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi.

xiii. Kumsimamisha kiongozi yoyote ndani ya kituo na kufanya uchunguzi endapo atabainika kuwa na tuhuma zozote dhidi yake na kumkaimisha mwanachama mwingine kati yao kuchukua nafasi yake mpaka uchunguzi utakapokamilika.

## HALMASHAURI KUU YA KATA:

a. Wajumbe wa halmashauri kuu ya Bodaboda kata ni viongozi wote wa vituo vya kata husika.
b. Halmashauri kuu ya kata itakuwa na vikao viwili (02) kwa mwaka, yaani mwezi juni na Decemba lakini kikao kinaweza kufanyika muda wowote endapo kutakuwa na dharura ya kufanya hivyo.

## MAJUKUMU YA HALMASHAURI KUU YA KATA:

a) Halmashauri kuu ya kata ni chombo ambacho kitapokea mapendekezo yaliyojadiliwa na kamati kuu ya kata kwa ajili ya uwajibikaji wa pamoja (collective responsibility) na uhifadhi wa siri za vikao.
b) Halmashauri wanawajibika kulinda na kutetea maamuzi yaliyoafikiwa na kikao hata kama kuna mjumbe asiyeunga mkono maamuzi hayo ilimradi maamuzi wanayoyatetea siyo kinyume cha katiba hii na hayalengi kuzuia haki kutendeka.
c) Hayakiuki misingi ya umoja na mshikamano katika umoja.
d) Hayana misingi ya ubaguzi.

## MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA KATA:

**Mkutano mkuu wa kata ni chombo cha maamuzi ya mwisho ndani ya kata**

i. Wajumbe wa mkutano mkuu wa kata watakuwa ni wanachama wote wa Bodaboda kata husika.
ii. Mkutano mkuu wa kata utafanyika mara moja (01) kwa mwaka, lakini unaweza kufanyika wakati wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo.
iii. Kupokea na kujadili taarifa ya kamati kuu kata juu ya hali ya umoja vituo na kamati za kikatiba ndani ya kata husika.

iv. Kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka ndani ya kata husika. .
v. Kutoa muhtasari wa shughuli zote ndani ya kata na maamuzi/majukumu, kuletwa ngazi ya wilaya.
vi. Kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali mbalimbali za chama ngazi ya kata.
vii. Kumsimamisha kiongozi yeyote au mwanachama yeyote anayetuhumiwa kukiuka Katiba na maadili ya chama na baada ya kupitia kwa kina tuhuma hizo na kumpa mtuhumiwa haki ya kusikilizwa na kuwasilisha mapendekezo mbele ya mkutano mkuu.
viii. Kujadili maswala ya jumla yatakayozingatiwa na kamati kuu wakati wa kuandaa taarifa itakayowasilishwa na kamati kuu kwenye mkutano mkuu.
ix. Kuwa kiunganishi cha wanaumoja walioko kwenye vituo na wale wa umoja mkubwa, kwa kuhimiza mahudhurio katika vikao mbalimbali vya umoja.
x. Kuhimiza ulipaji wa michango mbalimbali na ada za umoja.
xi. Kuainisha kero mbalimbali katika umoja na wanaumoja hasa kuhusiana na mwenendo wa uendeshaji na usimamizi wa maswala ya umoja.
xii. Kutafakari juu ya uongozi wa umoja ndani ya vituo kwenye kata husika ili kama kuna maoni ya kuboresha yawasilishwe kwa katibu mkuu wa umoja ngazi ya Wilaya kwa maandishi.
xiii. Kutambua wanachama wapya walioingia kwenye vituo ndani ya kata husika.
xiv. Kushirikiana na kamati kuu ya wilaya, kusimamia nidhamu ya wanaumoja kwenye kata husika.
xv. Kuhimiza wanaumoja kwenye kata kwa mujibu wa katiba hii.
xvi. Kuhudhuria vikao vya umoja na matukio mbalimbali ya umoja ikiwa ni pamoja na matukio ya kiserikali na taasisi nyingine.
xvii. Kuhakikisha kuwa wanachama walioko kwenye kata hawafanyi jambo lolote linalopingana na katiba, kanuni, maamuzi na maelekezo ya kamati kuu, halmashauri kuu, mkutano mkuu au viongozi wakuu wa umoja.

## VIKAO VYA CHAMA NGAZI YA WILAYA:

Kutakuwa na vikao vya bodaboda katika kila wilaya na wajumbe wake watakuwa ni:

a) Kamati kuu ya wilaya (Viongozi wote wa wilaya wa kuchaguliwa).
b) Halmashauri kuu ya wilaya (Viongozi wote wa kila kata ndani ya wilaya husika).
c) Mkutano mkuu wa wilaya (Viongozi wote wa vituo wa kuchaguliwa ndani ya wilaya husika).

**Kamati kuu ya wilaya:**

Kamati kuu ni chombo cha utekelezaji wa maswala yote yatakayopitishwa halmashauri kuu ya wilaya na mkutano mkuu wa umoja ngazi ya wilaya.

a) Kamati kuu ya wilaya itakaa vikao vyake mara tatu (03) kwa mwaka kama ifuatavyo; Mwezi wa Marchi, julai, Novemba, na vitafanyika mwisho wa kila mwezi.
b) Wajumbe wa kamati hiyo wanaweza kufanya vikao vya dharura wakati wowote endapo itahitajika kufanya hivyo.

## MAJUKUMU YA KAMATI KUU YA WILAYA:

Kamati kuu ya wilaya itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kuhakikisha panakuwepo na umoja na mshikamano wa wanachama ndani ya wilaya husika.
ii. Kusimamia maendeleo na kutoa miongozo ya kiutendaji kwenye kata, vituo na kamati za kikatiba.
iii. Kusimamia utekelezaji wa kanuni, katiba na kuhakikisha ustawi wa umoja kwa ujumla.
iv. Kuratibu shughuli za kila siku za umoja.
v. Kupokea wanachama wapya wanaojiunga na umoja.
vi. Kusimamia mapato na matumizi kwenye kata na vituo.
vii. Kusimamia nidhamu kwa wanachama katika utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa katiba hii.
viii. Kuhamasisha ulipaji wa ada na michango mbalimbali kwa wanachama.
ix. Kutoa taarifa kwa wanachama ilimradi taarifa hizo haziathiri malengo na madhumuni ya umoja.
x. Kufuatilia masuala, maamuzi na maandalizi yanayopaswa kufanywa kwa ajili ya chama katika sehemu mbalimbali ikiwemo serikalini, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi zingine.
xi. Kumwongezea majukumu madogomadogo kiongozi yeyote kwa jinsi itakavyoona inafaa ili akaimu nafasi ya kiongozi ambayo iko wazi au mwenye kuishikilia anaudhuru unaomfanya asiweze kutekeleza majukumu yake. Baada ya kumwongezea majukumu kiongozi kamati kuu itawajulisha wanachama eidha kupitia viongozi wa kata au mkutano mkuu.
xii. Kwa kushirikiana na kamati ya fedha na uchumi ili kubuni na kuibua fursa mbalimbali za maendeleo ya umoja ikiwa ni pamoja na:

xiii. Kutathimini maendeleo ya umoja kiuchumi.
xiv. Kuchukua hatua kwa nia ya kujikwamua au kujitegemea kiuchumi.
xv. Kushughulikia maswala yanayohusiana na nidhamu kwa wanachama.
xvi. Kusimamia uwajibikaji kwenye umoja.
xvii. Kusimamia viongozi wa kata na vituo.
xviii. Kusimamia viongozi wa kamati za kikatiba.
xix. Kupanga na kusimamia shughuli zote za chama ndani ya wilaya.

**Kupanga kalenda ya vikao vyote vya chama ikiwa ni pamoja na:**

a. Vikao vya mkutano mkuu wa chama ndani ya wilaya.
b. Vikao vya bodi ya Wadhamini.
c. Vikao vya kamati Kuu.
d. Vikao vya halmashauri kuu na
e. Mikutano mingineyo kama itakavyoonekana inafaa.
f. Kupanga mikakati ya uchaguzi katika wilaya.
g. Kuziongoza halmashauri za kata zote kila kata.

## HALMASHAURI KUU YA WILAYA:

4.13. Halmashauri kuu ni chombo ambacho kitapokea mapendekezo yaliyojadiliwa na kamati kuu

4.14. Halmashauri kuu ya wilaya itakuwa na vikao viwili (02) kwa mwaka, yaani mwezi Juni na Decemba lakini kikao kinaweza kufanyika muda wowote endapo kutatokea dharura ya kufanya hivyo.

## MAJUKUMU YA HALMASHAURI YA WILAYA:

**Halmashauri ya Umoja itakuwa na majukumu yafuatayo:**

i. Kupokea na kujadili taarifa ya kamati kuu juu ya hali ya umoja katika ngazi ya kata, vituo na kamati za kikatiba.
ii. Kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka.
iii. Kutekeleza maamuzi yatakayotolewa na mkutano mkuu wa wilaya.
iv. Kupokea ushauri utakaotolewa na Bodi ya wadhamini au mlezi wa chama ndani ya wilaya.
v. Kuunda Idara za Taasisi kutegemeana na mahitaji kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali mahususi za chama kama idara ya (Mipango na fedha, sheria na usalama barabarani, elimu, michezo na burudani, uchaguzi, nidhamu na idara nyingine kutokana

na mahitaji ya taasisi) kamati itaandaa kanuni na wajumbe wa kamati zote zitakazo ainishwa.

vi. Kupitisha na kupendekeza mambo na taarifa mbalimbali zinazohusu hali na ustawi wa usalama barabarani ndani ya wilaya.

vii. Kutoa muhtasari wa shughuli zote na maamuzi na majukumu yaliyopaswa kutekelezwa mbele ya kamati kuu.

viii. Kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali mbalimbali za chama.

ix. Kupendekeza jina la mkaguzi wa hesabu na kuliwasilisha mbele ya wajumbe wa mkutano mkuu wa chama ili kuidhinishwa.

x. Kumsimamisha au kumfukuza kiongozi yeyote au mwanachama yeyote anayetuhumiwa kukiuka katiba na maadili ya chama kwa mujibu wa katiba na baada ya kupitia kwa kina tuhuma hizo na kumpa mtuhumiwa haki ya kusikilizwa na kuwasilisha mapendekezo mbele ya mkutano mkuu umfukuze uongozi au imrejeshee uongozi mtuhumiwa.

xi. Baada ya maamuzi hayo kufanyika nakala itapelekwa kwenye uongozi wa bodaboda Mkoa.

xii. Kujadili maswala ya jumla yatakayozingatiwa na kamati kuu wakati wa kuandaa taarifa itakayowasilishwa na kamati kuu kwenye mkutano mkuu.

xiii. Kujadili na kupitisha kanuni mbalimbali za umoja ambazo zitawezesha utekelezaji bora wa katiba.

xiv. Kwa minajili ya uwajibikaji wa pamoja (Collective responsibility) na uhifadhi wa siri za vikao/wajumbe wa halmashauri wanawajibika kulinda na kutetea maamuzi yaliyofikiwa hata Kama kuna mjumbe asiyeunga mkono maamuzi hayo ilimradi maamuzi wanayoyatetea siyo kinyume cha katiba hii.

## MKUTANO MKUU WA WILAYA:

4.25. Mkutano mkuu utakuwa ni mkutano wa viongozi wote wa vituo na kata wa kuchaguliwa ndani ya wilaya.

i. Mkutano mkuu huo ndio chombo cha juu kabisa cha maamuzi katika umoja ndani ya wilaya.

ii. Mkutano mkuu utafanyika mara moja (01) kwa mwaka mwanzo wa mwezi Decemba.

iii. Akidi ya mkutano mkuu itakuwa ni 75% ya wajumbe wote wa umoja.

iv. Mkutano mkuu wa dharura utaitishwa kwa uamuzi wa halmashauri kuu (viongozi wa kata) endapo kutakuwepo na jambo lolote la dharura linalohitaji uamuzi wa mkutano mkuu au kwa maagizo ya uongozi wa juu.

v. Akidi ya mkutano mkuu wa dharura itakuwa ni 40% ya wajumbe wote wa umoja.
vi. Mkutano mkuu utaanza saa 3 asubuhi na kumalizika saa 10 jioni.
vii. Kwa ridhaa ya wajumbe walio wengi dk 15 kabla ya muda wa kawaida wa kikao kuisha mwenyekiti wa mkutano anaweza kuongeza dakika hadi dk 30 kumalizia agenda zilizobaki.

## MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA WILAYA:

4.26. Mkutano mkuu utakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Kupokea na kujadili taarifa ya hali ya umoja ngazi ya kituo, kata hadi wilaya kwa kipindi cha mwaka mmoja.
ii. Kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka.
iii. Kupokea taarifa ya kiutendaji ndani ya mwaka
iv. Kutoa maelekezo, madaraka kwa halmashauri na kamati kuu kwa maswala mahususi kadri utakavyoona inafaa ilimradi isiwe kinyume ya katiba ya umoja.
v. Wajumbe watakaochagua viongozi ngazi ya wilaya ni wajumbe wa mkutano mkuu.
vi. Kupitisha marekebisho ya katiba ya umoja.
vii. Viiongozi waliochaguliwa ( au uongozi mzima) wanaweza kuondolewa madarakani kabla ya kutimiza miaka (5) iwapo itatokea asilimia 75% ya wanachama wote wa ngazi husika watadai kwa maandishi na kutia saini zao kuitishwa kwa mkutano mkuu maalum kwa sababu ya upungufu wa kiongozi/makosa ( au uongozi mzima). na katibu mara tu atakapopata madai hayo, atatoa taarifa ndani ya siku kumi na nne (14) ya kuitisha mkutano mkuu maalumu ambao utajadili hoja za wanachama walioitisha mkutano huo na hawezi kuendelea na madaraka yake, basi ataondolewa na mkutano huo na nafasi yake itajazwa na mkutano huo. Ila tu kiongozi hataondolewa madarakani bila kupewa fursa ya kujitetea.
viii. Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za chama iliyotolewa na halmashauri kuu ya umoja ndani wilaya,na kutoa maelekezo ya utekelezaji wa chama kwa kipindi kijacho.
ix. Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi za juu yanatekelezwa ipasavyo.
x. Kuzungumzia mambo yote yanayohusu ulinzi, usalama na maendeleo kwa ujumla katika wilaya.
xi. Unapofika wakati wa uchaguzi mkutano mkuu wa chama wa wilaya utashughulikia mambo yafuatayo:
xii. Kumuchagua mwenyekiti wa wilaya.
xiii. Makamu mwenyekiti wilaya.

xiv. Katibu mkuu wilaya.
xv. Naibu katibu wilaya.
xvi. Mtunza hazina wilaya.
xvii. Mtunza nidhamu wilaya (kamanda wilaya).
xviii. Kuunda kamati za mkutano mkuu wa wilaya kwa kadri itakavyoonekana inafaa.
xix. Mkutano mkuu wa wilaya unaweza kukasimisha madaraka yake kwa halmashauri kuu ya wilaya kuhusu utekelezaji wa kazi zake kwa kadri utakavyoona inafaa.

## VIKAO VYA UMOJA NGAZI YA MKOA:

4.27. Kutakuwa na vikao vya bodaboda vya Mkoa na wajumbe wake watakuwa ni:
a. Kamati kuu ya Mkoa (Viongozi wote wa mkoa wa kuchaguliwa)
b. Halmashauri kuu ya Mkoa (Viongozi wote wa kila wilaya ndani ya Mkoa)
c. Mkutano mkuu wa Mkoa (Viongozi wote wa kata, wilaya na Mkoa wa kuchaguliwa).

4.28. Kamati kuu ya Mkoa ni chombo cha utekelezaji wa maswala yote yatakayopitishwa na halmashauri kuu ya mkoa na mkutano mkuu wa umoja ngazi ya Mkoa.
a) Kamati kuu ya Mkoa itakaa vikao vyake mara tatu (03) kwa mwaka kama ifuatavyo; Mwezi wa Marchi, julai, Novemba, na vitafanyika mwisho wa kila mwezi.
b) Wajumbe wa kamati hiyo wanaweza kufanya vikao vya dharura wakati wowote endapo itahitajika kufanya hivyo.

## MAJUKUMU YA KAMATI KUU YA MKOA:

4.29. Kamati kuu ya mkoa itakuwa na majukumu yafuatayo:
i. Kuhakikisha panakuwepo na umoja na mshikamano wa wanachama ndani ya Mkoa.
ii. Kusimamia maendeleo na kutoa miongozo ya kiutendaji kwenye vituo, kata, wilaya na kamati za kikatiba ndani ya Mkoa.
iii. Kusimamia utekelezaji wa kanuni, katiba na miongozo mbalimbali kuhakikisha ustawi wa umoja unaimarika.
iv. Kuratibu shughuli za kila siku za umoja ndani ya Mkoa.
v. Kupokea wanachama wapya wanaojiunga na umoja kwenye Mkoa.
vi. Kusimamia mapato na matumizi kwenye vituo, kata, wilaya na Mkoa.
vii. Kusimamia nidhamu kwa wanachama katika utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa katiba hii.

viii. Kuhamasisha ulipaji wa ada na michango mbalimbali kwa wanachama.
ix. Kuteua na kuajiri maafisa watendaji wa chama.
x. Kujadili taarifa za ukiukaji wa Katiba uliofanywa na mwanachama na kupendekeza hatua za kinidhamu dhidi ya kiongozi yeyote wa Chama.
xi. Kuunda kamati ya fedha na kamati nyininezo kadri itakavyoona inafaa.
xii. Kutoa taarifa kwa wanachama ilimradi taarifa hizo haziathiri malengo na madhumuni ya umoja.
xiii. Kufuatilia masuala, maamuzi na maandalizi yanayopaswa kufanywa kwa ajili ya chama katika sehemu mbalimbali ikiwemo serikalini, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi zingine.
xiv. Kumwongezea majukumu madogomadogo kiongozi yeyote kwa jinsi itakavyoona inafaa ili akaimu nafasi ya kiongozi ambayo iko wazi au mwenye kuishikilia anaudhuru unaomfanya asiweze kutekeleza majukumu yake.
xv. Kuandaa agenda za mkutano wa halmashauri kuu ya Mkoa.

4.30. Baada ya kumwongezea majukumu kiongozi kamati kuu itawajulisha wanachama eidha kupitia viongozi wa kata au mkutano mkuu.

a) Kwa kushirikiana na kamati ya fedha na uchumi ili kubuni na kuibua fursa mbalimbali za maendeleo ya umoja ikiwa ni pamoja na:
b) Kutathimini maendeleo ya umoja kiuchumi.
c) Kushughulikia maswala yanayohusiana na nidhamu kwa wanachama.
d) Kusimamia uwajibikaji kwenye umoja.
e) Kusimamia viongozi wa vituo, kata na wilaya.
f) Kusimamia viongozi wa kamati za kikatiba za ngazi zote.
g) Kupanga na kusimamia shughuli zote za chama ndani ya mkoa.

4.31. Kupanga kalenda ya vikao vyote vya chama ikiwa ni pamoja na:

a) Vikao vya mkutano mkuu wa chama ndani ya Mkoa.
b) Vikao vya bodi ya Wadhamini.
c) Vikao vya kamati Kuu.
d) Vikao vya halmashauri kuu na
e) Mikutano mingineyo ka
f) ma itakavyoonekana inafaa.
g) Kupanga mikakati ya uchaguzi katika wilaya.
h) Kuziongoza halmashauri za wilaya zote ndani ya Mkoa.

## HALMASHAURI KUU YA MKOA:

4.32. Halmashauri kuu ya mkoa ni chombo ambacho kitapokea mapendekezo yaliyojadiliwa na kamati kuu au mkutano mkuu wa Mkoa.

a) Halmashauri kuu ya Mkoa itakuwa na vikao viwili (02) kwa mwaka, yaani mwezi Juni na Decemba mwanzo wa kila mwezi.

b) Lakini kikao kinaweza kufanyika muda wowote endapo kutatokea dharura ya kufanya hivyo.

## MAJUKUMU YA HALMASHAURI KUU YA MKOA:

i. Kupokea na kujadili taarifa ya kamati kuu juu ya hali ya umoja katika Mkoa.

ii. Kuongoza na kusimamia ujenzi wa chama katika Mkoa.

iii. Kutoa msukumo wa utekelezaji wa katiba ya umoja na kusimamia utekelezaji wamaazimio yaliyopitishwa na mkutano mkuu wa Mkoa.

iv. Kupokea, kuzingatia na kuamua juu ya mapendekezo ya vikao vya chama vilivyo chini yake.

v. Kuziongoza halmashauri kuu za umoja za wilaya katika njia zinazofaa za kuimarisha umoja na kuleta maendeleo katika Mkoa.

vi. Kuangalia mwenendo na vitendo vya wanachama na viongozi wa umoja katika Mkoa na inapolazimu kutoa taarifa kwa vikao vinavyohusika.

vii. Kufikisha maazimio na maagizo ya vikao kwa ngazi za chini yake.

viii. Kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka.

ix. Kutekeleza maamuzi yatakayotolewa na mkutano mkuu wa mkoa.

x. Kupokea ushauri utakaotolewa na Bodi ya wadhamini au mlezi wa chama ndani ya Mkoa.

xi. Kuunda Idara za Taasisi kutegemeana na mahitaji kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali mahsusi za chama kama idara ya (Mipango na fedha, sheria na usalama barabarani, elimu, michezo na burudani, uchaguzi, nidhamu na idara nyingine kutokana na mahitaji ya taasisi) kamati itaandaa kanuni na wajumbe wa kamati zote zitakazo ainishwa.

xii. Kupitisha na kupendekeza taarifa mbalimbali zinazohusu hali na ustawi wa usalama barabarani ndani ya Mkoa.

xiii. Kutoa muhtasari wa shughuli zote na maamuzi na majukumu yaliyopaswa kutekelezwa mbele ya kamati kuu.

xiv. Kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali mbalimbali za chama ndani ya Mkoa.

xv. Kupendekeza jina la mkaguzi wa hesabu na kuliwasilisha mbele ya wajumbe wa mkutano mkuu wa chama ili kuidhinishwa.

xvi. Kumsimamisha au kumfukuza kiongozi yeyote au mwanachama yeyote anayetuhumiwa kukiuka katiba na maadili ya chama kwa mujibu wa katiba na baada ya kupitia kwa kina tuhuma hizo na kumpa mtuhumiwa haki ya kusikilizwa na kuwasilisha mapendekezo mbele ya mkutano mkuu wa mkoa umfukuze uongozi au imrejeshee uongozi mtuhumiwa.

xvii. Baada ya maamuzi hayo kufanyika nakala itapelekwa kwenye uongozi wa bodaboda Mkoa.

xviii. Kujadili maswala ya jumla yatakayozingatiwa na kamati kuu wakati wa kuandaa taarifa itakayowasilishwa na kamati kuu kwenye mkutano mkuu wa Mkoa

xix. Kujadili na kupitisha kanuni mbalimbali za umoja ambazo zitawezesha utekelezaji bora wa katiba.

xx. Kwa minajili ya uwajibikaji wa pamoja (Collective responsibility) na uhifadhi wa siri za vikao wajumbe wa halmashauri wanawajibika kulinda na kutetea maamuzi yaliyofikiwa hata Kama kuna mjumbe asiyeunga mkono maamuzi hayo ilimradi maamuzi wanayoyatetea siyo kinyume cha katiba hii.

## MKUTANO MKUU WA MKOA:

4.33. Mkutano mkuu wa Mkoa utakuwa ni mkutano wa viongozi wote wa kata, wilaya na Mkoa wa kuchaguliwa ndani ya Mkoa. Mkutano mkuu huo ndio chombo cha juu kabisa cha maamuzi katika umoja ndani ya Mkoa.

i. Mkutano mkuu utafanyika mara moja (01) kwa mwaka mwanzo wa mwezi Decemba.

ii. Akidi ya mkutano mkuu itakuwa ni 75% ya wajumbe wote wa umoja.

iii. Mkutano mkuu wa dharura utaitishwa kwa uamuzi wa halmashauri kuu (viongozi wa wilaya) endapo kutakuwepo na jambo lolote la dharura linalohitaji uamuzi wa mkutano mkuu au kwa maagizo ya uongozi wa juu.

iv. Akidi ya mkutano mkuu wa dharura itakuwa ni 40% ya wajumbe wote wa umoja.

v. Mkutano mkuu utaanza saa 3 asubuhi na kumalizika saa 10 jioni.

vi. Kwa ridhaa ya wajumbe waliowengi dk 15 kabla ya muda wa kawaida wa kikao kuisha mwenyekiti wa mkutano anaweza kuongeza dakika hadi dk 30 kumalizia agenda zilizobaki.

## MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA MKOA:

4.34. Mkutano mkuu wa Mkoa utakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Kupokea na kujadili taarifa ya hali ya umoja ngazi ya, kata, wilaya kwa kipindi cha mwaka mmoja.
ii. Kupokea na kujadili taarifa ya fedha kwa kipindi cha mwaka.
iii. Kupokea taarifa ya kiutendaji ndani ya mwaka
iv. Kutoa maelekezo, madaraka kwa halmashauri na kamati kuu kwa maswala mahususi kadri utakavyoona inafaa ilimradi isiwe kinyume ya katiba ya umoja.
v. Wajumbe watakaochagua viongozi ngazi ya Mkoa ni wajumbe wa mkutano mkuu.
vi. Kupitisha marekebisho ya katiba ya umoja.
vii. Viiongozi waliochaguliwa ( au uongozi mzima) wanaweza kuondolewa madarakani kabla ya kutimiza miaka (5) iwapo itatokea asilimia 75% ya wanachama wote wa ngazi husika watadai kwa maandishi na kutia saini zao kuitishwa kwa mkutano mkuu maalum kwa sababu ya upungufu wa kiongozi/makosa ( au uongozi mzima) na katibu mara tu atakapopata madai hayo, atatoa taarifa ndani ya siku kumi na nne (14) ya kuitisha mkutano mkuu maalumu ambao utajadili hoja za wanachama walioitisha mkutano huo na hawezi kuendelea na madaraka yake, basi ataondolewa na mkutano huo na nafasi yake itajazwa na mkutano huo. Ila tu kiongozi hataondolewa madarakani bila kupewa fursa ya kujitetea.
viii. Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za chama iliyotolewa na halmashauri kuu ya umoja ndani wilaya, na kutoa maelekezo ya utekelezaji wa chama kwa kipindi kijacho.
ix. Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi za juu yanatekelezwa ipasavyo.
x. Kuzungumzia mambo yote yanayohusu ulinzi, usalama na maendeleo kwa ujumla katika Mkoa.
xi. Unapofika wakati wa uchaguzi mkutano mkuu wa chama wa Mkoa utashughulikia mambo yafuatayo,
xii. Kumchagua mwenyekiti wa Mkoa.
xiii. Makamu mwenyekiti Mkoa.
xiv. Katibu mkuu Mkoa.
xv. Naibu katibu Mkoa.
xvi. Mtunza hazina Mkoa.
xvii. Mtunza nidhamu Mkoa.
xviii. Kuunda kamati za mkutano mkuu wa Mkoa kwa kadri itakavyoonekana inafaa.
xix. Mkutano mkuu wa Mkoa unaweza kukasimisha madaraka yake kwa halmashauri kuu ya Mkoa kuhusu utekelezaji wa kazi zake kwa kadri utakavyoona inafaa.

# SURA YA TANO:

## 5.1. MUUNDO WA UONGOZI;

Kutakuwa na muundo wa uongozi wa chama Mkoa ambao utakuwa na wajibu wa kuelekeza shughuli za kila siku chini ya usimamizi wa kamati kuu ya Mkoa muundo huo utakuwa Kama ifuatavyo:

a. Viongozi wa vituo.
b. Viongozi wa kata.
c. Viongozi wa wilaya.
d. Viongozi wa Mkoa na
e. Kamati mbalimbli za kikatiba.

## 5.2. VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA KITUO:

Viongozi wa kituo watakuwa ni:

a) Mwenyekiti.
b) Makamu mwenyekiti.
c) Katibu.
d) Naibu katibu.
e) Mhasibu/au mweka hazina.
f) Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu.
g) Mtunza nidhamu msaidizi.

## 5.3. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA KITUO:

Mwenyekiti wa kituo atachaguliwa miongoni mwa wanachama hai na atafanya kazi zifuatazo:

i. Mwenyekiti ndiye kiongozi wa chama ngazi ya kituo.
ii. Atasimamia na Kufuatilia shughuli zote za chama za kiutawala akisaidiana na viongozi. Wengine waandamizi kwenye kituo husika.
iii. Ataitisha vikao vyote viwe vya dharura au vya kikatiba akishirikiana na katibu wake.
iv. Kuendesha na kusimamia vikao vyote vya mikutano ya kituo kwa haki na kwa utulivu.
v. Atashirikiana na katibu wake kutia saini katika kumbukumbu za mikutano ya kituo.
vi. Kupiga kura ya turufu kama kura zitafungamana katika maamuzi yote ngazi ya kituo.
vii. Kuwakilisha chama katika mialiko na shughuli mbalimbali ngazi ya kituo.
viii. Iwapo mwenyekiti wa kituo hatakuwepo kwa muda wa miezi sita (6) kwa udhuru maalum, kujiuzulu kazi yake kukoma, kustaafu au kuachishwa uongozi wanachama wa kituo

watamteua mjumbe miongoni mwao kukaimu nafasi hiyo kwa muda mpaka uchaguzi utakapofanyika.

## 5.4. MAJUKUMU YA MAKAMU MWENYEKITI WA KITUO:

a. Makamu mwenyekiti ndiye msaidizi wa mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za mwenyekiti endapo:
b. Mwenyekiti hayupo au mwenyekiti amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
c. Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.5 MAJUKUMU YA KATIBU WA KITUO:

Katibu wa kituo atachaguliwa miongoni mwa wanachama hai na atafanya kazi zifuatazo:

i. Atakuwa ni mtendaji na mratibu wa shughuli zote za umoja ngazi ya kituo
ii. Kuhudhulia mikutano yote ya kituo na kutunza kumbukumbu za mikutano hiyo.
iii. Kufanya mawasiliano yote yanayo husika katika kituo na kuwasomea taarifa mbalimbali wanachama iwapo itajitokeza haja hiyo.
iv. Ni mtekelezaji mkuu wa maamuzi ya vikao vya mkutano mkuu wa kituo.
v. Kuitisha vikao vya umoja kwa kushirikiana na mwenyekiti wa kituo.
vi. Kuandika na kusoma mihutasari ya vikao vyote vya umoja ngazi ya kituo.
vii. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yote ya vikao vya umoja ngazi ya kituo.
viii. Ni kiunganishi wa shughuli zote za umoja ngazi ya kituo.
ix. Kutunza vitabu vya fedha na hati za malipo za kituo.
x. Kuandaa bajeti na mpango wa kazi za kituo.
xi. Kwa kushauriana na mwenyekiti au makamu mwenyekiti anaweza kutenda kwa haraka bila kusubiri kamati ya kituo, ila baada ya kukamilisha jambo hilo, matendo au maamuzi yaliyofikiwa katika jambo hilo la dharura atayawasilisha mbele ya kamati ya kituo ili yapate baraka.

## 5.6 MAJUKUMU YA NAIBU KATIBU WA KITUO:

a) Naibu katibu ndiye msaidizi wa katibu ambaye atafanya kazi zote za katibu endapo:
b) Katibu hayupo au katibu amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
c) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.7 MAJUKUMU YA MWEKA HAZINA WA KITUO:

a) Mtunza hazina wa kituo atakuwa na majukumu yafuatayo:

b) Kupokea na kutunza kumbukumbu zote za fedha za umoja ngazi ya kituo
c) Kuandaa, kuhakiki na kutoa taarifa za fedha zinazohusu ada, viingilio, adhabu, na michango mingine ya wanachama ngazi ya kituo.
d) Kuaandaa taarifa ya mapato, matumizi na madeni ya wanachama
e) Kutoa nakala za taarifa za fedha kwenye kikao cha kamati ya kituo.
f) Mtunza hazina atahakikisha kuwa fedha zote za ada, michango, kutoka kwa wanachama wote zinapelekwa banki.
g) Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi
h) Kutoa stakabadhi ya malipo ya fedha iliyopokelewa kwenye umoja inayohusu ngazi ya kata.

## 5.8 MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MKUU WA KITUO:

a) Kiongozi mkuu wa nidhamu atakuwa ni msimamizi na mwelekezaji mkuu wa maswala yote ya kinidhamu ndani ya chama ngazi ya kituo
b) Atakuwa ni mtatuzi mkuu wa migogoro ya kinidhamu itakayojitokeza ndani ya kituo husika
c) Atasimamia nidhamu ndani ya vikao vyote vya kituo.
d) Atahakikisha ulinzi wa vyombo na mali zote za wanachama zinakuwa salama kwenye vikao vyote vya kituo.
e) Atafanya kazi za kuimarisha usalama ndani ya kituo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa mwanachama yeyote atakayevunja taratibu ambazo zilizopo ndani ya katiba hii.
f) Atamwajibisha mwanachama muda wowote endapo itabainika amevunja utaratibu wa kituo hata kama mwenyekiti na katibu hawapo ilimradi awafikishie taarifa ya hatua alizochukua dhidi ya mwanachama huyo.
g) Iwapo mwanachama huyo atakataa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na mtunza nidhamu atatoa taarifa kwa mwenyekiti au katibu ili kufikisha taarifa hizo kwa uongozi wa kata.

## 5.9 MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA KITUO:

a) Mtunza nidhamu msaidizi ndiye msaidizi mkuu wa nidhamu ambaye atafanya kazi zote za mtunza nidhamu mkuu endapo:
b) Mtunza nidhamu mkuu hayupo au amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
c) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.10 VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA KATA:

Viongozi wa kata watakuwa ni:

a) Mwenyekiti
b) Makamu mwenyekiti
c) Katibu
d) Naibu katibu
e) Mhasibu/au mweka hazina
f) Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu
g) Mtunza nidhamu msaidizi.

## 5.11. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA KATA:

i. Mwenyekiti ndiye kiongozi wa chama ngazi ya kata.
ii. Atasimamia na Kufuatilia shughuli zote za chama za kiutawala akisaidiana na viongozi. Wengine waandamizi kwenye kata husika.
iii. Ataitisha vikao vyote viwe vya dharura au vya kikatiba akishirikiana na katibu wake.
iv. Kuendesha na kusimamia vikao vyote vya mkutano ndani ya kata.
v. Atashirikiana na katibu wake kutia saini katika kumbukumbu za mikutano ya kata.
vi. Kupiga kura ya turufu kama kura zitafungamana katika maamuzi yote ngazi ya kata.
vii. Kuwakilisha chama katika mialiko na shughuli mbalimbali ngazi ya kata.

## 5.12. MAJUKUMU YA MAKAMU MWENYEKITI WA KATA:

a) Makamu mwenyekiti ndiye msaidizi wa mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za mwenyekiti endapo:
b) Mwenyekiti hayupo au mwenyekiti amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
c) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.13. MAJUKUMU YA KATIBU WA KATA:

Kutakuwa na katibu wa chama wa kata atakayeteuliwa na kamati kuu ya chama mkoa. Katibu wa kata atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa chama katika kata na atafanya kazi zake chini ya usimamizi wa kamati kuu ya kata na kuwajibika kwa katibu wa wilaya. Na Katibu atakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Atakuwa ni mtendaji na mratibu wa shughuli zote za umoja ngazi ya kata
ii. Kuhudhulia mikutano yote ya chama katika kata.
iii. Kutunza kumbukumbu sahihi ya mapato na matumizi ndani ya kata.

iv. Ni mtekelezaji mkuu wa maamuzi ya vikao vya mkutano mkuu wa kata.
v. Kuitisha vikao vya umoja kwa kushirikiana na mwenyekiti wa kata.
vi. Kuandika na kusoma mihutasari ya vikao vyote vya umoja ngazi ya kata.
vii. Kuweka kumbukumbu zote za umoja ngazi ya kituo.
viii. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yote ya vikao vya umoja ngazi ya kata
ix. Ni kiunganishi wa shughuli zote za umoja ngazi ya kata
x. Kwa kushauriana na mwenyekiti au makamu mwenyekiti anaweza kutenda kwa haraka bila kusubiri kamati ya kituo, ila baada ya kukamilisha jambo hilo, matendo au maamuzi yaliyofikiwa katika jambo hilo la dharura atayawasilisha mbele ya uongozi wa kata ili yapate baraka.

## 5.14. MAJUKUMU YA NAIBU KATIBU WA KATA:

Kutakuwa na naibu katibu wa chama wa kata atakayeteuliwa na kamati kuu ya chama mkoa. Naibu katibu wa kata atakuwa ndiye mtendaji mkuu msaidizi wa katibu wa chama kata na atafanya kazi zake chini ya usimamizi wa kamati kuu ya kata na kuwajibika kwa katibu wa wilaya. Na Katibu atakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Naibu katibu ndiye msaidizi wa katibu ambaye atafanya kazi zote za katibu endapo:
b) Katibu hayupo au katibu amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
c) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.15. MAJUKUMU YA MWEKA HAZINA WA KATA:

i. Mtunza hazina wa kata atakuwa na majukumu yafuatayo:
ii. Kupokea na kutunza kumbukumbu zote za fedha za umoja ngazi ya kata
iii. Kuandaa, kuhakiki na kutoa taarifa za fedha zinazohusu ada, viingilio, adhabu, na michango mingine ya wanachama ngazi ya kata.
iv. Kuaandaa taarifa ya mapato, matumizi na madeni ya wanachama.
v. Kutoa nakala za taarifa za fedha kwenye kikao cha kamati kuu ya kata.
vi. Mtunza hazina atahakikisha kuwa fedha zote za ada, michango, kutoka kwa wanachama wote zinapelekwa benki.
vii. Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi.
viii. Kutoa stakabadhi ya malipo ya fedha iliyopokelewa kwenye umoja inayohusu ngazi ya kata.

## 5.14. MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MKUU WA KATA:

i. Kiongozi mkuu wa nidhamu atakuwa ni msimamizi na mwelekezaji mkuu wa maswala yote ya kinidhamu ndani ya chama ngazi ya kata.
ii. Atakuwa ni mtatuzi mkuu wa migogoro ya kinidhamu itakayojitokeza ndani ya kata husika.
iii. Atasimamia nidhamu ndani ya vikao vyote vya kata.
iv. Atahakikisha ulinzi wa vyombo na mali zote za wanachama zinakuwa salama kwenye vikao vyote vya kata.
v. Atafanya kazi za kuimarisha usalama ndani ya kata na kuchukua hatua za kinidhamu kwa mwanachama yeyote atakayevunja taratibu ambazo zilizopo ndani ya katiba hii.
vi. Atamwajibisha mwanachama muda wowote endapo itabainika amevunja utaratibu wa kata hata kama mwenyekiti na katibu hawapo ilimradi awafikishie taarifa ya hatua alizochukua dhidi ya mwanachama huyo.
vii. Iwapo mwanachama huyo atakataa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na mtunza nidhamu atatoa taarifa kwa mwenyekiti au katibu ili kufikisha taarifa hizo kwa uongozi wa kata.

## 5.15. MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA KATA:

a) Mtunza nidhamu msaidizi ndiye msaidizi mkuu wa nidhamu ambaye atafanya kazi zote za mtunza nidhamu mkuu endapo:
b) Mtunza nidhamu mkuu hayupo au amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
c) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi

## 5.16 AFISA HABARI WA CHAMA NGAZI YA KATA:

a) Kutakuwa na afisa habari wa chama kata.
b) Atateuliwa na kamati kuu ya kata.

## 5.17 MAJUKUMU YA AFISA HABARI WA CHAMA:

a) Atakuwa ndiye mtoa taarifa zote za chama kwa maelekezo ya vikao vya kamati kuu.
b) Uafisa habari wake utakoma pindi kamati kuu itakapoona ameenda tofauti/kinyume na maelekezo ya kamati kuu ya kata

## 5.18. VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA WILAYA:

Viongozi wa wilaya watakuwa ni:

a) Mwenyekiti

b) Makamu mwenyekiti
c) Katibu
d) Naibu katibu
e) Mhasibu/au mweka hazina
f) Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu
g) Mtunza nidhamu msaidizi.

### 5.19. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA WILAYA:

i. Mwenyekiti ndiye kiongozi wa chama ngazi ya wilaya.
ii. Atasimamia na Kufuatilia shughuli zote za chama za kiutawala akisaidiana na viongozi. Wengine waandamizi kwenye wilaya husika.
iii. Ataitisha vikao vyote viwe vya dharura au vya kikatiba akishirikiana na katibu wake.
iv. Kuendesha na kusimamia vikao vyote vya mikutano ndani ya wilaya.
v. Atashirikiana na katibu wake kutia saini katika kumbukumbu za mikutano ya wilaya.
vi. Kupiga kura ya turufu kama kura zitafungamana katika maamuzi yote ngazi ya wilaya.
vii. Kuwakilisha chama katika mialiko na shughuli mbalimbali ngazi ya wilaya.

### 5.20. MAJUKUMU YA MAKAMU MWENYEKITI WA WILAYA:

a) Makamu mwenyekiti ndiye msaidizi wa mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za mwenyekiti endapo:
b) Mwenyekiti hayupo au mwenyekiti amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
c) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

### 5.21. MAJUKUMU YA KATIBU WA WILAYA:

Kutakuwa na katibu wa chama wa wilaya atakayeteuliwa na kamati kuu ya chama mkoa. Katibu wa wilaya atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa chama katika wilaya na atafanya kazi zake chini ya usimamizi wa kamati kuu ya wilaya na kuwajibika kwa katibu mkuu wa mkoa. Na Katibu atakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Katibu atakuwa na majukumu yafuatayo:
ii. Atakuwa ni mtendaji na mratibu wa shughuli zote za umoja ngazi ya wilaya.
iii. Ni mtekelezaji mkuu wa maamuzi ya vikao vya mkutano mkuu wa wilaya.
iv. Kuitisha vikao vya umoja kwa kushirikiana na mwenyekiti wa wilaya.
v. Kuandika na kusoma mihutasari ya vikao vyote vya umoja ngazi ya wilaya.
vi. Kuweka kumbukumbu zote za umoja ngazi ya wilaya.
vii. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yote ya vikao vya umoja ngazi ya wilaya

viii. Ni kiunganishi wa shughuli zote za umoja ngazi ya wilaya

ix. Kwa kushauriana na mwenyekiti au makamu mwenyekiti anaweza kutenda kwa haraka bila kusubiri uongozi wa wilaya, ila baada ya kukamilisha jambo hilo, matendo au maamuzi yaliyofikiwa katika jambo hilo la dharura atayawasilisha mbele ya uongozi wa wilaya ili yapate baraka.

## 5.22. MAJUKUMU YA NAIBU KATIBU WA WILAYA:

Kutakuwa na naibu katibu wa chama wa wilaya atakayeteuliwa na kamati kuu ya chama mkoa. Naibu katibu wa wilaya atakuwa ndiye mtendaji mkuu msaidizi wa katibu wa chama wilaya na atafanya kazi zake chini ya usimamizi wa kamati kuu ya wilaya na kuwajibika kwa katibu wa mkoa . Na Katibu atakuwa na majukumu yafuatayo

a) Naibu katibu ndiye msaidizi wa katibu ambaye atafanya kazi zote za katibu endapo:

b) Katibu hayupo au katibu amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:

c) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.23. MAJUKUMU YA MWEKA HAZINA WA WILAYA:

i. Mtunza hazina wa wilaya atakuwa na majukumu yafuatayo:

ii. Kupokea na kutunza kumbukumbu zote za fedha za umoja ngazi ya wilaya

iii. Kuandaa, kuhakiki na kutoa taarifa za fedha zinazohusu ada, viingilio, adhabu, na michango mingine ya wanachama ngazi ya wilaya.

iv. Kuaandaa taarifa ya mapato, matumizi na madeni ya wanachama.

v. Kutoa nakala za taarifa za fedha kwenye kikao cha kamati kuu ya wilaya.

vi. Mtunza hazina atahakikisha kuwa fedha zote za ada, michango, kutoka kwa wanachama wote zinapelekwa benki.

vii. Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi.

viii. Kutoa stakabadhi ya malipo ya fedha iliyopokelewa kwenye umoja inayohusu ngazi ya wilaya.

## 5.24. MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MKUU WA WILAYA:

i. Kiongozi mkuu wa nidhamu atakuwa ni msimamizi na mwelekezaji mkuu wa maswala yote ya kinidhamu ndani ya chama ngazi ya wilaya.

ii. Atakuwa ni mtatuzi mkuu wa migogoro ya kinidhamu itakayojitokeza ndani ya wilaya husika.

iii. Atasimamia nidhamu ndani ya vikao vyote vya wilaya.

iv. Atahakikisha ulinzi wa vyombo na mali zote za wanachama zinakuwa salama kwenye vikao vyote vya wilaya.
v. Atafanya kazi za kuimarisha usalama ndani ya wilaya na kuchukua hatua za kinidhamu kwa mwanachama yeyote atakayevunja taratibu zilizopo ndani ya katiba hii.
vi. Atamwajibisha mwanachama muda wowote endapo itabainika amevunja utaratibu wa kata hata kama mwenyekiti na katibu hawapo ilimradi awafikishie taarifa ya hatua alizochukua dhidi ya mwanachama huyo.
vii. Iwapo mwanachama huyo atakataa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na mtunza nidhamu atatoa taarifa kwa mwenyekiti au katibu ili kufikisha taarifa hizo kwa uongozi wa wilaya.

### 5.25. MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA WILAYA:

a. Mtunza nidhamu msaidizi ndiye msaidizi mkuu wa nidhamu ambaye atafanya kazi zote za mtunza nidhamu mkuu endapo:
b. Mtunza nidhamu mkuu hayupo au amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
c. Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

### 5.26. AFISA HABARI WA CHAMA NGAZI YA WILAYA:

a. Kutakuwa na afisa habari wa chama wilaya.
b. Atateuliwa na kamati kuu ya wilaya.

### 5.27. MAJUKUMU YA AFISA HABARI WA CHAMA:

a. Atakuwa ndiye mtoa taarifa zote za chama kwa maelekezo ya vikao vya kamati kuu.
b. Uafisa habari wake utakoma pindi kamati kuu itakapoona ameenda tofauti/kinyume na maelekezo ya kamati kuu ya wilaya.

### 5.28. VIONGOZI WA CHAMA NGAZI YA MKOA:

Kutakuwa na Kamati kuu ya mkoa itakayokuwa ndicho chombo cha juu cha utekelezaji wa maamuzi ya Chama na itawajibika kufanya maamuzi yote na

(a) Viongozi wa mkoa watakuwa ni:
(b) Mwenyekiti wa mkoa
(c) Makamu mwenyekiti wa mkoa
(d) Katibu wa mkoa
(e) Naibu katibu wa mkoa
(f) Mhasibu/au mweka hazina wa mkoa
(g) Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu mkoa

(h) Mtunza nidhamu msaidizi wa mkoa.

## 5.29. MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA MKOA:

Mwenyekiti wa mkoa atakuwa ndiye msimamizi na mwangalizi mkuu wa shughuli zote za Chama na majukumu yake makuu yatakuwa yafuatayo:-

i. Atasimamia na Kufuatilia shughuli zote za chama za kiutawala akisaidiana na viongozi wengine waandamizi kwenye mkoa
ii. Ataitisha vikao vyote viwe vya dharura au vya kikatiba akishirikiana na katibu wake.
iii. Kuendesha na kusimamia vikao vyote vya mkutano ndani ya mkoa.
iv. Atashirikiana na katibu wake kutia saini katika kumbukumbu za mikutano ya mkoa.
v. Kupiga kura ya turufu kama kura zitafungamana katika maamuzi yote ngazi ya mkoa.
vi. Kuwakilisha chama katika mialiko na shughuli mbalimbali ngazi ya mkoa
vii. Kuhakikisha kuwa katiba, kanuni na taratibu zote zilizopangwa zinafuatwa katika utekelezaji wa shughuli na majukumu ya chama na wale wote wanaohusika
viii. Kuwa msemaji mkuu wa chama.

## 5.30. MAJUKUMU YA MAKAMU MWENYEKITI WA MKOA:

Makamu mwenyekiti ndiye msaidizi wa mwenyekiti na ambaye atafanya kazi zote za mwenyekiti endapo:

a) Mwenyekiti hayupo au mwenyekiti amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
b) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.31. MAJUKUMU YA KATIBU MKUU WA MKOA:

Katibu Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu wa Chama anayewajibika katika utekelezaji wa maamuzi yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu, na atafanya shughuli zifuatazo:-

i. Atakuwa ni mtendaji na mratibu wa shughuli zote za umoja ngazi ya mkoa.
ii. Kutoa msaada utakaohitajika kwa wakaguzi wa hesabu za chama.
iii. Kusimamia utunzaji wa hesabu za fedha za chama na kutolea maelezo matumizi yote ya fedha za chama na kuhimiza utawala mzuri wa fedha za chama.
iv. Ni mtekelezaji mkuu wa maamuzi ya vikao vya mkutano mkuu wa mkoa.
v. Kuitisha vikao vya umoja kwa kushirikiana na mwenyekiti wa mkoa.
vi. Kuandika na kusoma mihutasari ya vikao vyote vya umoja ngazi ya mkoa.
vii. Kuweka kumbukumbu zote za umoja ngazi ya mkoa.

viii. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yote ya vikao vya umoja ngazi ya mkoa
ix. Ni kiunganishi wa shughuli zote za umoja ngazi ya mkoa
x. Kwa kushauriana na mwenyekiti au makamu mwenyekiti anaweza kutenda kwa haraka bila kusubiri uongozi wa mkoa, ila baada ya kukamilisha jambo hilo, matendo au maamuzi yaliyofikiwa katika jambo hilo la dharura atayawasilisha mbele ya uongozi wa mkoa ili yapate baraka.

## 5.32. MAJUKUMU YA NAIBU KATIBU MKUU WA MKOA:

Majukumu ya Naibu katibu mkuu ndiye msaidizi wa katibu ambaye atafanya kazi zote za katibu zifuatazo:

i. Katibu hayupo au katibu amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine kama:
ii. Kukaimu nafasi ya Katibu Mkuu pale itakapoonekana ipo haja ya kufanya hivyo.
iii. Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.33. MAJUKUMU YA MWEKA HAZINA WA MKOA:

Mtunza hazina wa mkoa atakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kuongoza vikao vyote vya kamati ya fedha.
ii. Kumshauri Katibu Mkuu juu ya masuala ya fedha
iii. Kuishauri Kamati kuu juu ya mbinu za kuongeza mapato.
iv. Kupokea na kutunza kumbukumbu zote za fedha za umoja ngazi ya mkoa
v. Kuandaa, kuhakiki na kutoa taarifa za fedha zinazohusu ada, viingilio, adhabu, na michango mingine ya wanachama ngazi ya mkoa.
vi. Kuaandaa taarifa ya mapato, matumizi na madeni ya wanachama.
vii. Kuhakikisha kuwa kanuni na taratibu za fedha zilizowekwa zinafuatwa kikamilifu.
viii. Kutoa nakala za taarifa za fedha kwenye kikao cha kamati kuu ya mkoa.
ix. Mtunza hazina atahakikisha kuwa fedha zote za ada, michango, kutoka kwa wanachama wote zinapelekwa benki.
x. Kufanya malipo mbalimbali na kutunza nakala za stakabadhi.
xi. Kutoa stakabadhi ya malipo ya fedha iliyopokelewa kwenye umoja inayohusu ngazi ya mkoa.

## 5.34. MAJUKUMU YA MTUNZA NIDHAMU MKUU WA MKOA:

i. Kiongozi mkuu wa nidhamu atakuwa ni msimamizi na mwelekezaji mkuu wa maswala yote ya kinidhamu ndani ya chama ngazi ya Mkoa.
ii. Atakuwa ni mtatuzi mkuu wa migogoro ya kinidhamu itakayojitokeza ndani ya Mkoa husika.
iii. Atasimamia nidhamu ndani ya vikao vyote vya Mkoa.
iv. Atahakikisha ulinzi wa vyombo na mali zote za wanachama zinakuwa salama kwenye vikao vyote vya Mkoa.
v. Atafanya kazi za kuimarisha usalama ndani ya Mkoa na kuchukua hatua za kinidhamu kwa mwanachama yeyote atakayevunja taratibu zilizopo ndani ya katiba hii.
vi. Atamwajibisha mwanachama muda wowote endapo itabainika amevunja utaratibu wa hata kama mwenyekiti na katibu hawapo ilimradi awafikishie taarifa ya hatua alizochukua dhidi ya mwanachama huyo.
vii. Iwapo mwanachama huyo atakataa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na mtunza nidhamu atatoa taarifa kwa mwenyekiti au katibu ili kufikisha taarifa hizo kwa uongozi wa mkoa.

## 5.35. MTUNZA NIDHAMU MSAIDIZI WA MKOA:

Mtunza nidhamu msaidizi ndiye msaidizi mkuu wa nidhamu ambaye atafanya kazi zote za mtunza nidhamu mkuu endapo:

a) Mtunza nidhamu mkuu hayupo au amekosa uwezo wa kufanya kazi zake kwa sababu ya kusafiri au kuugua au sababu nyingine.
b) Kujiuzulu au kufukuzwa uongozi.

## 5.36. AFISA HABARI WA CHAMA NGAZI YA MKOA:

a) Kutakuwa na afisa habari wa chama mkoa.
b) Atateuliwa na kamati kuu ya mkoa.

## 5.37. MAJUKUMU YA AFISA HABARI WA CHAMA:

(a) Atakuwa ndiye mtoa taarifa zote za chama kwa maelekezo ya vikao vya kamati kuu.
(b) Uafisa habari wake utakoma pindi kamati kuu itakapoona ameenda tofauti/kinyume na maelekezo ya kamati kuu ya Mkoa

## 5.38 KAMATI MBALIMBNALI ZA CHAMA KIKATIBA:

Umoja utakuwa na kamati mbalimbali za chama kikatiba na muundo wake ni kama ifuatavyo:

(a) Kamati za kata
(b) Kamati za wilaya na
(c) Kamati za Mkoa.

Kamati hizo zimegawanyika katika sehemu kuu tano ambazo ni:

(a) Kamati ya uchaguzi
(b) Kamati ya fedha na uchumi/mipango.
(c) Kamati ya nidhamu na maadili.
(d) Kamati maalum
(e) Kamati ya huduma za jamii.
(f) Kamati ya rufaa ya Mkoa.

## 5.39 KAMATI YA UCHAGUZI NGAZI KATA:

(i) Kamati hii ya uchaguzi ya kata itaratibu na kusimamia shughuli zote za uchaguzi ngazi kata.
(ii) Kamati hiyo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (05)
(iii) Kamati hii itaongozwa na mwenyekiti na katibu watakao chaguliwa na wajumbe wa kamati hiyo.
(iv) Majina ya wajumbe wa kamati ya uchaguzi yatapendekezwa na kamati kuu ya wilaya kisha kupigiwa kura na halmashauri kuu ya kata.
(v) Wajumbe wa kamati hii watakuwa ni wanachama na siyo wagombea wa nafasi yoyote ya uongozi ndani ya kata.
(vi) Kamati hii itafikia ukomo wake baada ya uchaguzi kuisha.

## 5.40 KAMATI YA UCHAGUZI NGAZI WILAYA:

(i) Kamati hii ya uchaguzi ya wilaya itaratibu na kusimamia shughuli zote za uchaguzi ngazi wilaya.
(ii) Kamati hiyo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (05)
(iii) Kamati hii itaongozwa na mwenyekiti na katibu watakao chaguliwa na wajumbe wa kamati hiyo.
(iv) Majina ya wajumbe wa kamati ya uchaguzi yatapendekezwa na kamati kuu ya Mkoa kisha kupigiwa kura na halmashauri kuu ya wilaya.
(v) Wajumbe wa kamati hii watakuwa ni wanachama na siyo wagombea wa nafasi yoyote ya uongozi ndani ya wilaya.

(vi) Kamati hii itafikia ukomo wake baada ya uchaguzi kuisha.

## 5.41 KAMATI YA UCHAGUZI NGAZI YA MKOA:

(i) Kamati hii ya uchaguzi ya mkoa itaratibu na kusimamia shughuli zote za uchaguzi ngazi Mkoa.
(ii) Kamati hiyo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (05)
(iii) Kamati hii itaongozwa na mwenyekiti na katibu watakao chaguliwa na wajumbe wa kamati hiyo.
(iv) Majina ya wajumbe wa kamati ya uchaguzi yatapendekezwa na kamati kuu ya Mkoa kisha kupigiwa kura na halmashauri kuu ya Mkoa.
(v) Wajumbe wa kamati hii watakuwa ni wanachama na siyo wagombea wa nafasi yoyote ya uongozi ndani ya Mkoa.
(vi) Kamati hii itafikia ukomo wake baada ya uchaguzi kuisha.

## 5.42. KAMATI YA FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO NGAZI YA KATA:

Kamati ya fedha uchumi na mipango itakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuibua miradi mbalimbali ya chama ndani ya kata husika.
(ii) Kutathimini maendeleo ya chama kifedha na kiuchumi ndani ya kata husika.
(iii) Kushauri chama juu ya hatua za kuchukua kwa nia ya kujikwamua na kujitegemea kiuchumi ndani ya kata husika.
(iv) Kuishauri kamati kuu ya kata kwa maswala yanayohusu fedha, michango na majukumu mengine watakayopangiwa na kamati kuu/halmashauri au mkutano mkuu.

## 5.43 KAMATI YA FEDHA UCHUMI NA MIPANGO NGAZI YA WILAYA:

Kamati ya fedha uchumi na mipango itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) Kuibua miradi mbalimbali ya chama ndani ya wilaya husika.
(b) Kutathimini maendeleo ya chama kifedha na kiuchumi ndani ya wilaya husika.
(c) Kushauri chama juu ya hatua za kuchukua kwa nia ya kujikwamua na kujitegemea kiuchumi ndani ya wilaya husika.
(d) Kuishauri kamati kuu ya wilaya kwa maswala yanayohusu fedha, michango na majukumu mengine watakayopangiwa na kamati kuu/halmashauri au mkutano mkuu.

## 5.44 KAMATI YA FEDHA UCHUMI NA MIPANGO NGAZI YA MKOA:

1. Kamati ya Fedha uchumi na Mipango itakuwa na wajumbe watano (5) ambao ni;
2. Afisa wa Chama atakayekuwa anaongoza Ofisi ya Fedha, Sera na Mipango ambaye atakuwa ni Katibu wa Kamati;
3. Afisa wa Chama atakayekuwa anaongoza Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za Chama na wajumbe watatu watapendekezwa na halimashauri kuu ya chama.

**Kamati ya fedha uchumi na mipango itakuwa na majukumu yafuatayo:**

i. Kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu utunzaji wa rasilimali na fedha za Chama;
ii. Kupokea Taarifa ya fedha toka kwa mweka hazina wa Chama, kuijadili na kutoa mapendekezo ya uboreshwaji wa Taarifa hiyo kabla haijawasilishwa mbele ya vikao vikuu vya Chama;
iii. Kupokea rasimu ya bajeti ya Chama, kuijadili na kutoa mapendekezo ya kuboresha rasimu hiyo kabla haijawasilishwa mbele ya vikao vya vyombo vikuu vya Chama;
iv. Kupokea na kuchambua Taarifa za fedha na bajeti za kata na wilaya kama zitakavyokuwa zimewasilishwa kwa Katibu Mkuu kwa mujibu wa Katiba hii;
v. Kupokea, kujadili na kuandaa taarifa fupi ya hoja za Mkaguzi wa nje wa Hesabu za Fedha wa Chama ikiwemo taarifa ya Mkaguzi wa ndani na kuwasilisha taarifa ya Kamati na mapendekezo mbele ya Kamati Kuu.
vi. Kutoa mapendekezo kwa Kamati Kuu kuhusu mipango yoyote itakayowezesha Chama kujiimarisha kifedha ili kuweza kutekeleza majukumu mbalimbali ya Chama kwa maslahi ya wanachama wake.
vii. Kushauri Kamati Kuu juu ya hatua za haraka zinazotakiwa kuchukuliwa ili kuepusha Chama kuingia katika matatizo ya kifedha au kuzuia ubadhilifu wowote wa fedha.
viii. Kamati ya Fedha uchumi na Mipango itakutana katika vikao vya kawaida mara mbili kwa mwaka na Katibu Mkuu wa Chama, baada ya Kushauriana na Mwenyekiti, ataratibu maandalizi ya Kikao cha Kamati hiyo.

## 5.45 KAMATI YA NIDHAMU NA MAADILI YA CHAMA KATA:

Kamati ya nidhamu na maadili itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kushughulikia maswala yote ya nidhamu yatakayoletwa na katibu wa kata.

ii. Kuelekeza hatua za kuchukua dhidi ya kituo, kata na kamati au mwana umoja aliyekutwa na hatia ya kukiuka taratibu za umoja ndani ya kata.
iii. Kushauri umoja/chama juu ya maswala yanayohusiana na nidhamu na maadili kwenye kata.
iv. Kushughulikia makosa yote isipokuwa makosa ya jinai kwenye kata.
v. Katika kushughulikia maswala ya nidhamu:
vi. Kamati itamwalika mwanachama au kumjulisha na kumfafanulia tuhuma dhidi yake ndani ya kata.
vii. Kamati itampatia nafasi mwanachama kujitetea dhidi ya tuhuma inayomkabili.
viii. Kamati itachambua utetezi dhidi ya makosa ya mwanachama anayotuhumiwa nayo.
ix. Kamati ya nidhamu itaandika uamuzi ambao pande zinazohusika na shauri hilo zitapewa uamuzi na nakala kwa katibu wa kata anachotokea mlalamikiwa/mlalamikaji
x. Kamati itatoa uamuzi wa haki au wenye kuzingatia misingi,mila na desturi za utoaji haki ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria za nchi.
xi. Kamati ya nidhamu na maadili haitakuwa na mamlaka ya kushughulikia shauri lolote isipokuwa lile litakalofikishwa mbele yake na katibu wa kata , na katibu wa kata ndiye mlalamikaji katika mashauri yote.

## 5.46 KAMATI YA NIDHAMU NA MAADILI YA CHAMA WILAYA:

Kamati ya nidhamu na maadili itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kushughulikia maswala yote ya nidhamu yatakayoletwa na katibu wa wilaya.
ii. Kuelekeza hatua za kuchukua dhidi ya kituo, kata na kamati au mwana umoja aliyekutwa na hatia ya kukiuka taratibu za umoja ndani ya wilaya.
iii. Kuuchauri umoja/chama juu ya maswala yanayohusiana na nidhamu na maadili kwenye wilaya.
iv. Kushughulikia makosa yote isipokuwa makosa ya jinai kwenye wilaya.
v. Katika kushughulikia maswala ya nidhamu:
vi. Kamati itamwalika mwanachama au kumjulisha na kumfafanulia tuhuma dhidi yake ndani ya wilaya.
vii. Kamati itampatia nafasi mwanachama kujitetea dhidi ya tuhuma inayomkabili.
viii. Kamati itachambua utetezi dhidi ya makosa ya mwanachama anayotuhumiwa nayo.

ix. Kamati ya nidhamu itaandika uamuzi ambao pande zinazohusika na shauri hilo zitapewa uamuzi na nakala kwa katibu wa wilaya anachotokea mlalamikiwa/mlalamikaji
x. Kamati itatoa uamuzi wa haki au wenye kuzingatia misingi, mila na desturi za utoaji haki ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria za nchi.
xi. Kamati ya nidhamu na maadili haitakuwa na mamlaka ya kushughulikia shauri lolote isipokuwa lile litakalofikishwa mbele yake na katibu wa wilaya, na katibu wa wilaya ndiye mlalamikaji katika mashauri yote.

## 5.47 KAMATI YA NIDHAMU NA MAADILI YA CHAMA MKOA:

Kamati ya nidhamu na maadili itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kushughulikia maswala yote ya nidhamu yatakayoletwa na katibu wa Mkoa.
ii. Kuelekeza hatua za kuchukua dhidi ya kituo, kata na wilaya kamati au mwanaumoja aliyekutwa na hatia ya kukiuka taratibu za umoja ndani ya Mkoa.
iii. Kuuchauri umoja/chama juu ya maswala yanayohusiana na nidhamu na maadili kwenye Mkoa.
iv. Kushughulikia makosa yote isipokuwa makosa ya jinai kwenye Mkoa.
v. Katika kushughulikia maswala ya nidhamu:
vi. Kamati itamwalika mwanachama au kumjulisha na kumfafanulia tuhuma dhidi yake ndani ya Mkoa.
vii. Kamati itampatia nafasi mwanachama kujitetea dhidi ya tuhuma inayomkabili.
viii. Kamati itachambua utetezi dhidi ya makosa ya mwanachama anayotuhumiwa nayo.
ix. Kamati ya nidhamu itaandika uamuzi ambao pande zinazohusika na shauri hilo zitapewa uamuzi na nakala kwa katibu wa Mkoa anachotokea mlalamikiwa/mlalamikaji.
x. Kamati itatoa uamuzi wa haki au wenye kuzingatia misingi, mila na desturi za utoaji haki ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria za nchi.
xi. Kamati ya nidhamu na maadili haitakuwa na mamlaka ya kushughulikia shauri lolote isipokuwa lile litakalofikishwa mbele yake na katibu wa Mkoa, na katibu wa Mkoa ndiye mlalamikaji katika mashauri yote.

## 5.48 KAMATI MAALUM YA CHAMA KATA:

i. Kamati maalumu inaweza kuundwa na halmashauri au mkutano mkuu wa kata baada ya wajumbe wake kupendekezwa na kamati kuu ya kata:
ii. Itaundwa iwapo kuna jambo maalum linalohitaji uchunguzi wa kina ndani ya kata

iii. Majina ya wajumbe wake yatatangazwa eidha kwenye mkutano mkuu au vikao vya kata ili wanachama wote wajue.
iv. Kazi za kamati/hadidu za rejea zitajulikana kwa wanachama wote.
v. Mamlaka ya uteuzi ambayo ni kamati kuu ya kata ndiyo itakayoamua kuteua viongozi wa kamati hiyo.
vi. Taarifa ya matokeo ya kazi itakayofanywa na kamati hiyo itawasilishwa kwa mamlaka iliyoiunda.
vii. Taarifa ya kamati maalum itawekwa wazi kwa wanachama wote kupitia mkutano mkuu wa kata.
viii. Uhai na kazi ya kamati maalum utaisha baada ya kukabidhi taarifa kwa mamlaka iliyoiunda.

## 5.49 KAMATI MAALUMU YA CHAMA WILAYA:

i. Kamati maalum inaweza kuundwa na halmashauri au mkutano mkuu wa wilaya baada ya wajumbe wake kupendekezwa na kamati kuu ya wilaya:
ii. Itaundwa iwapo kuna jambo maalum linalohitaji uchunguzi wa kina ndani ya wilaya.
iii. Majina ya wajumbe wake yatatangazwa eidha kwenye mkutano mkuu au vikao vya wilaya ili wanachama wote wajue.
iv. Kazi za kamati/hadidu za rejea zitajulikana kwa wanachama wote.
v. Mamlaka ya uteuzi ambayo ni kamati kuu ya wilaya ndiyo itakayoamua kuteua viongozi wa kamati hiyo.
vi. Taarifa ya matokeo ya kazi itakayofanywa na kamati hiyo itawasilishwa kwa mamlaka iliyoiunda.
vii. Taarifa ya kamati maalum itawekwa wazi kwa wanachama wote kupitia mkutano mkuu wa wilaya.
viii. Uhai na kazi ya kamati maalum utaisha baada ya kukabidhi taarifa kwa mamlaka iliyoiunda.

## 5.50 KAMATI MAALUMU YA CHAMA MKOA:

i. Kamati maalumu inaweza kuundwa na halmashauri au mkutano mkuu wa Mkoa baada ya wajumbe wake kupendekezwa na kamati kuu ya Mkoa:
ii. Itaundwa iwapo kuna jambo maalum linalohitaji uchunguzi wa kina ndani ya Mkoa
iii. Majina ya wajumbe wake yatatangazwa eidha kwenye mkutano mkuu au vikao vya Mkoa ili wanachama wote wajue.
iv. Kazi za kamati/hadidu za rejea zitajulikana kwa wanachama wote.

v. Mamlaka ya uteuzi ambayo ni kamati kuu ya Mkoa ndiyo itakayoamua kuteua viongozi wa kamati hiyo.
vi. Taarifa ya matokeo ya kazi itakayofanywa na kamati hiyo itawasilishwa kwa mamlaka iliyoiunda.
vii. Taarifa ya kamati maalum itawekwa wazi kwa wanachama wote kupitia mkutano mkuu wa Mkoa.
viii. Uhai na kazi ya kamati maalum utaisha baada ya kukabidhi taarifa kwa mamlaka iliyoiunda.

## 5.51 KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII YA CHAMA KATA:

1. Kamati ya Huduma za Jamii
2. Kamati hiyo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (10)
3. Kamati ya Huduma za Jamii itakuwa na majukumu yafuatayo:
   a) Kutoa huduma mbali mbali kwenye matukio ya Umoja  kama vile: ajali,ugonjwa, misiba n.k
   b) Kusimamia Ulinzi na Usalama katika matukio mbali mbali ya umoja
   c) Kuushauri Umoja namna bora ya utoaji wa huduma na majukumu mengine watakayopewa na Kamati Kuu, Halmashauri au Mkutano Mkuu.
   d) Kamati hii itamaliza muda wake mara baada ya uongozi kumaliza muda wake uliowekwa kikatiba.

## 5.52 KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII YA CHAMA WILAYA:

1. Kamati ya Huduma za Jamii.
2. Kamati hiyo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (10)
3. Kamati ya Huduma za Jamii itakuwa na majukumu yafuatayo:
   a) Kutoa huduma mbali mbali kwenye matukio ya Umoja kama vile: ajali,ugonjwa, misiba n.k
   b) Kusimamia Ulinzi na Usalama katika matukio mbali mbali ya umoja.
   c) Kuushauri Umoja namna bora ya utoaji wa huduma na majukumu mengine watakayopewa na Kamati Kuu, Halmashauri au Mkutano Mkuu.
   d) Kamati hii itamaliza muda wake mara baada ya uongozi kumaliza muda wake uliowekwa kikatiba.

## 5.53 KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII YA CHAMA MKOA:

1. Kamati ya Huduma za Jamii.
2. Kamati hiyo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (10)

3. Kamati ya Huduma za Jamii itakuwa na majukumu yafuatayo:
   a) Kutoa huduma mbali mbali kwenye matukio ya Umoja kama vile: ajali, ugonjwa, misiba n.k.
   b) Kusimamia Ulinzi na Usalama katika matukio mbali mbali ya umoja.
   c) Kuushauri Umoja namna bora ya utoaji wa huduma na majukumu mengine watakayopewa na Kamati Kuu, Halmashauri au Mkutano Mkuu.
   d) Kamati hii itamaliza muda wake mara baada ya uongozi kumaliza muda wake uliowekwa kikatiba.

## 5.54 KAMATI YA RUFAA YA CHAMA MKOA:

Kamati ya rufaa ya Mkoa kitakuwa ni chombo cha kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi kwa rufaa zote zitakazopelekwa mbele yake.

a) Kamati hiyo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (05)
b) Kamati hii itaongozwa na mwenyekiti na katibu watakao chaguliwa na wajumbe wa kamati hiyo.
c) Majina ya wajumbe wa kamati ya rufaa yatapendekezwa na kamati kuu ya Mkoa kisha kupigiwa kura na halmashauri kuu ya Mkoa.
d) Wajumbe wa kamati hii watakuwa ni wanachama na siyo wagombea wa nafasi yoyote ya uongozi ndani ya Mkoa.
e) Kamati hii itafikia ukomo wake baada ya muhula wa kwanza wa uongozi ngazi kumaliza muda wake.

## 5.55 MAJUKUMU YA KAMATI YA RUFAA YA MKOA:

i. Iwapo mwanachama hakuridhika na uamuzi wa kamati ya nidhamu na maadili au kamati ya uchaguzi ana wajibu wa kukata rufaa kama katiba inavyomuelekeza.
ii. Atapeleka malalamiko yake kwa maandishi kwenye kamati ya rufaa akieleza sababu za kutoridhishwa na uamuzi wa kamati ya nidhamu na maadili na nakala kutolewa kwa upande mwingine baada ya kusainiwa na katibu wa kamati au mjumbe mwingine na kugongwa muhuri wa kamati ya rufaa.
iii. Rufaa hiyo itakatwa ndani ya siku nane (08) bila kujali siku za mwisho wa juma tangu kupokea uamuzi wa kamati ya nidhamu na maadili.
iv. Endapo kamati ya nidhamu na maadili imekiuka masharti ya katiba na kanuni katika kutoa uamuzi;
v. Uamuzi wa kamati ya nidhamu na maadili umekuwa mkali mno kiasi cha kukiuka misingi ya haki.

vi. Endapo kamati ya nidhamu na maadili haikutoa nafasi ya kujitetea au kusikilizwa.
vii. Endapo kamati ya nidhamu na maadili haikuzingatia utetezi na ushahidi uliotolewa;
viii. Endapo kamati ya nidhamu na maadili ilisikiliza upande mmoja bila kutoa wito kwa upande mwingine.
ix. Kamati ya Rufaa inaweza kupokea rufaa baada ya siku nane kupita tangu mrufani kupokea uamuzi wa Kamati ya nidhamu na maadili iwapo kuna sababu za msingi na zenye kuthibitishwa zilizomfanya achelewe kuwasilisha rufaa yake.

## 5.56 BARAZA LA WAZEE CHAMA KWENYE KITUO:

a) Kutakuwa na baraza la wazee wanaotokana na umoja katika kila ngazi ya uongozi.
b) Wajumbe wa mabaraza hayo watakuwa wazee wote kuanzia miaka hamsini (50) na kuendelea.
c) Kamati ya wazee katika ngazi zote itapatikana kwa kuteuliwa na viongozi wakuu wa umoja katika ngazi husika.
d) Baraza la wazee katika ngazi husika itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (05) na baraza hilo wajumbe wake watachagua mwenyekiti na katibu na watakaobaki watakuwa wajumbe wa baraza hilo.

**Katika kuteuwa wajumbe wa baraza hilo la wazee baraza litazingatia:**

a) Uwezo wa mzee katika uelewa wa masuala ya Umoja;
b) Uwezo wa mzee kuwa mkweli na asiyekuwa mwoga;
c) Uwezo wa kuheshimu na kufuata Katiba na Kanuni;
d) Uwezo wa kutunza siri za majadiliano na uamuzi; na
e) Umakini, kujitoa kwa moyo na jitihada za dhati katika kushughulikia masuala ya Umoja

## 5.57 MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE:

Baraza la wazee litakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kupokea, kupitia na kuteua wagombea katika kila ngazi husika ya uongozi;
ii. Kusuluhisha migogoro ya kiuongozi na kibinafsi kwa viongozi wa umoja.
iii. Katika kusuluhisha migogoro baraza litazingatia:
iv. Kurudisha maelewano baina ya viongozi;
v. Ushauri na siyo uamuzi;
vi. Kulinda maslahi mapana ya Umoja;
vii. Kutoa mawazo huru juu ya kiini cha tatizo;
viii. Kuzisaidia pande zinazohusika kuona ukweli;

ix. Kutumia busara na ushawishi ili kudhoofisha misimamo kinzani na
x. Kushughulikia migogoro iliyofikishwa mbele yake kwa maandishi na kiongozi yoyote wa ngazi husika au mjumbe yeyote wa Halmashauri.
xi. Barua ya kupeleka mgogoro mbele ya baraza la wazee sharti:
xii. Ielezee kiini cha mgogoro,
xiii. Wahusika katika mgogoro,
xiv. Hatua zilizochukuliwa kuutatua, na
xv. Taarifa nyingine zinazoweza kuisadia baraza la wazee katika kutatua mgogoro huo katika kutekeleza jukumu la usuluhishi baraza la wazee litawajibika:
xvi. Kutafuta taarifa kutoka kwa mtu yeyote juu ya mgogoro unaohitaji usuluhishi.
xvii. Kuwaita na kuongea na viongozi wanoahusika kwenye mgogoro huo; na
xviii. Mgogoro usipotatuliwa kuandaa taarifa fupi itakayowasilishwa kwenye kikao cha Halmashauri. kiongozi asipotii wito wa kumtaka afike mbele ya baraza la wazee:-
xix. baraza la wazee litatoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri;
xx. Halmashauri itamhoji kiongozi juu ya sababu za kukaidi wito wa baraza la wazee;
xxi. Halmashauri itakapojiridhisha kwamba kiongozi hakuwa na sababu za kutotii wito wa baraza la wazee itachukua hatua zifaazo ikiwa ni pamoja na kupendekeza Mkutano Mkuu umvue uongozi
xxii. Kiongozi hatachukuliwa kwamba hakukaidi wito wa baraza la wazee iwapo:
xxiii. Taarifa ya wito haikumfikia;
xxiv. Itathibitika kwamba alishindwa kufika mbele ya Kamati kwa sababu za ugonjwa;
xxv. Itathibitika kwamba ni kwa sababu ya msiba wa ndugu au jamaa wa karibu naye.
xxvi. Atatoa udhuru kwa sababu ya mwajili wake kumhitaji awe kazini.
xxvii. Itathibitika kwamba alikuwa na wito kwa vyombo vya dola mfano mahakamani au polisi;
xxviii. Atatoa udhuru wa safari ambayo aliipanga kabla ya kupokea wito wa baraza la wazee

## 5.58 BARAZA LA WAZEE WA CHAMA KATA:

a) Kutakuwa na baraza la wazee wanaotokana na umoja katika kila ngazi ya uongozi.
b) Wajumbe wa mabaraza hayo watakuwa wazee wote kuanzia miaka hamsini (50) na kuendelea.
c) Kamati ya wazee katika ngazi zote itapatikana kwa kuteuliwa na viongozi wakuu wa umoja katika ngazi husika.
d) Baraza la wazee katika ngazi husika itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (05) na baraza hilo wajumbe wake watachagua mwenyekiti na katibu na watakaobaki watakuwa wajumbe wa baraza hilo.

**Katika kuteuwa wajumbe wa baraza hilo la wazee baraza litazingatia:**

i. Uwezo wa mzee katika uelewa wa masuala ya Umoja.
ii. Uwezo wa mzee kuwa mkweli na asiyekuwa mwoga.
iii. Uwezo wa kuheshimu na kufuata Katiba na Kanuni.
iv. Uwezo wa kutunza siri za majadiliano na uamuzi; na
v. Umakini, kujitoa kwa moyo na jitihada za dhati katika kushughulikia masuala ya Umoja

## 5.59. MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE:

Baraza la wazee litakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kupokea, kupitia na kuteua wagombea katika kila ngazi husika ya uongozi;
ii. Kusuluhisha migogoro ya kiuongozi na kibinafsi kwa viongozi wa umoja.
iii. Katika kusuluhisha migogoro baraza litazingatia:
iv. Kurudisha maelewano baina ya viongozi;
v. Ushauri na siyo uamuzi;
vi. Kulinda maslahi mapana ya Umoja;
vii. Kutoa mawazo huru juu ya kiini cha tatizo;
viii. Kuzisaidia pande zinazohusika kuona ukweli;
ix. Kutumia busara na ushawishi ili kudhoofisha misimamo kinzani na
x. Kushughulikia migogoro iliyofikishwa mbele yake kwa maandishi na kiongozi yoyote wa ngazi husika au mjumbe yeyote wa Halmashauri.
xi. Barua ya kupeleka mgogoro mbele ya baraza la wazee sharti:
xii. Ielezee kiini cha mgogoro;
xiii. Wahusika katika mgogoro;
xiv. Hatua zilizochukuliwa kuutatua; na
xv. Taarifa nyingine zinazoweza kuisadia baraza la wazee katika kutatua mgogoro huo katika kutekeleza jukumu la usuluhishi baraza la wazee litawajibika:
xvi. Kutafuta taarifa kutoka kwa mtu yeyote juu ya mgogoro unaohitaji usuluhishi;
xvii. Kuwaita na kuongea na viongozi wanoahusika kwenye mgogoro huo; na
xviii. Mgogoro usipotatuliwa kuandaa taarifa fupi itakayowasilishwa kwenye kikao cha Halmashauri. kiongozi asipotii wito wa kumtaka afike mbele ya baraza la wazee:-
xix. baraza la wazee litatoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri;
xx. Halmashauri itamhoji kiongozi juu ya sababu za kukaidi wito wa baraza la wazee;

xxi. Halmashauri itakapojiridhisha kwamba kiongozi hakuwa na sababu za kutotii wito wa baraza la wazee itachukua hatua zifaazo ikiwa ni pamoja na kupendekeza Mkutano Mkuu umvue uongozi

xxii. Kiongozi hatachukuliwa kwamba hakukaidi wito wa baraza la wazee iwapo:

xxiii. Taarifa ya wito haikumfikia;

xxiv. Itathibitika kwamba alishindwa kufika mbele ya Kamati kwa sababu za ugonjwa;

xxv. Itathibitika kwamba ni kwa sababu ya msiba wa ndugu au jamaa wa karibu naye;

xxvi. Atatoa udhuru kwa sababu ya mwajili wake kumhitaji awe kazini;

xxvii. Itathibitika kwamba alikuwa na wito kwa vyombo vya dola mfano mahakamani au polisi;

xxviii. Atatoa udhuru wa safari ambayo aliipanga kabla ya kupokea wito wa baraza la wazee

### 5.60. BARAZA LA WAZEE WA CHAMA WILAYA:

a) Kutakuwa na baraza la wazee wanaotokana na umoja katika kila ngazi ya uongozi.
b) Wajumbe wa mabaraza hayo watakuwa wazee wote kuanzia miaka hamsini (50) na kuendelea.
c) Kamati ya wazee katika ngazi zote itapatikana kwa kuteuliwa na viongozi wakuu wa umoja katika ngazi husika.
d) Baraza la wazee katika ngazi husika itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (05) na baraza hilo wajumbe wake watachagua mwenyekiti na katibu na watakaobaki watakuwa wajumbe wa baraza hilo.

**Katika kuteuwa wajumbe wa baraza hilo la wazee baraza litazingatia:**

a) Uwezo wa mzee katika uelewa wa masuala ya Umoja;
b) Uwezo wa mzee kuwa mkweli na asiyekuwa mwoga;
c) Uwezo wa kuheshimu na kufuata Katiba na Kanuni;
d) Uwezo wa kutunza siri za majadiliano na uamuzi; na
e) Umakini, kujitoa kwa moyo na jitihada za dhati katika kushughulikia masuala ya Umoja

### 5.61. MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE:

Baraza la wazee litakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kupokea, kupitia na kuteua wagombea katika kila ngazi husika ya uongozi;

ii. Kusuluhisha migogoro ya kiuongozi na kibinafsi kwa viongozi wa umoja.

iii. Katika kusuluhisha migogoro baraza litazingatia:

iv. Kurudisha maelewano baina ya viongozi;

v. Ushauri na siyo uamuzi;

vi. Kulinda maslahi mapana ya Umoja;
vii. Kutoa mawazo huru juu ya kiini cha tatizo;
viii. Kuzisaidia pande zinazohusika kuona ukweli;
ix. Kutumia busara na ushawishi ili kudhoofisha misimamo kinzani na
x. Kushughulikia migogoro iliyofikishwa mbele yake kwa maandishi na kiongozi yoyote wa ngazi husika au mjumbe yeyote wa Halmashauri.
xi. Barua ya kupeleka mgogoro mbele ya baraza la wazee sharti:
xii. Ielezee kiini cha mgogoro;
xiii. Wahusika katika mgogoro;
xiv. Hatua zilizochukuliwa kuutatua; na
xv. Taarifa nyingine zinazoweza kuisadia baraza la wazee katika kutatua mgogoro huo katika kutekeleza jukumu la usuluhishi baraza la wazee litawajibika:
xvi. Kutafuta taarifa kutoka kwa mtu yeyote juu ya mgogoro unaohitaji usuluhishi;
xvii. Kuwaita na kuongea na viongozi wanoahusika kwenye mgogoro huo; na
xviii. Mgogoro usipotatuliwa kuandaa taarifa fupi itakayowasilishwa kwenye kikao cha Halmashauri. kiongozi asipotii wito wa kumtaka afike mbele ya baraza la wazee:-
xix. baraza la wazee litatoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri;
xx. Halmashauri itamhoji kiongozi juu ya sababu za kukaidi wito wa baraza la wazee;
xxi. Halmashauri itakapojiridhisha kwamba kiongozi hakuwa na sababu za kutotii wito wa baraza la wazee itachukua hatua zifaazo ikiwa ni pamoja na kupendekeza Mkutano Mkuu umvue uongozi
xxii. Kiongozi hatachukuliwa kwamba hakukaidi wito wa baraza la wazee iwapo:
xxiii. Taarifa ya wito haikumfikia;
xxiv. Itathibitika kwamba alishindwa kufika mbele ya Kamati kwa sababu za ugonjwa;
xxv. Itathibitika kwamba ni kwa sababu ya msiba wa ndugu au jamaa wa karibu naye;
xxvi. Atatoa udhuru kwa sababu ya mwajili wake kumhitaji awe kazini;
xxvii. Itathibitika kwamba alikuwa na wito kwa vyombo vya dola mfano mahakamani au polisi;
xxviii. Atatoa udhuru wa safari ambayo aliipanga kabla ya kupokea wito wa baraza la waze

## 5.62. BARAZA LA WAZEE WA CHAMA MKOA:

a) Kutakuwa na baraza la wazee wanaotokana na umoja katika kila ngazi ya uongozi.
b) Wajumbe wa mabaraza hayo watakuwa wazee wote kuanzia miaka hamsini (50) na kuendelea.

c) Kamati ya wazee katika ngazi zote itapatikana kwa kuteuliwa na viongozi wakuu wa umoja katika ngazi husika.
d) Baraza la wazee katika ngazi husika itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (05) na baraza hilo wajumbe wake watachagua mwenyekiti na katibu na watakaobaki watakuwa wajumbe wa baraza hilo.

**Katika kuteuwa wajumbe wa baraza hilo la wazee baraza litazingatia:**

a) Uwezo wa mzee katika uelewa wa masuala ya Umoja;
b) Uwezo wa mzee kuwa mkweli na asiyekuwa mwoga.
c) Uwezo wa kuheshimu na kufuata Katiba na Kanuni.
d) Uwezo wa kutunza siri za majadiliano na uamuzi; na
e) Umakini, kujitoa kwa moyo na jitihada za dhati katika kushughulikia masuala ya Umoja.

## 5.63 MAJUKUMU YA BARAZA LA WAZEE:

Baraza la wazee litakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kupokea, kupitia na kuteua wagombea katika kila ngazi husika ya uongozi;
ii. Kusuluhisha migogoro ya kiuongozi na kibinafsi kwa viongozi wa umoja.
iii. Katika kusuluhisha migogoro baraza litazingatia:
iv. Kurudisha maelewano baina ya viongozi;
v. Ushauri na siyo uamuzi;
vi. Kulinda maslahi mapana ya Umoja;
vii. Kutoa mawazo huru juu ya kiini cha tatizo;
viii. Kuzisaidia pande zinazohusika kuona ukweli;
ix. Kutumia busara na ushawishi ili kudhoofisha misimamo kinzani na
x. Kushughulikia migogoro iliyofikishwa mbele yake kwa maandishi na kiongozi yoyote wa ngazi husika au mjumbe yeyote wa Halmashauri.
xi. Barua ya kupeleka mgogoro mbele ya baraza la wazee sharti:
xii. Ielezee kiini cha mgogoro;
xiii. Wahusika katika mgogoro;
xiv. Hatua zilizochukuliwa kuutatua; na
xv. Taarifa nyingine zinazoweza kuisadia baraza la wazee katika kutatua mgogoro huo katika kutekeleza jukumu la usuluhishi baraza la wazee litawajibika:
xvi. Kutafuta taarifa kutoka kwa mtu yeyote juu ya mgogoro unaohitaji usuluhishi;
xvii. Kuwaita na kuongea na viongozi wanoahusika kwenye mgogoro huo; na

xviii. Mgogoro usipotatuliwa kuandaa taarifa fupi itakayowasilishwa kwenye kikao cha Halmashauri. kiongozi asipotii wito wa kumtaka afike mbele ya baraza la wazee:-

xix. baraza la wazee litatoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri;

xx. Halmashauri itamhoji kiongozi juu ya sababu za kukaidi wito wa baraza la wazee;

xxi. Halmashauri itakapojiridhisha kwamba kiongozi hakuwa na sababu za kutotii wito wa baraza la wazee itachukua hatua zifaazo ikiwa ni pamoja na kupendekeza Mkutano Mkuu umvue uongozi

xxii. Kiongozi hatachukuliwa kwamba hakukaidi wito wa baraza la wazee iwapo:

xxiii. Taarifa ya wito haikumfikia;

xxiv. Itathibitika kwamba alishindwa kufika mbele ya Kamati kwa sababu za ugonjwa;

xxv. Itathibitika kwamba ni kwa sababu ya msiba wa ndugu au jamaa wa karibu naye;

xxvi. Atatoa udhuru kwa sababu ya mwajili wake kumhitaji awe kazini;

xxvii. Itathibitika kwamba alikuwa na wito kwa vyombo vya dola mfano mahakamani au polisi;

xxviii. Atatoa udhuru wa safari ambayo aliipanga kabla ya kupokea wito wa baraza la wazee

# SURA YA SITA:

## UCHAGUZI WA VIONGOZI KWENYE UMOJA NA SIFA ZAKE:

### 6.1 SIFA ZA KUWA KIONGOZI:

6.1.1 Sifa za kiongozi huweza kuwa na tafsiri mbalimbali, lakini Kwa malengo ya ibara hii sifa za kiongozi maana yake ni:

a) Kuzungumza na kujadiliana na watu.
b) Kueleza, kushawishi na kutoa ushauri unaojenga.
c) Kufanya kazi kwa vitendo ili kufikia malengo yanayotarajiwa.
d) Kuchukua wajibu kwaajili ya chama na kutoa mwelekeo, maelekezo na mpangilio.
e) Kutia moyo watu wengine ili kufikia malengo.
f) Kuwawezesha wale walio chini yake ili kutekeleza malengo yaliyowekwa.

6.1.2 Mafanikio ya umoja yatategemea uongozi bora uliopo, ili aweze kuongoza vizuri Kiongozi inabidi:

i. Awe mtu wa kutegemewa katika maamuzi
ii. Awe mwenye msimamo (asiye yumba yumba)
iii. Awe mwenye uwezo wa kujenga na kusimamia hoja sahihi kwa ujasiri na kwa kujiamini
iv. Awe mwadilifu katika mwenendo wake katika maisha kwa ujumla

v. Awe mwenye kujiamini katika eneo lake la majukumu na mwenye kujitoa kikamilifu katika utendaji
vi. Awe mwenye kuweza kufanya maamuzi ndani ya muda, kwa wakati mwafaka na kuyasimamia.
vii. Asiwe mbinafsi, kila wakati ajitolee kwa manufaa ya wengine kabla ya kufikiria atavyonufaika yeye.
viii. Asitumie nafasi yake kwa faida yake, watu wenye nasaba naye au uswahiba.
ix. Awe msema kweli daima na fitina kwake mwiko.
x. Awe ni mtu mwenye maarifa na ujuzi.
xi. Awe mwenye moyo wa kusamehe, asiwe mlipa kisasi.
xii. Asiwe na mabaya ya matumizi ya rasilimali zilizopo.
xiii. Awe ni mtu jasiri katika kukabiliiana na changamoto za taasisi.
xiv. Awe mbunifu, muwazi, mkweli na mwadilifu.
xv. Awe na uelewa kuhusu kanuni, sera, katiba, dira na dhima ya chama.
xvi. Awe mpashanaji habari mzuri wa kutumia mikondo rasmi ya mawasiliano.
xvii. Awe anajua kushughulikia mizozo, migongano na migogoro
xviii. Atambue kwamba binadamu hutofautiana katika sifa na uwezo wa kufikiri, utashi, huluka, tabia na imani.
xix. Asiwe na tama ya fedha
xx. Awe na uwezo wa kuwaunganisha wanachama katika mambo yanayowahusu.

6.1.3. Masharti ya kuwa kiongozi ndani ya chama;

i. Awe na umri angalau miaka 18 na kuendelea
ii. Asiwe mwajiriwa kwenye taasisi nyingine kwani atakosa muda wa kuwatumikia wanachama.
iii. Asiwe na kumbukumbu ya makosa ya jinai.
iv. Awe mtanzania wa kuzaliwa au kuasili.
v. Awe amejiunga na chama kwa muda usiopungua miezi sita na kuendelea.
vi. Awe mwendesha pikipiki ya magurudumu mawili au matatu
vii. Kiongozi ataruhusiwa kugombea nafasi yoyote ya uongozi kwa mihula miwili tu kwa nafasi ile ile isipokuwa anaruhusiwa kugombea nafasi nyingine yeyote

## 6.2. UCHAGUZI WA VIONGOZI NDANI YA CHAMA (UBOMA):

6.2.1. Uchaguzi wa viongozi ndani ya umoja;

a) Mkutano mkuu wa uchaguzi utaitishwa kila baada ya miaka mitano (5) ngazi ya mkoa, miaka minne (04) ngazi ya wilaya, miaka mitatu (03) ngazi ya kata na miaka (02) ngazi kituo.
b) Mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi ndani ya umoja utafanyika tarehe kumi na tano (15) mwezi November katika ngazi husika.
c) Mkutano mkuu wa uchaguzi utaitishwa na katibu wa umoja katika ngazi husika baada ya kushauriana na mwenyekiti wake.
d) Mwenyekiti atafungua mkutano mkuu wa uchaguzi na kuwakaribisha wajumbe wa kamati ya chaguzi wachukue nafasi yao.
e) Baada ya wajumbe wa kamati ya uchaguzi kujongea mbele, mwenyekiti wa umoja atatangaza kujiuzulu na hivyo kumaliza muda wa uongozi wake na viongozi wengine waliokuwa chini yake ambao ni:

i. Mwenyekiti.
ii. Makamu mwenyekiti.
iii. Katibu.
iv. Naibu katibu.
v. Mhasibu/au mweka hazina.
vi. Mmamizi mkuu wa nidhamu na
vii. Naibu msimamizi wa nidhamu na
viii. Kamati za kikatiba.

6.2.2. Kamati ya uchaguzi katika kujadili na kuteua wagombea wa uongozi wa chama katika nafasi mbalimbali za uongozi inakatazwa kujihusisha na mambo yafuatayo:

a) Ushabiki, ubaguzi wa kjinsia au ubaguzi mwingine wa moja kwa moja au usiokuwa wa moja kwa moja
b) Ushawishi wa viongozi au mtu yeyote ambaye si mjumbe wa kamati
c) Maslahi binafsi, undugu, ukabila au nasaba
d) Mitazamo ya kisiasa, mwegemeo wa imani za kidini na hali ya mtu kijamii.
e) Ubaguzi kwa misingi ya eneo analotokea mgombea.

6.2.3. Viongozi waliomaliza muda wao wa uongozi ngazi husika wataondoka meza kuu na kamati ya uchaguzi watachukua nafasi ili kusimamia uchaguzi.

i. Mchakato wa kuwapata viongozi wapya utaanza baada ya muhula wa kwanza wa viongozi walioko madarakani kumalizika.
ii. Mchakato wa uchaguzi wa kuwapata viongozi wapya katika ngazi husika utaanzia ngazi ya kituo, kata, wilaya na Mkoa

iii. Viongozi wa ngazi husika watawatangazi wanachama wao kuchukua fomu kwa katibu wa ngazi husika ndani ya wiki moja tu (siku 07).
iv. Baada ya wanachama kuchukua fomu hizo watazirejesha kwa katibu wa kamati ya uchaguzi wa ngazi husika ndani ya wiki moja (siku 07).
v. Baada ya kamati ya uchaguzi kupokea fomu hizo itafanya mchujo wa majina ya wagombea walioomba nafasi mbalimbali za uongozi ndani wiki moja (siku 07).
vi. Baada ya kamati kufanya mchujo wa wagombea kila nafasi itatakiwa kuwa na wagombea wafuatao:
vii. Ngazi ya Mkoa watano (05), ngazi ya wilaya wanne( 04), ngazi ya kata na watatu (03) ngazi ya kituo wawili (02)
viii. Baada ya mchakato huo wa mchujo majina hayo yaliyopitishwa kutoka kwenye ngazi husika yatawasilishwa kwenye Kamati ya uchaguzi ndani ya wiki moja (siku 7) kabla ya tarehe uchaguzi kutangazwa.

6.2.4. Katika kupendekeza majina uongozi wa ngazi husika utafanya yafuatayo;

a) Hautapendekeza jina la mwanachama ambaye hajamaliza miezi sita (06) tangu ajiunge na umoja.
b) Hautapendekeza jina la mwanachama ambaye ametumikia vipindi viwili katika nafasi hiyo hiyo ya uongozi.
c) Hautapendekeza jna la mwanachama aliyefukuzwa kwa makosa aliyoyatenda akiwa kiongozi ambayo yameianishwa kwa mujibu wa katiba hii na katiba ya nchi.
d) Hautapendekeza jina la mwanachama ambaye hajui kusoma na kuandika.
e) Hautapendekeza jina la mwanachama ambaye anafanya kazi ya bodaboda nje ya mkoa wa Arusha.
f) Hautapendekeza jina la mwanachama ambaye siyo hai kwa mujibu wa katiba ya umoja.

6.2.5**.** Katibu mkuu wa ngazi husika atakabidhi majina ya wagombea kwa kamati ya uchaguzi:

6.2.6. Baada ya kamati ya uchaguzi kupokea majina ya wagombea waliopendekezwa kutoka kwa katibu wa ngazi husika kamati itawajibika kufanya yafuatayo:

i. Itahifadhi majina ya wagombea wote kama alivyoyapokea toka kwa katibu wa ngazi husika.
ii. Mwenyekiti atakubaliana na kushauriana na katibu wa kamati ya uchaguzi kuitisha kikao cha uteuzi wa mwisho wa wagombea.
iii. Kikao cha kamati ya uchaguzi cha uteuzi wa wagombea kitakaa na kufanya mchujo wa kupitisha majina ya wagombea ndani ya wiki moja (siku 07) kabla ya tarehe ya uchaguzi kutangazwa.

iv. Akidi ya wajumbe wa kikao cha kamati ya uchaguzi ni kuanzia asilimia hamsini 50% n a kuendelea.

v. Baada ya kamati ya uchaguzi kufanya mchujo wa wagombea katika nafasi mbalimbali za uongozi itatangaza majina ya wagombea na kuyaweka wazi kwa wanachama ili wawajue wagombea husika.
vi. Kampeni zitaanza punde tu majina hayo yatakapotangazwa.
vii. Kampeni zitafungwa siku moja kabla ya tarehe ya uchaguzi.
viii. Ni kosa kisheria kwa mgombea yeyote kufanya kampeni siku ya uchaguzi na endapo atabainika kufanya hivyo kamati ya uchaguzi ikajiridhisha na kosa hilo atakuwa amepoteza sifa ya kuwa mgombea na jina lake litaondolewa kwenye orodha ya wagombea katika nafasi husika aliyoiomba.
ix. Baada ya kutangaza majina ya wagombea kutoka kamati ya uchaguzi katika ngazi husika katiba hii inatoa muda wa kufanya kampeni kama ifuatavyo:

a) Ngazi ya kituo wiki moja [siku 07]
b) Ngazi ya kata wiki mbili [siku 14]
c) Ngazi ya wilaya wiki tatu [siku 21]
d) Ngazi ya mkoa wiki nne [siku 28].

6.2.7. Kamati ya uchaguzi haitagawa karatasi za kupiga kura mpaka:

a) Wageni na wanachama wasiokuwa hai wametengewa nafasi maalumu ili wasipige kura.
b) Wagombea ambao majina yao yamekatwa na kamati ya uchaguzi kwa kukiuka taratibu za uchaguzi kwa mujibu wa katiba.
c) Kufanya uhakiki wa akidi ya wajumbe ipasavyo kwa mujibu wa katiba.
d) Itahakikisha kuna amani na utulivu wa kutosha ili kuwapa uhuru wapiga kura kutekeleza jukumu hilo kwa mujibu wa katiba.

6.2.8. Viongozi watachaguliwa kwa mtiririko ufuatao:

a) Mwenyekiti
b) Makamu mwenyekiti
c) Katibu
d) Naibu katibu
e) Mhasibu/au mweka hazina
f) Kiongozi wa mkuu wa nidhamu/Msimamizi Mkuu wa nidhamu
g) Naibu msimamizi wa nidhamu

6.2.9**.** Utaratibu wa kuwasimika viongozi waliochaguliwa kwenye umoja:

a) Washindi wa nafasi mbalimbali za uongozi watatangazwa baada ya zoezi la uchaguzi kukamilika.
b) Uchaguzi ukishakamilika mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi atawaalika viongozi waliochaguliwa kujongea mbele ili kuwatangaza rasmi.
c) Mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi atawatangazia wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi kushangilia viongozi waliochaguliwa.
d) Kushangilia viongozi ni kuashiria kwamba viongozi waliochaguliwa sasa wamesimikwa rasmi.

### 6.3. ADHABU MBALIMBALI ZA MWANACHAMA NDANI YA CHAMA:

6.3.1. Nini maana ya adhabu: Ni malipizi ambayo mtu hupewa kutokana na kosa alilofanya kwa makusudi au kwa bahati mbaya.

6.3.2. Umoja wa bodaboda Mkoa wa Arusha utakuwa na adhabu mbalimbali ndani ya chama kuanzia:

a. KITUO.
b. KATA.
c. WILAYA na
d. MKOA.

6.3.3. Mwanachama anaweza kuadhibiwa ngazi ya kituo endapo ataonekana ametenda yafuatayo;

**(a)** Amedharau uongozi au maelekezo yaliyopo kwa mujibu wa katiba katika ngazi husika.
**(b)** Atatoa lugha ya matusi, kupigana akiwa kwenye eneo lake la kazi lkn pia na kwa wateja wake.
**(c)** Mwanachama yeyote kwenye umoja kuwa na hali ya Ubaguzi kama vile; ukabila, udini, siasa n.k.
**(d)** Halipi ada au michango mbalimbali ya umoja kwa mujibu wa katiba.
**(e)** Kupaki kwenye kituo ambacho hajasajiliwa au eneo ambalo halijarasimishwa kuwa kituo (mvamizi).
**(f)** Ni marufuku kutumia vitu vifuatavyo unapokuwa kwenye eneo la kazi Kama vile; Bangi, Pombe, Mirungi, Unga, Sigara n.k.
**(g)** Kutofuata utaratibu au miongozo iliyowekwa ndani ya kituo husika.
**(h)** Kufanya michezo ya kunyanyua tairi ya pikipiki ya mbele juu, kupiga nirinda au kupiga resi akiwa kwenye kituo chake cha kazi.

**(i)** Kuhamasisha mgomo kwa wenzake pindi akiwa kwenye eneo lake la kazi.
**(j)** Kutoudhuria vikao au mikutano ya umoja katika ngazi husika.
**(k)** Kuchelewa muda wa kuhudhuria kikao au mkutano katika ngazi husika.
**(l)** Kujihusisha na mambo yafuatayo Kama vile: wizi wa kutumia pikipiki, uporaji (Tatu mzuka).
**(m)** Kujihusisha na makossa yoyote ya kijinai.
**(n)** Kumtania mwanachama mwenzake kwa maneno ya kashfa na kejeli.
**(o)** Kubeba abria zaidi ya mmoja yaani (Mshikaki).
(p) Kutokuwa na helmeti mbili ndani ya kituo kipindi akiendesha pikipiki yake.
**(q)** Kutofanya vitu vifuatavyo kwenye pikipiki yake ndani ya kituo chake
(r) Kufunga taa zenye mwanga mkali yaani sport right.
(s) Kubadilisha mfumo wa pikipiki.
(t) Kufunga Exosity inayopiga kelele(Trampa)
(u) Kufunga plate namba za kuchora na ambayo siyo plate namba orginal ya kutoka na pikipiki.
(v) Kuvaa malapa, sendo na viatu vyote ambavyo haviruhusiwi kwa mujibu wa sheria za umoja.

6.3.4. Makosa yote yaliyoorodheshwa katika kifungu 6.1.16 cha katiba hapo juu mwanachama ataadhibiwa katika ngazi ya juu yake endapo ataonekana kukaidi ngazi ya chini yake na faini zimetofautiana kila ngazi kwa mujibu wa katiba hii.

# SURA YA SABA:

## 7.0. MFUKO WA CHAMA.

## 7.1. MFUKO MKUU WA CHAMA:

7.1.1 Chama cha (UBOMA) kitakuwa na mfuko mkuu wa chama ambao utatumika kuendesha shughuli mbalimbali za chama kwa mujibu wa katiba hii.

7.1.2 Baada ya mfuko mkuu wa chama katiba hii inatambua kuwa kutakuwa na mifuko mbalimbali kuanzia ngazi ya **kituo**, **kata** na **wilaya** kwa ujumla.

7.1.3 Pia katiba hii inaelekeza ngazi zote zilizotajwa hapo juu fedha zote zitahifadhiwa kwenye akaunti bank na siyo vinginevyo.

7.1.4 Chama kitaendesha shughuli zake kutokana na mapato yatakayotokana na;

a) Viingilio vya wanachama wapya watakaojiunga na Umoja ngazi ya Kata
b) Ada ya kila mwezi kutoka kwa wanachama;
c) Adhabu za papo kwa papo
d) Adhabu zinazotokana na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu na Maadili
e) Kutunisha mfuko kwa njia ya
f) Harambee
g) Mnada
h) Faida itokanayo na mikopo;
i) Ruzuku ya aina yoyote itakayotolewa kwa mujibu wa sheria yoyote ya nchi
j) Faida itokanayo na uwekezaji; (miradi)
k) Misaada kutoka kwa watu binafsi au taasisi;

7. 1.5 Vyanzo vingine vitakavyoibuliwa na kuidhinishwa na Chama kwa mujibu wa Katiba hii.

7.1.6 Mapato hayo yatatumika kwa mujibu wa kanuni za fedha na utaratibu uliowekwa na Katiba hii.

7.1.7 Sambamba na Katiba hii, Baraza Kuu litapokea, kujadili na kupitisha pendekezo la Kanuni za Fedha au mabadiliko ya kanuni hizo ambayo hayatakinzana na Katiba hii.

## 7.2. UTUNZAJI WA FEDHA ZA CHAMA:

7.2.1 Chama kitafungua na kusimamia akaunti ya benki ambayo itahifadhi mapato yote ya Chama.

7.2.2 Mwekahazina wa chama kwa kushirikiana na katibu mkuu wa chama atawajibika kuwasilisha kwa wakati gawio la michango ya ada kwenye kituo,kata,na wilaya mara tu michango hiyo inapowasilishwa kwenye mfuko mkuu wa Chama.

7.2.3 Utaratibu wa utoaji fedha benki, uidhinishwaji wa fedha na utunzaji wa vitabu vya kumbukumbu za hesabu utaainishwa kwenye Kanuni za Fedha.

7.2.4 Mwaka wa fedha wa Chama utaanza mwanzo wa mwezi Januari na kuishia mwisho wa Mwezi Disemba mwaka unaofuata.

7.2.5 Bajeti ya Chama itaandaliwa na kamati kuu ya Chama, kujadiliwa na Kamati ya Fedha uchumi na Mipango, Kamati Kuu ya Chama na kuwasilishwa mkutano mkuu kwa ajili ya kuidhishwa rasmi.

7.2.6 Matumizi yoyote yatakayokuwa ya dharura na ambayo yatatokea nje ya bajeti iliyopitishwa na mkutano mkuu, yatatakiwa kuidhinishwa na halimashauri kuu na Taarifa yake itapelekwa kwenye kikao kinachofuata cha mkutano mkuu kwa Taarifa.

7.2.7 Mkutano mkuu utakuwa na mamlaka ya kuhoji na kuchukua hatua stahiki pale ambapo itaonekana matumizi ya Chama yameenda kinyume na bajeti iliyopitishwa na kwamba Kamati Kuu imeshindwa kueleza mambo yaliyosababisha kuwa na matumizi nje ya bajeti.

## 7.3. UKAGUZI WA FEDHA ZA CHAMA

7.3.1 Chama, pale itakapowezekana, kitaajiri Afisa wa Chama atakayekuwa ni Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za Fedha za Chama;

7.3.2 Hesabu za fedha na mali za Chama – Mkoa zitakaguliwa mara moja kwa mwaka na Mkaguzi wa nje mahsusi aliyeteuliwa na Kamati Kuu na kuthibitishwa na mkutano mkuu.

7.3.4 Kamati kuu itapendekeza muda wa mkataba wa mkaguzi wa nje wa hesabu za fedha za chama.

7.3.5 Mkutano mkuu utapokea taarifa ya ukaguzi wa hesabu za fedha na mali za chama kutoka kwa Kamati Kuu, litajadili na kuidhinisha Taarifa hiyo au kutoa maelekezo au mapendekezo mahsusi kwa Kamati Kuu.

7.3.6 Taarifa za wanachama pamoja na mahesabu yaliyokaguliwa, yatapelekwa kwenye mkutano mkuu kwa Taarifa kila baada ya miaka miwili..

7.3.7 Mweka hazina wa chama ataratibu ukaguzi wa matumizi ya fedha za Chama ngazi ya kituo, kata,na wilaya kwa kila mwaka na Taarifa yake itawasilishwa kwenye Kamati Kuu baada ya kujadiliwa na Kamati ya Fedha uchumi na Mipango.

## 7.4. UWAJIBIKAJI KWENYE MASWALA YA FEDHA;

7.4.1 Mtumishi wa Chama, Kiongozi au Mwanachama yoyote ana wajibu wa kutunza fedha na mali za Chama kwa uangalifu mkubwa.

7.4.2 Chama kitachukua hatua za Kisheria dhidi ya Mtumishi, Mwanachama au Kiongozi yoyote wa Chama atakayebainika kufanya ubadhilifu wa fedha au mali za Chama na katika kufanya hivyo Chama kinaweza kushirikisha mamlaka yoyote ili kuweza kufidia ubadhilifu uliojitokeza.

## 7.5. UTARATIBU WA UTOAJI POSHO;

7.5.1 Chama kitaandaa kanuni za fedha ambazo pamoja na mambo mengine zitaweka utaratibu na viwango vya posho mbalimbali kwa viongozi wa Chama.

7.5.2 Viongozi wafuatao wa Kamati Kuu ya Chama kila ngazi watalipwa posho ya madaraka kwa kuzingatia viwango vitakavyowekwa kwenye Kanuni za Fedha na kuidhinishwa na mkutano mkuu wa Chama kila ngazi watakaolipwa posho ni:

(a) Mwenyekiti
(b) Katibu mkuu
(c) Naibu katibu mkuu
(d) Mweka Hazina
(e) Watunza nidhamu na viongozi wa kamati za kikatiba.

7.5.3. Kanuni za fedha zitaweka viwango vya posho za safari na vikao mbalimbali kwa Wajumbe wote wa Kamati Kuu.

7.5.4. Pendekezo la viwango vya posho litaandaliwa na halimashauri kuu ya Chama, kujadiliwa na Kamati Kuu na kuwasilishwa mkutano mkuu kwa majadiliano na kutolea maamuzi.

7.5.5. Katika kujadili na kufanya maamuzi juu ya pendekezo la posho za viongozi, mkutano mkuu utazingatia mambo yafuatayo;

(a) Nafasi ya Kiongozi ndani ya Chama na majukumu aliyonayo ndani ya Chama.
(b) Kuongeza motisha na morali ya kazi na kuwatia nguvu viongozi katika kujitoa ili kutetea maslahi ya wanachama katika ngazi mbalimbali.
(c) Hali ya kifedha ndani ya Chama na umuhimu wa kutotumia rasilimali kubwa ya Chama kwa malipo ya posho.
(d) Umuhimu wa kufanya Chama kiweze kuwekeza katika miradi mingine ya Kiuchumi na hivyo kuimarisha akiba ya Chama kifedha.
(e) Mwekahazina atahakikisha kumbukumbu zote za malipo kwa viongozi zinatunzwa vyema na kwamba taarifa ya malipo hayo inakuwa ni sehemu ya taarifa ya fedha itakayojadiliwa katika vikao husika kwa mujibu wa Katiba hii.

(f) Mwekahazina wa chama atakuwa na mamlaka ya kuidhinisha malipo yote ya Posho na atakuwa na wajibu wa kusimamia miongozo ndani ya Chama inayoainisha malipo yote ya posho

(g) Mwekahazina atakuwa ni Afisa Masuuli wa Chama na endapo kutafanyika malipo au matumizi yoyote ndani ya Chama pasipo kufuata utaratibu, atawajibika moja kwa moja mbele ya Kamati Kuu na vyombo vingine vya juu vya Chama na hatua stahiki za kinidhamu zitachukuliwa kwake endapo atashindwa kutafsiri au kuzembea katika kuidhinisha malipo yoyote bila kufuata miongozo ya Chama.

7.5.6. Mfuko mkuu wa Umoja utatumika kwa mambo yafuatayo:

a) Kutoa huduma zilizoainishwa na katiba hii na viwango vyake kutajwa kwenye kanuni;
b) Kugharamia vikao vya Umoja na uendeshaji wa Umoja;
c) Uwekezaji kwenye SACCOS; na
d) Uwekezaji kwenye miradi.
e) Kulipa kodi ya pango ya kila mwezi ya ofisi ya bodaboda mkoa.
f) Uendeshaji wa gharama za ofisi ya bodaboda mkoa.
g) Gharama za maandalizi ya mikutano.
h) Posho za vikao.
i) Posho za utatuzi wa migogoro ya wanachama ngazi ya mkoa.
j) Gharama za Safari za viongozi.
k) Kuhudumia wanachama katika ajali na vifo vinavyotambulika kikatiba.
l) Malipo ya mishahara kwa waajiriwa na chama.
m) Malipo ya kuendeshea kesi katika kulinda haki za Chama na mwanachama.
n) Malipo ya adhabu yoyote iliyotolewa dhidi ya Chama
o) Uwekezaji Kama itakavyoamuliwa na chama.
p) Malipo ya ushirikishwaji wa Chama.
q) Malipo mengine halali kwa manufaa ya chama
r) Malipo ya mafunzo na semina kwa viongozi na wanachama wenyewe
s) Malipo ya safari mbalimbali na posho za viongozi ngazi ya wilaya katika uwakilishi wa chama.

7.5.7. Masharti yafuatayo yatatawala uwekaji fedha kwenye mfuko mkuu wa chama;

a) Kila mwanachama atalipa ada ya kila mwezi na michango mbalimbali ya chama kupitia mifumo rasmi iliyowekwa na katiba hii.
b) Malipo yoyote yaliyofanywa na mwanachama mwekahazina wa chama atahakikisha anayakatia stakabadhi ya malipo.
c) Fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya mfuko mkuu zitawekwa kwenye akaunti za umoja;

d) Malipo yote yaliyofanyika ngazi ya kituo, na kata na wilaya yatakatiwa stakabadhi na mweka hazina wa kata au wilaya ambayo pekee ndiyo uthibitisho wa malipo hayo;
e) Malipo yatahesabika kuwa yamefanyika baada ya kupokea stakabadhi ya Umoja ngazi ya mkoa;
f) Fedha itatolewa kwenye akaunti pamoja na hundi kwa watia saini wawili kati ya watatu
g) Watia saini kwenye akaunti pamoja na hundi watachaguliwa na Halmashauri ya Umoja;
h) Watia saini kwenye akaunti ya umoja wawe wanaweza kupatikana Kwa urahisi.
i) Mifuko yote ya umoja kuanzia kituo na kata na mkoa itakuwa chini ya usimamizi wa mfuko Mkuu

7.5.8. Mazingira yanayoruhusiwa kupokea Fedha Taslim;

7.5.9. Viongozi wanaruhusiwa kupokea fedha taslimu inayotokana na:
a) Mnada na ambayo imelipwa wakati mnada unaendelea au mara tu baada ya kumalizika;
b) Harambee wakati inaendelea au mara tu baada ya kumalizika;
c) Malipo yoyote yaliyofanywa na mtu ambaye siyo mwanaumoja;
d) Zawadi iliyotolewa papo hapo; na
e) Fedha nyingine ambayo itapokelewa Kwa mazingira yaliyoruhusiwa na Halmashauri.

7.5.10 Bila kuathiri vifungu vingine vya katiba, itakuwa kinyume cha masharti ya Katiba hii kwa:
a) Mwanaumoja yeyote kulipa fedha taslimu Kwa kiongozi; na
b) Kiongozi yeyote kupokea fedha taslim kutoka Kwa mwanaumoja Yeyote.

7.5.11. Kiongozi atakayekiuka katazo la kupokea fedha taslim:
a) Atakuwa ametenda kosa;
b) Atafikishwa mbele ya Kamati ya Nidhamu na Maadili; na
c) Atawajibika kutekeleza uamuzi wa Kamati ya Nidhamu.

7.5.12. Matumizi ya mfuko ngazi ya kata yatakuwa Kama ifuatavyo:
a) Kulipa kodi ya pango ya kila mwezi ya ofisi ya kata.
b) Uendeshaji wa gharama za ofisi ya bodaboda kata.
c) Gharama za maandalizi ya mikutano ndani ya kata.
d) Posho za vikao ngazi ya kata.
e) Posho za utatuzi wa migogoro ya wanachama ngazi ya kata.
f) Gharama za Safari za viongozi ngazi ya kata.
g) Kuhudumia wanachama waliopata ajali na vifo vinavyotambulika kikatiba.
h) Uwekezaji Kama itakavyoamuliwa na chama.
i) Malipo mengine halali kwa manufaa ya chama.

7.5.13. Matumizi ya mfuko ngazi ya Kituo yatakuwa Kama ifuatavyo:
a) Gharama za maandalizi mkutano wa kituo
b) Posho za viongozi wa kituo wanapoitwa kwenye vikao vya chama

c) Posho za viongozi wa kituo wakati wa utatuzi wa migogoro ya wanachama wao.
d) Kuhudumia wanachama katika ajali na vifo vinavyotambulika kikatiba.

7.5.14. Umoja utatoa mikopo midogomidogo kwa wanaumoja kwa mashartiya fuatayo:

a. Muda wa kulipa mkopo na riba yake ni miezi minne;
b. Mkopo utarejeshwa katika marejesho manne kwa utaratibu wa kurejesha kila mwezi 25% au zaidi ya mkopo wote pamoja na riba; na
c. Mkopo utatozwa riba yaasilimia 10 kwa kipindi chote cha miezi minne.
d. Mkopo hautatolewa mpaka:
e. Mwanaumoja awe ametimiza mwaka mmoja tangu kujiunga na Umoja;

7.5.15 Mkopaji awe amejaza fomu ya maombi ya mkopo na kudhaminiwa na

f. Wadhamini wasiopungua wawili;
g. Kamati Kuu iwe imejiridhisha kwamba mkopaji hajawahi kushindwa kulipa
h. Mkopo;
i. Kama aliwahikushindwa kulipa mkopo ithibitike kwamba alishalipa hela ya
j. Wadhamini ambayo walimlipia kwa mkopo alioshindwa kurejesha;
k. Mkopaji na wadhamini wake wawe wanaumoja hai; na
l. Awe nauwezo wa kurejesha.
m. Kuchelewesha Mkopo
n. Atakayecheleweshа mkopo:
o. Atatozwa adhabu ya asilimi 10 ya mkopo wote pamoja na riba yake iwapo
p. Atalipa ndani ya siku thelathini tangu muda wakawaida wakulipa mkopo
q. Kuisha;
r. Mweka-Hazina atawajulisha wadhamini wa mkopaji baada ya mkopo
s. Kucheleweshwa siku 10;
t. Mkopaji na wadhamini watawajibika kulipa mkopo, riba na adhabu ndani ya
u. Siku 30 tangu muda wakawaida wa kulipa kuisha;
v. Siku 30 zikiisha bila kulipa mkopo mkopaji na wadhamini watafungiwa
w. huduma kwa kushindwa kulipa Mkopo
x. Iwapo wadhamini watalipa mkopo kabla au baada ya kufungiwa huduma:
y. Kwa maombi ya wadhamini mkopaji ataendelea kufungiwa huduma;
z. Kwa maombi ya wadhamini atafikishwa Kamati ya Nidhamu na Maadili; na
aa. Kama mkopaji ni kiongozi atapoteza nafasi yake ya uongozi.

# SURA YA NANE:

## 8.0. BODI YA WADHAMINI:

8.1. Muundo wa bodi ya Wadhamini.

8.2. Kutakuwa na bodi ya Wadhamini itakuwa na wajumbe watatu (3)

8.3. Bodi ya Wadhamini itateuliwa na kudumu kwa muhula mmoja wenye kipindi cha miaka mitano (5)

8.4. Uteuzi wa bodi ya wadhamini utafanywa na Mkutano Mkuu wa Chama mkoa kufuatia mapendekezo yatakayokuwa yametolewa na kamati Kuu

8.5. Baada ya uteuzi huo kufanyika atapatikana mwenyekiti wa bodi na katibu alafu atakayebaki ni mjumbe.

### 8.6. Sifa Za Kuwa Kwenye Bodi Ya Wadhamini.

8.6.1. Ili kuteuliwa kuwa mjumbe wa bodi ya Wadhamini, mtu atatakiwa kuwa sifa zifuatazo:

(a) Uadilifu unaokubalika na jamii inayomzunguka na pia jamii ya waendesha bodaboda.

(b) Awe na uwezo wa kuwa na mali isiyohamishika kama nyumba, kiwanja au anafanyabiashara na biashara hiyo iweze kuwa na thamani ya kuanzia milioni hamsini na kuendelea.

(c) Awe tayari na nia ya kukitumikia Chama katika nafasi hii.

(d) Asiwe ni kiongozi wa Chama cha siasa wakati wa kuteuliwa na muda wote atakaokuwa anahudumu katika nafasi ya udhamini ndani ya Chama.

(e) Awe ni mtu anayeweza kuwa na ushawishi mbele ya jamii au ndani ya wanachama wa bodaboda.

(f) Awe ni mtu mwenye uwezo wa kuheshimika kupitia uzoefu au mchango wake katika kazi alioutoa au anaoendelea kuutoa katika ngazi mbalimbali.

### 8.6.2 Kazi za bodi ya wadhamini.

8.6.3 Bodi ya wadhamini itakuwa na kazi zifuatazo;

(a) Kushauri Chama uendeshaji bora wa shughuli za Chama.

(b) Kushauri kuhusu usimamizi bora wa rasilimali za Chama

(c) Kushauri namna ya kutatua migogoro ya uongozi ndani ya Chama au masuala mbalimbali yanayohusu migogoro baina ya wafanyakazi na waajiri.

(d) Kusimamia Utunzaji wa hatimiliki za mali za Chama

(e) Kushawishi masuala mbalimbali kwa wafadhili, waajiri na pia serikalini kwa manufaa ya Chama.

(f) Katibu Mkuu atahakikisha, kupitia maelekezo ya Kamati Kuu, kuwa bodi ya wadhamini linapewa ushirikiano wa kutosha ndani ya Chama ili kuweza kutimiza majukumu yake.

## 8.6.4 Haki za bodi ya wadhamini.

8.11. Katika utekelezaji wa kazi zake,

8.12. Bodi ya wadhamini itakuwa na haki zifuatazo;

(a) Haki ya kuomba na kupatiwa taarifa zote zinazohusu mali za Chama na taarifa zote za ukaguzi zinazohusu mali hizo.
(b) Haki ya kutoa ushauri kwa jambo lolote lile ambalo wajumbe wa kamati kuu wataona inafaa.
(c) Haki ya kuomba na kuruhusiwa kuhudhuria kikao cha Mkutano Mkuu wa Chama ili kushuhudia shughuli mbalimbali zitakazokuwa zinaendelea ndani ya kikao husika.
(d) Haki ya kutembelea ofisi za Makao Makuu ya Chama na kujionea shughuli mbalimbali za Chama.
(e) Haki ya kulipiwa gharama zote za usafiri na posho za vikao kwa viwango vitakavyoainishwa kwenye Kanuni za fedha wanapokuwa wakitimiza majukumu yao.
(f) Wajumbe wa Baraza la Wadhamini hawatatakiwa;
(g) Kutoa siri za Chama Kwa watu wasiohusika isipokuwa pale wanapotakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria za nchi.
(h) Kuingilia shughuli za utendaji ndani ya Chama au maamuzi halali yanayopitishwa na vikao vya Chama.
(i) Bodi ya Wadhamini watakutana mara moja kwa mwaka katika Kikao ambacho kitahudhuriwa na Wajumbe wote wa Kamati Kuu ambapo;
(j) Mwenyekiti wa Chama mkoa atatoa Taarifa ya kina ya maendeleo ya Chama kwa kipindi hicho.
(k) Watapokea changamoto mbalimbali ambazo Chama kinakabiliana nazo na kushauri namna ya kutatua changamoto hizo au kutoa msaada mwingine wowote katika utatuzi wa changamoto hizo
(l) Watapokea taarifa za vikao vyote vilivyofanyika vya halimashauri kuu na Mkutano Mkuu pamoja na taarifa ya ukaguzi wa mali za Chama kwa kipindi cha miaka miwili.

## 8.13. Ukomo wa Ujumbe wa bodi ya Wadhamini.

Nafasi ya Mjumbe wa bodi itahesabika kuwa wazi endapo jambo lolote kati ya haya yafuatayo litatokea;

(a) Mkutano Mkuu wa Chama mkoa kupitia pendekezo litakalokuwa limetoka, halmashauri kuu itaazimia kuwa mjumbe amekosa sifa za kuendelea kuwa mjumbe wa bodi ya Wadhamini.
(b) Mjumbe kujiuzuru
(c) Mjumbe kufariki dunia
(d) Mjumbe kuteuliwa katika nafasi ya Uongozi ndani ya Chama cha siasa
(e) Mjumbe kushtakiwa na kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai lenye Kifungo cha zaidi ya miezi sita au kosa lolote linalohusiana na rushwa au udhalilishaji wa kijinsia.
(f) Kushindwa kutimiza majukumu yake kwa sababu za ugonjwa.

(g) Kamati Kuu itakuwa na wajibu wa kutoa taarifa halimashauri Kuu kuhusiana na kuwa wazi kwa nafasi ya mjumbe yeyote wa halimashauri kuu na kuwasilisha pendekezo la kujazwa kwa nafasi hiyo

# SURA YA TISA:

## 9.1. TARATIBU ZA AJIRA, UTUMISHI NA USIMAMIZI WA WATENDAJI

9.2. Aina za ajira na nafasi za kuajiriwa.
9.3. Chama kitaajiri watumishi kwa ngazi mbalimbali katika ofisi zake za Makao Makuu ili kuweza kutekeleza majukumu mbalimbali ya kiutendaji.
9.4. Ajira zote ndani ya Chama zitakuwa kwa mujibu wa katiba na waajiriwa wote watasainishwa mikataba ya kazi na chama.
9.5. Bila kuathiri masharti mengine yaliyotajwa katika Katiba hii, Chama kinaweza kuajiri watumishi kwa mikataba ya muda mfupi endapo itaonekana inafaa kufanya hivyo.

9.6. Chama kitaandaa Kanuni za Ajira na Utumishi ambazo zitaainisha masuala mbalimbali ya utumishi ikiwemo;
9.7. Sifa za mtu kuajiriwa katika nafasi mbalimbali
9.9. Viwango vya mishahara kwa kila nafasi ya ajira
9.10. Majukumu ya kila ngazi ya ajira
9.11. Utaratibu wa kupanda cheo au ngazi ya mshahara
9.12. Taratibu za kinidhamu kwa watumishi.

9.13. Sifa za mtumishi kuteuliwa kuongoza Ofisi yoyote ndani ya Chama na Maslahi mengine ya watumishi.
9.14. Kamati kuu ya chama itahusika na utaratibu wa kuajiri watumishi wote chini yake.
9.15. Kamati kuu itaandaa mapendekezo ya watumishi wanaopaswa kuongoza Ofisi mbalimbali ndani ya Chama na mapendekezo hayo yatajadiliwa na kutolewa maamuzi na halimashauri Kuu.

9.16. Mamlaka ya Mwisho ya maamuzi ya kinidhamu kwa watumishi wote, itakuwa ni Kamati Kuu ya Chama.
9.17. Nafasi ya Katibu Mkuu katika usimamizi wa Watumishi
9.18. Katibu Mkuu atakuwa ni;
9.19. Afisa Mtendaji Mkuu wa Chama katika masuala yote ya kiutendaji na usimamizi wa shughuli za kila siku za Menejimenti ya Chama.
9.20. Msimamizi mkuu wa nidhamu ya watumishi mbalimbali walioajiriwa na Chama.
9.21. Mratibu wa zoezi la kuajiri watumishi kwa mujibu wa taratibu zitakazoelezwa ndani ya Kanuni na kuwasilisha mapendekezo yote ya ajira mbele ya Kamati Kuu kwa maamuzi.

9.22. Mtekelezaji Mkuu wa jambo lingine lolote linalohusu utendaji wa kila siku wa Chama na atawajibika mbele ya Kamati Kuu kwa jambo lolote litakalotekelezwa na Mtumishi aliye chini yake kwa jina la Chama

9.23. Katika kutoa mapendekezo ya nafasi yoyote ya Kiutawala ndani ya Chama, pamoja na sifa nyingine zitakazoainishwa kwenye Kanuni, Katibu Mkuu atatakiwa kuzingatia yafuatayo;

9.24. Uzoefu kazini alionao mtumishi husika

9.25. Uwiano wa kijinsia hasa pale inapotokea kuna watumishi wenye sifa zilizolingana

9.26. Tabia njema na uwezo wa kuongoza walio chini yake

9.27**. Utaratibu wa kuandaa Mikataba ya Ajira.**

9.28. Kila Mtumishi atakayeajiriwa atasaini Mkataba wa ajira na kumbukumbu za Mkataba huo kuhifadhiwa Makao Makuu ya Chama

9.29. Utaratibu na muundo wa mkataba wa ajira utaainishwa katika Kanuni za Utumishi.

9.30. **Kanuni za Utumishi**

9.31. Kanuni za Utumishi zilizokuwepo wakati Katiba hii ikipitishwa, zitaendelea kufanya kazi kwa kipindi chote ambacho Kanuni mpya zitakuwa zikiandaliwa ili kuendana na misingi ya Katiba hii.

9.32. Kanuni mpya za Utumishi zitazingatia Mikataba iliyopo sasa ya ajira na kuhuisha masharti ya Mikataba hiyo kwa mujibu wa misingi ya Katiba hii.

9.33. Endapo kutatokea mgongano wa kimaslahi baina ya Mikataba iliyopo sasa ya watumishi au mtumishi yeyote na Kanuni zitakazopendekezwa, Mtumishi atapewa haki ya kuchagua kuendelea na maslahi aliyonayo sasa ama kukubaliana na masharti mapya kulingana na kile ambacho Mtumishi ataona ni bora zaidi kwake.

9.34.Endapo Mtumishi aliyeajiriwa kabla ya kupitishwa kwa Katiba hii ameajiriwa kwa mkataba usio wa kudumu, basi atapewa haki ya kuendelea na masharti ya Mkataba wake mpaka utakapofika mwisho na atalazimika kukubaliana na masharti mapya ya ajira ili kuweza kuongezewa mkataba mpya wa ajira usio wa kudumu.

9.35. Viwango vya mishahara na stahiki nyinginezo za Watumishi vitazingatia uwezo wa Chama na rasilimali zilizopo na pia umuhimu wa kutumia rasilimali hizo katika shughuli nyingine za maendeleo ndani ya Chama.

9.36. Mtumishi yeyote atakayeteuliwa kushika nafasi ya Utawala atatakiwa kufanyiwa tathmini ya utendaji wake wa kazi kila baada ya miaka mitatu ili kuweza kuteuliwa tena kuendelea kushikilia nafasi hiyo ya Kiutawala.

9.37. Kanuni mpya za Utumishi zitawasilishwa mbele ya halimashauri Kuu ili kuweza kupata idhini ya kuanza kutumika.

# SURA YA KUMI:

## 10.0. MENGINEYO

### 10.1. Utaratibu wa Kutengeneza Kanuni

10.2. Kamati Kuu itakuwa na wajibu wa kuratibu mchakato wowote wa uundwaji wa Kanuni za Chama isipokuwa pale ambapo imeelezwa tofauti ndani ya Katiba hii.

10.3. Kamati Kuu inaweza kuazimia kuundwa kwa Kamati ndogo ya wataalamu watakaoandaa rasimu ya Kanuni ambazo zitawasilishwa kwa Katibu Mkuu ili ziweze kujadiliwa na Kamati Kuu na hatimaye kuwasilishwa mbele ya halmashauri kuu ya chama ili kupata idhini.

10.4. Halmashauri itakuwa ni chombo cha mwisho cha kufanya maamuzi kuhusu uundwaji na upitishwaji wa Kanuni isipokuwa pale ambapo imeelezwa tofauti ndani ya Katiba hii.

10.5. Kanuni zitakazoidhinishwa na halmashauri kuu, zitawasilishwa kwenye Kikao kinachofuata cha Mkutano Mkuu kwa taarifa.

10.6. Mkutano Mkuu wa Chama unaweza kuazimia kwa kura ya wajumbe wasiopungua 2/3 waliohudhuria kikao husika, kufuta kipengele, sehemu au kanuni husika endapo Mkutano Mkuu utaridhika kuwa utaratibu wa kutengeneza Kanuni ulikiukwa au Kipengele, sehemu au Kanuni husika zinakinzana na Katiba hii au kanuni husika hazina maslahi kwa Chama.

### 10.7. Taratibu za ada ya uwakala

10.8. Chama kinaweza kuingia kwenye makubaliano na taasisi yoyote ya serikali au binafsi ili kuweza kupata tozo ya ada ya uwakala kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

10.9. Mgawanyo wa makusanyo ya ada ya uwakala utakuwa sawa na mgawanyo wa michango mingine ya ada za wanachama inayokusanywa kutoka kituo, kata na wilaya husika.

10.11. Makusanyo ya ada ya uwakala yatakuwa na akaunti tofauti na makusanyo mengine na yatatumika katika matukio au shughuli zitakazoratibiwa na Chama zikihusisha wanachama wote.

### 10.12. Kipindi cha Mpito

10.13. Viongozi wote wa vituo,kata, wilaya na Viongozi wa Chama mkoa waliopo wakati wa kupitishwa Katiba hii wataendelea na nafasi zao kwa kipindi cha miaka miwili toka tarehe ambayo Msajili wa Vyama kutoka wizara ya mambo ya ndani ya nchi ataidhinisha Katiba hii na baada ya hapo viongozi wa Chama mkoa wataratibu uchaguzi wa viongozi ngazi ya kituo, kata,wilaya na baadae mkoa.

10.14. Masharti yaliyomo katika Katiba hii kuhusiana na muundo wa Menejimenti ya Chama na masuala ya wafanyakazi walioajiriwa au watakaoajiriwa na Chama yataanza kutumika mara baada ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi kuidhinisha Katiba hii.

10.15. Viongozi wa Kamati kuu ya mkoa watakaokuwepo wakati wa kupitishwa kwa Katiba hii watakuwa ni wajumbe wa Mpito wa Kamati Kuu ya Chama wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama mkoa kwa kipindi chote cha mpito kabla ya kuitishwa kwa Uchaguzi Mkuu.

10.16. Katibu Mkuu wa Chama wa sasa au kiongozi yeyote atakayekuwa anakaimu nafasi hiyo atakaimu nafasi ya Katibu Mkuu wa Chama ili kuweza kuongoza Menejimenti ya Chama katika kipindi cha Mwaka mmoja wa mpito ili kuandaa mazingira upya ya kiutendaji ndani ya Chama.

10.17. Muundo wa halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu utaendelea kama ulivyo sasa kwa kipindi cha mpito cha miaka miwili mpaka pale uchaguzi Mkuu mpya wa vituo,kata, wilaya na mkoa utakapofanyika kwa mujibu wa Katiba hii.

## 10.18. TARATIBU ZA USHIRIKIANO NA VYAMA AU TAASISI NYINGINE:

10.19. Ushirikiano na Taasisi za Serikali.

10.20. Katika kutekeleza majukumu yake kwa maslahi ya Wanachama wake, Chama kitashirikiana na Serikali na taasisi zake na kushiriki katika masuala yanayohusiana na wanachama na maslahi yao.

10.21. Chama kitajiepusha na shughuli zenye mwelekeo wa kuwagawa wanachama wake kwa misingi ya kisiasa, kikabila au kidini.

10.23. Chama kitashiriki kutoa ushauri kwa serikali na taasisi zake kwa malengo ya kushawishi masuala yenye manufaa na tija kwa wanachama.

10.24. Chama kitashirikiana na serikali katika majadiliano yoyote chini ya serikali yenye malengo ya kuboresha maslahi bora kwa wanachama na kudumisha uhusiano mwema.

## 10.25. Ushirikiano na Vyama rafiki au vyenye mlengo sawa

10.26. Chama kitaendelea kuimarisha ushirikiano na vyama vingine vya Bodaboda hapa nchini katika masuala mbalimbali yahusuyo haki na maslahi ya wanachama.

10.27. Chama, kwa kupitia azimio litakalopitishwa na zaidi ya nusu ya wajumbe watakaohudhuria wa Mkutano Mkuu, kinaweza kujiunga na shirikisho/mashirikisho ya vyama vya bodaboda kwa mujibu wa sheria.

10.28. Chama kitashirikiana na vyama vingine kwa mujibu wa sheria kuweza kutetea kwa sauti moja maslahi ya wanachama wake.

### 10.29. Utaratibu wa kuunganisha vyama

108.1. Endapo yatatokea maombi au wazo lolote la kutaka kuunganisha Chama hiki na Chama kingine ili kuwa Chama kimoja chenye malengo ya kutetea haki za wanachama, jambo hilo litafanyiwa maamuzi na Mkutano Mkuu wa Chama.
10.30. Kuunganisha Chama hiki na Chama kingine na hivyo kuzaa Chama kipya kutamaanisha kuvunjwa rasmi kwa UBOMA na kuunda chama kipya cha bodaboda.
10.31. Wazo lolote la kuunganisha Chama hiki na chama kingine litaanza kujadiliwa katika ngazi ya vituo, kata, wilaya na mkoa na Mkutano Mkuu wa Chama utakuwa na maamuzi ya mwisho kupitia kura ya siri ya zaidi ya theruthi mbili ya wajumbe wa Mkutano Mkuu.

### 10.32. Uwakilishi kwenye mialiko mbalimbali

10.33. Katika matukio yote ya mkoa, Chama kitawakilishwa na Mwenyekiti wa Chama mkoa.
10.34. Mwenyekiti wa Chama mkoa, anaweza kuteua mwakilishi mwingine endapo atakuwa na majukumu mengine au udhuru wowote. 10.35. Katibu Mkuu atakuwa ni sehemu ya uwakilishi wa Chama katika vikao vya kiutendaji ambavyo vinapokea maelekezo au maagizo kutoka serikalini au taasisi nyingine zinazoshirikiana na Chama

## SURA YA KUMI NA MOJA:

### 11.0. MAREKEBISHO YA KATIBA:

11.1. Katiba hii na vipengele vyake vinaweza kurekebishwa na mkutano mkuu iwapo theluthi mbili 2/3 ya

11.2. Wanachama waliohudhuria watapapiga Kura ya kuunga mkono wa urekebishwaji huo.

11.3. Endapo kutakuwa na hoja ya mabadiliko ya kipengele au sehemu yoyote ya Katiba hii au kuundwa Katiba mpya, hoja hiyo itawasilishwa kwa Katibu Mkuu kwa njia ya maandishi baada ya kujadiliwa kwenye ngazi ya mkutano mkuu wa tawi husika

11.4. Endapo hoja husika imeanzia ngazi ya Kamati Kuu, Kamati Kuu itaandaa hoja hiyo kwa maandishi, baada ya mjadala ndani ya Kamati Kuu, na kuwasilisha pendekezo lililoandaliwa kitaalamu kwa Baraza Kuu ili kuweza kupata idhini ya kupeleka jambo hilo katika Mkutano Mkuu.

11.5Bila kuathiri taratibu nyingine zozote, nia ya kufanya mabadiliko yoyote ya Kipengele au sehemu ya Katiba hii au uundwaji wa Katiba Mpya itatangazwa katika matawi yote ya Chama na Katibu Mkuu mara baada ya azimio la kufanya hivyo kupitishwa na Baraza Kuu

11.5. Endapo pendekezo litakalowasilishwa kwenye Baraza Kuu litahusu mabadiliko ya kipengele au sehemu ya Katiba hii, Baraza Kuu linaweza kuidhinisha uandaaji wa rasimu yenye kueleza sababu za mabadiliko hayo na vipengele vitakavyobadilishwa na rasimu hiyo, baada ya kujadiliwa na Kamati Kuu itawasilishwa Baraza Kuu na hatimaye Mkutano Mkuu ili kuweza kupitishwa.

11.6. Baraza Kuu linaweza kupinga wazo lolote la kufanya mabadiliko au uundwaji wa Katiba mpya endapo itaonekana kuwa hakuna haja ya kufanyika hivyo na uamuzi huu utatakiwa uungwe mkono na zaidi ya nusu ya wajumbe waliohudhuria kikao husika

11.3. Mabadiliko ya Katiba yatafanyika kila baada ya miaka mitano.

11.4. Kamati Kuu itaunda Kamati ya Katiba na kuwasilisha majina ya wajumbe kwenye Halmashauri ya Umoja ambayo:

a) Inaweza kubadilisha muundo, idadi na aina ya wajumbe wa Kamati ya katiba iwapo
b) Kuna sababu za msingi; na
c) Itaridhia iwapo hakuna sababu za msingi za kufanya mabadiliko.
d) Kamati ya Katiba itaanza kazi rasmi mara baada ya kuridhiwa na Halmashauri;
e) Kamati ya Katiba itakamilisha kazi ya kuandika rasimu ya katiba na katiba
f) Itapitishwa na Mkutano Mkuu.
g) Maoni ya marekebisho ya Katiba yatakusanywa kwa utaratibu ufuatao-
h) Mwanachama atawasilisha kwa katibu wa Kata yake na katibu wa kata atayafikisha kwa katibu wilaya maoni ya marekebisho ya katiba
i) Kwa maandishi muda wowote anapogundua mapungufu kwenye katiba inayotumika;
j) Katibu wa kata ataweka maoni ya mwanaumoja mahala pa usalama;

11.5. Katibu wa mkoa atawasilisha maoni hayo kwa Kamati ya Marekebisho ya Katiba muda wa kurekebisha Katiba utakapowadia; na
   a) Mwanaumoja atafuatilia kuhakikisha kwamba Kamati ya Kurekebisha Katiba
   b) Imepokea maoni yake; na
   c) Kamati ya Katiba itaweka utaratibu muafaka kwaajili ya kupata maoni kutoka kwa wanaumoja wengi kadri iwezekanavyo.
   d) Iwapo kwa sababu zozote zile idadi ya wajumbe wa Kamati ya Katiba itapungua-
   e) Kamati Kuu itaongeza wajumbe kulingana na idadi ya wajumbe waliopungua;

f) Kama hakuna kikao cha Kamati Kuu kinachotarajia kuitishwa ndaniya siku 15 tangu
g) Idadi ya wajumbe kupungua, Katibu Mkuu baada ya kushauriana na Mwenyekiti.
h) Makubaliano yatafikiwa kwa njia ya kupiga kura; na
i) Iwapo Kura zitagawanyika nusu kwa nusu mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

11.6. Katika kupitisha vifungu vya katiba na hatimaye katiba nzima, vifungu ambavyo vitazua mabishano-

a) Wanaumoja watazingatia maelezo ya wajumbe wa Katiba;
b) Iwapo kuna haja Kura zitapigwa na kifungu kitapitishwa kwa kura za wanaumoja
c) Wengi; na
d) Kamati ya marekebisho ya katiba itaingiza nyongeza ya vifungu vilivyoamuliwa na Mkutano Mkuu;
e) Isipokuwa makosa yakiuchapishaji tu, kamati ya katiba haitafanya marekebisho
f) Yoyote kwenye katiba iliyopitishwa na MkutanoMkuu.

11.7. Baada ya Kamati ya Katiba kumaliza kuandaa katiba iliyopitishwa:

a) Mwenyekiti na Katibu Mkuu watatia saini zao kwenye Katiba kuthibitisha kupitishwa Kwake kwenye Mkutano Mkuu; na
b) Katiba iliyosainiwa kwenye nakala za kutosha itawasilishwa kwa mamlaka zinazohusika Ili isajiliwe.
c) Kuanza kutumika Kwa Katiba hii

11. 8. Mabadiliko ya Katiba au uundwaji wa Katiba Mpya utapitishwa na Mkutano Mkuu kwa kura ya siri na itahesabika kuwa mabadiliko au Katiba mpya imekubaliwa endapo zaidi ya nusu ya wajumbe waliohudhuria kikao husika wamekubaliana na pendekezo lililowasilishwa.

10.9. Katiba hii imepitishwa na wanaumoja kwenye Mkutano Mkuu na kuanza kutumika leo

Siku ya......................mwezi wa.......................................

**MWENYEKITI (W) …………….** **KATIBU MKUU (W)…………..**

# KANUNI ZA UMOJA WA BODABODA MKOA WA ARUSHA ( UBOMA).

Kwa vile katiba ni sheria mama ambayo hutoa kwa ujumla miongozo na taratibuza uendeshaji wa taasisi husika,usimamizi wa kina wa shughuli za taasisi huundiwa kanuni ili kuifanya katiba iwe ndogo na utekelezaji wake uwe rahisi kwa malengo ya kueleweka.

Wajumbe wa halmashauri kuu kwa mamlaka waliyopewa na katiba ya umoja wa bodaboda mkoa wa Arusha toleo la 2024 sura ya kumi ibara 10.1. Baada ya majadiliano wameamua kutengeneza kanuni za umoja ambazo zitawezesha utekelezaji bora wa katiba kwa mustakabali wa umoja wetu.

Kanuni hizi zitatajwa kama kanuni za umoja wa bodaboda mkoa wa Arusha Toleo la 2024 na zitaaza kutumika tarehe 16/04/2024.

# KUJIUNGA NA UMOJA NA KIINGILIO:

1.1 Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 3.5 cha katiba ya umoja, mtu yeyote mwenye sifa za kujiunga na umoja kama zilivyoainishwa kwenye kifungu cha 3.5 (a-r) atajaza fomu ya maombi ya kujiunga na umoja ambayo

1.2 itajulikana kama F.U.B.M.1.na kulipa kiingilio kabla ya kuikabidhi kwa katibu wa kituo ambaye ataiwasilisha kwa katibu wa kata na baada ya hapo katibu wa kata atawasilisha fomu hiyo kwa katibu mkuu wa umoja kwa ajili ya kujadiliwa.

1.3 Baada ya kuweka maoni, kata itawasilisha fomu kamati kuu ambayo ndiyo itakayokuwa na uamuzi wa mwisho wa kumpokea mwanachama mpya ( Katiba 3.6)

1.4 Isipokuwa kwa mtu ambaye maombi yake yamekataliwa kwa sababu ya kukosa vigezo vilivyowekwa na kifungu cha (katiba 3.7) cha katiba ya umoja kiingilio hakitarudishwa.

1.5 Kiingilio cha mwanachama mpya atakaye jiunga na umoja wa bodaboda mkoa wa Arusha kitakuwa ni shilingi za kitanzania Laki moja (50,000) tu.

1.6 Kiingilio hicho kitakuwa na mchanganuo ufuatao kwa mujibu wa katiba ya umoja-:

   a) Kiasi cha shilingi Elfu kumi (10,000) kitawekwa kwenye akaunti ya bodaboda mkoa.
   b) Kiasi cha shilingi Elfu kumi (10,000) kitawekwa kwenye akaunti ya bodaboda ya wilaya husika.
   c) Kiasi cha shilingi Elfu kumi (10,000) kitawekwa kwenye akaunti ya kata mwanachama anachoenda kufanyia kazi.
   d) Kiasi cha shilingi Elfu kumi (10,000) kitawekwa kwenye akaunti ya kituo

1.7 Kanuni za umoja wa bodaboda mkoa wa Arusha zinaelekeza uongozi wa Kituo endapo watakuwa na fedha kwenye mfuko wao wa kituo, kituo kitampa utaratibu mwanachama mpya atakayejiunga na kituo hicho kulipa fedha kidogokidogo ili aweze kuendana na wenzake ndani ya mfuko ili atakapopata shida aweze kuhudumiwa na kituo chake.

1.8 Kiingilio cha mwanachama kitalipwa Kwa mkupuo na iwapo mwanachama atabainika alitoa taarifa za uongo kipindi anajiunga na kituo hicho basi uanachama wake utakuwa batili. ( Katiba 3.7)

1.9 Bila kuathri kifungu cha 1.7 cha kanuni mwanachama aliyejiunga na umoja ataanza kupata huduma baada ya kumaliza kulipia kiasi cha fedha kilichoko kwenye mfuko baada ya kupewa mchanganuo kwa kila mwanachama.

1.10 Kamati kuu haitapokea au kujadili fomu ya maombi ya kujiunga na umoja ya mtu ambaye hana sifa ya kujiunga na umoja kwa masharti yaliyoanishwa kwenye kifungu cha 3.5 na kifungu cha 3.6 cha katiba ya umoja.

1.11 Mwanachama mpya ataanza kulipa ada ya kila mwezi kuanzia mwezi aliojiunga kwenye kituo baada ya mwezi kupita tangu ajiunge na umoja.

## Ada ya kila Mwezi:

1.12. Ada ya mwanachama ya kila mwezi itakuwa ni shilingi Elfu moja (Tshs 1000/=) Tu. Na italipwa kwa mkupuo.

1.13. Ada ya kituo ya kila mwezi itakuwa ni shilingi Elfu tano tu (Tshs 5000/=)

1.14. Mwanachama hatapewa huduma yoyote kati ya huduma zitolewazo na umoja iwapo atakuwa hajalipa kikamilifu ada ya kila mwezi kwa muda wa miezi mitatu au zaidi.

1.15. Mweka hazina wa Bodaboda kata atawajibika kuaandaa taarifa ya madeni, mapato na matumizi kila mwezi na kuiwasilisha kwa mweka hazina wa chama ngazi ya wilaya.

## Michango mingine:

1.16. Kwa ridhaa ya mkutano mkuu na kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na umoja kunaweza kufanyika michango mingine.

1.17. Harambee inayohusisha wanaumoja na wageni waalikwa itaitishwa kwa ajili ya kuchangia fedha zitakazowezesha jambo lililokubaliwa na halmashauri kuu.

## Taarifa za wanachama:

**1.18.** Kamati kuu itatunza usajili wa taarifa zote za wanachama na wategemezi kwenye daftari maalum au kwenye mfumo laini wa computa ya umoja.

1.19. Ni jukumu la mwanachama kujaza fomu ya taarifa zake na ndugu zake wanaotambulika kikatiba kwa usahihi.

1.20. Hatahudumiwa mtegemezi wa mwanachama asiyetambulika kikatiba.

## Msiba,

1.21. Mara Msiba utokeapo Kamati kuu ya umoja wa bodaboda mkoa wa Arusha itashirikiana na uongozi wa bodaboda wilaya,kata,na kituo pamoja na mfiwa kupanga taratibu zote za msiba kulingana na mazingira ya msiba husika. Hii ni pamoja na maandalizi ya awali ya mazishi na kuhudumia msiba kabla ya kusafirisha mwili wa marehemu.

1.22. Mwenyekiti au kiongozi mwingine aliyeteuliwa atawakilisha umoja na atakuwa sehemu ya Kamati ya Msiba na atashiriki kikamilifu kulingana na mazingira ya msiba ulipotokea.

1.23. Wanachama wenye nia ya kusindikiza msiba watajiandikisha kwa kiongozi mwenye dhamana ya mawasiliano kwenye Umoja ndani ya muda utakaokuwa umetangazwa

1.24. Panapotokea msiba, kituo husika pamoja na kata husika ambapo msiba umetokea wanaweza kulala msibani angalau kwa siku moja au mbili kama itahitajika kufanya hivyo kulingana na mazingira ya msiba husika.
1.25. Iwapo waliojiandikisha ni wengi kuliko uwezo wa gari lililoandaliwa, Wanaumoja wa Kata yake watapewa kipaumbele kwanza, wanaotokea kijiji au kata msiba unapopelekwa na baadaye waliojiandikisha watafuata.
1.26. Kamati Kuu itamteua mmoja wa Wanachama wanaosindikiza msiba kuwa kiongozi na mratibu wa wanaumoja kabla ya kuanza safari ya kuelekea msibani.
1.27. Gharama za mwanachama huyo atayekiwakilisha chama kwenda na kurudi kutoka msibani zitalipwa na umoja kulingana na umbali wa eneo husika.
1.28. Wanaumoja wanashauriwa kuwa na ushiriki mzuri kwenye msiba kuliko kutumia muda wao mwingi kwenye ratiba zisizohusiana na msiba waliosindikiza.
1.29. Kwa msiba unaosafirishwa na usiosafirishwa kiasi cha Shilingi Laki Tano (Tsh.500, 000) Tu kitatolewa na Umoja kwa ajili ya maandalizi ya awali ya mazishi kwa mujibu wa katiba hii.

## Ugonjwa,

1.30. Kwa ugonjwa wa kulazwa hospitalini Mwanaumoja au mtegemezi atapewa shilingi Laki Mbili Tsh 200,000/-Tu kama huduma ya matibabu.
1.31. Huduma ya matibabu itatolewa iwapo mnufaika wa huduma za umoja kikatiba atakuwa amelazwa hospitalini siku tatu na kuendelea.
1.32. Mnufaika wa huduma ya matibabu kikatiba atapewa shilingi laki mbili (Tsh 200,000/-) hata kama hakulazwa hospitalini lakini kwa sababu ya aina au namna alivyougua ugonjwa umepelekea kuugulia nyumbani kwa zaidi ya mwezi mmoja na kuendelea.
1.33. Mnufaika aliyetajwa katika kanuni hii kanuni ndogo ya 7.21 atatakiwa kuthibitisha ugonjwa huo kwa ripoti ya daktari au mwenendo wa matibabu ya hospitali
1.34. Huduma ya matibabu inaweza kutolewa tena kwa mnufaika yuleyule kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 21 na 22 baada ya miezi sita tangu huduma ileile kutolewa.
1.35. Mwanachama atatakiwa kutoa taarifa kwa kiongozi mwenye dhamana ya mawasiliano ndani ya masaa kumi na mawili (12) tangu alazwe hospitali ili Wanaumoja wamtembelee na kumjulia hali na atalazimika kutoa taarifa mara baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali.
1.36. Mwanaumoja ambaye ni mgonjwa kwa sababu ya ugonjwa anaougua amepoteza matumaini ya kupona na kuamua kusafiri ili aendelee kuugulia nyumbani, na akalazimika kusitisha uanachama wake kwenye umoja atalipwa Shilingi Milioni Moja (Tsh.1, 000,000/-)
1.37. Huduma hiyo ya mwanachama mgonjwa haitatolewa mpaka mwanachama awe amedumu kwenye umoja kipindi cha miaka 10 tangu kujiunga kwake na lazima awe mwanachama hai ambaye analipa ada yake kwa wakati.
1.38. Mwanaumoja ambaye ametajwa katika kanuni hii kanuni ndogo ya 7.25. Atawasilisha barua ya maombi kwenye Kamati Kuu ili alipwe hela ya kwenda kuugua na kwa kufanya hivyo ajue anahitimisha uanachama wake tangu siku ya kulipwa fedha kwa mujibu wa kanuni hii

1.39. Iwapo mgonjwa/mnufaika wa huduma iliyotolewa chini ya kanuni hii kanuni hii akipona na kurudi kwenye umoja atalazimika kufuata taratibu za kujiunga upya na umoja kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha katiba.

1.40. Huduma haitatolewa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 36, iwapo Kamati Kuu itajiridhisha kwamba kwa jinsi anavyougua, hasitahili kupata huduma hiyo.

1.41. Bila kujali kanuni hii kanuni ndogo ya 7.25, Kamati Kuu italazimika kutoa huduma kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo iwapo mnufaika amewasilisha taarifa ya Daktari wa Hospitali ya Wilaya au Mkoa kuthibitisha kwamba mwanachama huyo yupo kwenye matibabu endelevu (palliative care) ya hatua za mwisho wa maisha.

## Uthibitisho wa huduma kwenye umoja,

1.42. Kwa minajili ya kanuni za fedha, wanachama wote watakaokuwa wamepewa huduma ya mchango wa matibabu, mazishi, na safari au kwa sababu nyingine yoyote; watasaini hati ya malipo mara tu baada ya malipo na baadaye kutoa uthibitisho kama wanastahili malipo hayo.

1.43. Kielelezo cha udhibitisho wa kulazwa hospitalini ni fomu ya kuruhusiwa kutoka hospitalini inayoonyesha tarehe ya kulazwa na tarehe ya kuruhusiwa; na uthibitisho wa msiba ni cheti cha kifo au barua ya afisa mtendaji wa kijiji kuthibitisha kutokea msiba husika.

1.44. Ni jukumu la mwanachama atakaye leta barua ya Afisa Mtendaji wa kijiji/mtendaji wa kata kuhakikisha kuwa inakuwa na taarifa zifuatazo:-

i. Anuani ya posta ya ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji.
ii. Majina matatu ya marehemu.
iii. Tarehe na mahali pa maziko.
iv. Majina kamili ya afisa mtendaji wa kijiji..
v. Mhuri, tarehe na sahihi ya Afisa Mtendaji.
vi. Namba ya simu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji.

1.45. Uthibitisho wowote wa huduma hizi lazima utolewe ndani ya siku 60 tangu kutolewa kwa huduma husika; na mwanachama atakayeshindwa kuwasilisha uthibitisho au kuwasilisha uthibitisho usiokidhi atalazimika kurejesha kiasi cha fedha aliyopewa kama huduma ndani ya siku 15 tangu siku 60 kuisha

1.46. Udanganyifu wowote katika kupata na kutoa huduma yoyote ya umoja ni kosa kubwa sana na la kumfanya mhusika aliyethibitika kufanya hivyo kufutiwa na kufukuzwa uanachama na kuchukuliwa hatua nyinginezo za kisheria.

1.47. Mkopo siyo huduma, hivyo mkopo unaweza kutolewa au usitolewe kutegemeana na uwezo wa mfuko, mwenendo wa mkopaji wa kurejesha mikopo na uamuzi wa mamlaka inayoidhinisha mikopo.

1.48. Mkopaji atakuwa mwanaumoja hai ambaye atakuwa ametimiza miezi 6 au zaidi tangu kujiunga na umoja.

1.49. Taratibu za kuomba mkopo ni mwanachama kujaza nakala tatu za fomu maalum ya maombi ya mkopo ambayo itajulikana kama. (F.U.B.M.A 2)

1.50. Mwombaji wa mkopo lazima adhaminiwe na Kituo chake na wanachama/Wanaumoja hai ambao pia wana sifa za kupata mkopo huo na ambao hawana deni lolote la mkopo wa Umoja.

1.51. Wadhamini watasaini maelezo ya wajibu wao na kuahidi kuyatekeleza kama (F.U.B.M.A 2) itakavyo eleza.
1.52. Kamati kuu ya Umoja wa Bodaboda mkoa wa Arusha ndiyo ina mamlaka ya mwisho ya kupitisha au kutopitisha mkopo.
1.53. Mkopo ni lazima ulipwe ndani ya miezi minne kwa riba ya 10% kwa kipindi chote.
1.54. Iwapo muda wa miezi minne umeisha na mkopaji hajamalizia kulipa mkopo wake , mkopaji na wadhamini yaani kituo anachopaki watawajibika kulipa mkopo na adhabu ya 10% ya mkopo pamoja na riba ndani ya siku thelathini baada ya muda wa kawaida kuisha.
1.55. Iwapo mkopaji na atashindwa kulipa mkopo wote pamoja na adhabu ya 10% hata baada ya nyongeza ya siku thelathini mkopaji atafungiwa huduma za Umoja lakini pia viongozi wa mkoa kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya, kata na kituo wanaweza kuchukua hatua kali za kisheria kumuondoa mwanachama huyo ndani ya kituo
1.56. Kiasi cha juu ambacho mwanachama anaweza kukopeshwa ni shilingi milioni (Tsh 2,000,000) kushuka chini.

# UBOMA DAY.

7.58 .Uboma Day ni suala la kikatiba na la haki kwa kila mwanaumoja kushiriki.

7.59. Mfuko wa Umoja utachangia kiasi cha fedha kilichoombwa na Kamati ya Maandalizi ya uboma Day na kukubaliwa na Kamati Kuu ambayo itaomba Mkutano Mkuu au itaruhusu Kamati ya Maandalizi ya uboma day kuomba Mkutano Mkuu kuridhia ili kufanikisha maandalizi ya sherehe hiyo.

7.60. Sikukuu ya Uboma day itafanyika kila jumapili ya mwisho mwezi December kila mwaka.

7.61. Kabla ya sherehe hiyo kutakuwa na matukio mbalimbali kama:

- Kuchangia damu.
- Kufanya usafi.
- Michezo mbalimbali ya kama vile; michezo ya bahati na sibu, mpira wa miguu, kufukuza kuku, kukimbia na gunia n.k

7.62. Kamati itaratibu na kusimamia sherehe nzima ya uboma day. Kamati hii itahakikisha uboma Day inakuwa na vionjo mbalimbali na hivyo kuifanya kuwa ya kipekee kwenye umoja wetu wa bodaboda mkoa wa Arusha.

7.63. Kwenye Mkutano Mkuu utakaofanyika baada ya sherehe ya uboma Day wanaumoja watafanya tathimini na kutoa mapendekezo ya kuboresha uboma Day kwa mwaka unaofuata.

## Mikutano, Vikao na Gharama za mikutano,

7.64. Vikao vya Kamati Kuu na vile vya kamati za kikatiba ambavyo wajumbe wanaweza kujipangia siku na muda wa vikao kulingana na mazingira ya wajumbe, muda wa kuanza vikao, mikutano. 5:00 asubuhi na kumaliza 10:00 alasiri.

7.65. Endapo kutakuwa na ulazima wa mkutano kuendelea baada ya saa 10:00 alasiri, Mwenyekiti wa kikao au Mkutano ataomba ridhaa ya kuongeza muda hadi dakika 30 na muda huo utaombwa dakika 15 kabla ya muda wa kawaida kuisha. Maombi hayo lazima yakubaliwe na wajumbe walio wengi.

7.66. Litaandaliwa daftari la mahudhurio kila kikao, msiba, na Mkutano Mkuu na Akidi ya Mkutano Mkuu ni asilimia 75% ya wanachama wote watakao kuwa tayari wamejiandikisha kuondoa wenye udhuru wa kudumu.

7.67. Mwanachama ambaye atashindwa kuhudhulia Mkutano Mkuu, vikao vya kata, kikao cha kituo au vikao vya viongozi kwa sababu za msingi lazima aombe udhuru saa moja kabla ya kuanza kikao.

7.68. Mwanaumoja atakaye omba udhuru kwa masharti ya kanuni hii atachukuliwa kuwa maombi yake ya udhuru yamekubaliwa iwapo amepokea majibu ya kukubaliwa na yanayoweza kuthibitika.

7.69. Kabla ya Mkutano, vikao vya Kata au kikao cha kituo kuanza Mwenyekiti atamwagiza Katibu kusoma majina ya walioomba udhuru.

7.70. Ni mwanachama wa umoja mwanachama pekee mwenye wajibu wa kuhudhuria na haki ya kupiga kura katika mkutano au kikao.

7.71. Umoja utatoa Shilingi Elfu Ishirini (Tsh. 20,000) kila mwezi kwa kiongozi aliyepewa dhamana ya mawasiliano kwa ajili ya mawasiliano yaani katibu mkuu wa umoja.

7.72. Mweka hazina atapewa Shilingi Laki Mbili (Tsh200, 000/-) Tu kwa ajili ya matumizi madogomadogo (petty cash) kila mwezi na iwapo haitatumika au kusalia lazima usuluhisho (reconciliation) kati ya mwezi ulioisha na unaoanza ifanyike ili kuondoa usumbufu wa kurudisha salio la matumizi madogomadogo (petty cash) benki.

7.73. Miezi ambayo Mkutano Mkuu unafanyika au miezi ambayo kutakuwepo na vikao vya Kamati mbalimbali, kiasi cha matumizi madogomadogo (Petty Cash) inaweza kuongezwa hadi Tshs 300,000/- kwa mwezi.

7.74. Kiasi cha Gharama za kuandaa mkutano mkuu kinaweza kupitishwa na kamati kuu na baadae kutoa mrejesho halmashauri kuu.

7.75. Kila mwanachama wa kituo atatoa kiasi cha shilingi elfu moja (Tsh 1,000) Tu kwa ajili kugharamia viongozi kituo watakao kwenda kwenye vikao vya juu.

7.76. Viongozi wa umoja watakao kwenda kutatua mgogoro kwenye kituo ngazi ya kata ni shilingi elfu ishilini 20,000/= kwa viongozi wote, Ngazi ya wilaya shilingi elf thelathini (30,000/=) na ngazi ya mkoa ni shilingi elfu arobaini (40,000/=

7.77. Viongozi wa umoja watakapo kaa vikao vya kikatiba au vya dharula ngazi ya kata watalipwa shilingi elfu kumi 10,000/= kwa kila mmoja, Ngazi ya wilaya kila mmoja atalipwa shilingi elfu ishilini 20,000/=na Ngazi ya mkoa kila mmoja atalipwa shilingi elfu thelathini 30,000/=

7.78. Posho za safari za viongozi kila ngazi husika zitalipwa kutegemea na safari yenyewe anakokwenda umbali pamoja na gharama za maradhi tangu alipoanza safari mpaka atakaporudi.

7.79. Gharama za safari zitalipwa endapo kiongozi au viongozi wanaenda kwa ajili ya maswala ya umoja na siyo vinginevyo.

## Kanuni za fedha,

7.75. Kutakuwa na kitabu cha mali za umoja kitakachotunzwa na Mweka Hazina wa Umoja

7.76. Vitabu vyote vya stakabadhi, hati za malipo na mali zote vitasajiliwa kwa namba maalumu katika kitabu cha mali cha Umoja.

7.77. Baada ya uongozi kumaliza muda wake, Mwekahazina atakabidhi kitabu cha mali kwa uongozi mpya.

7.78. Kila malipo yote yanayofanywa na Umoja lazima yathibitishwe kama kanuni za malipo zinavyotaka. Kukosa uthibitisho kutoka kwa kiongozi au mwanaumoja juu ya matumizi ya fedha yoyote atabeba wajibu wa kurudisha fedha hizo.

7.79. Makusanyo yote yanayofanyika lazima yalipwe benki na kukatiwa stakabadhi baada ya mlipaji kuwasilisha pay-in-slip halisi kwa mweka hazina.

7.80. Kwa kutambua unyeti wa shughuli ya harambee na/au mnada inayoendeshwa na Umoja, Mwekahazina anaweza kupokea fedha taslim za malipo yote yanayofanyika kwenye mnada husika na ni lazima azipeleke au asababishe zipelekwe benki ndani ya siku mbili tangu tarehe ya mnada na baadaye kutoa stakabadhi.

7.81. Bila ya kuathiri kanuni hii na masharti ya kifungu cha katiba ni kosa kwa mwanachama au kiongozi yoyote asiyekuwa na idhini ya Mwekahazina kupokea fedha taslim kwa niaba ya Umoja.

7.82. Kila mlipaji ni lazima aandike kwenye Bank Deposit Slip jina lake, na dhumni la malipo hayo mfano faini, adhabu, mkopo, kiingilio, ada ya mwezi, nakadhalika.

7.83. Mwanaumoja sharti alipe madeni ambayo muda wake ni mrefu kabla ya kulipa madeni mapya.

7.84. Malipo yote yanayofanywa na Umoja kwenda kwa mtu yeyote ni lazima yawe na ushahidi wa maandishi aidha kwa stakabadhi iliyotolewa au maandishi mengine kulingana na taratibu za katiba au kanuni hizi.

7.85. Malipo yote kuanzia Tsh 100,000/- yatakayofanywa kwa mwanaumoja au mtu mwingine yeyote na umoja yatalipwa kwa kutumia hundi (bank cheque) na malipo yote chini ya Tsh 100,000/- yatalipwa kwa pesa taslimu kutoka kwenye petty cash na kusaini kwenye petty cash voucher.

7.90. Bila kuathiri masharti ya kanuni hii kanuni ndogo ya 7.89, malipo yanayozidi Tshs 100,000/- yanaweza kulipwa Taslim pale mazingira yanapolazimu.

# Ukaguzi wa Hesabu za Umoja.

7.91. Kamati kuu itateua mkaguzi wa fedha wa nje (external auditor) mwenye sifa zinazotambuliwa na mamlaka za nchi.

7.92. Mkaguzi wa fedha wa nje atateuliwa kutoka miongoni mwa wanaumoja na kama hayupo atateliuwa nje ya wanaumoja.

7.93. Iwapo mkaguzi wa fedha atatoka ndani ya umoja atalazimika asiwe kiongozi.

7.93. Mkaguzi wa fedha atathibitishwa kila baada ya miaka miwili tangu kuteuliwa japo kwa sababu za msingi juu ya utendaji wake Halmshauri inaweza kumwondoa na kuthibitisha mwingine muda wowote.

7.94. Halmashauri inaweza kupitisha posho ya Mkaguzi wa Nje ambaye siyo Mwanaumoja kadri itakavyoona inafaa lakini kwa vyovyote vile isiwe zaidi ya Tshs 500,000/-

7.95. Majina ya wakaguzi wa nje yaliyoteuliwa na kamati kuu yatachambuliwa na mmojawapo kuthibitishwa na Halmashauri.

7.96. Iwapo kuna tuhuma za ubadhirifu wa fedha dhidi ya Kamati Kuu, Halmashauri inayo mamlaka na uhuru wa kuteua na kuthibitisha mkaguzi yeyote wa nje ambaye si Mwanachama wa Umoja wa bodaboda mkoa Arusha kwa ajili ya kufanya ukaguzi maalum.

7.97. Iwapo Mkaguzi wa nje ameteuliwa na kufanya ukaguzi kwa mujibu wa kanuni ndogo, taarifa ya matokeo ya ukaguzi itakabidhiwa kwenye kikao cha Halmashauri kuu.

7.98. Kiongozi yeyote atawajibishwa na mamlaka mbali mbali kutokana na ripoti ya mkaguzi wa nje ikiwemo kulipa gharama ya fedha, kusimamishwa uongozi, na ikibidi baadaye kufukuzwa uanachama.

7.99. Ripoti ya ukaguzi wa fedha ni jambo la lazima na lisilo na mjadala. Uongozi utakaoshindwa kuwasilisha ripoti halisi na kuisoma mbele ya mkutano mkuu wa Desemba bila sababu za msingi utawajibishwa na mkutano mkuu.

## Mfuko mkuu wa Umoja

7.100. Isipokuwa kwa matukio yasiyoweza kuzuilika, muda wote Mfuko wa Umoja utakuwa na salio lisilopungua Shilingi Milioni hamusini (Tsh 50,000,000/-) Tu

7.101. Iwapo itatokea Mfuko wa Umoja ukawa chini ya TZS 50,000,000/- na kwa vyovyote vile makusanyo yanayotegemewa kwenye kipindi cha miezi sita inayofuatia hayawezi kuirudisha, Kamati Kuu itagawa sawa kwa wanaumoja wote kiasi kisichoweza kurudishwa ili Wanaumoja wakichange ndani ya miezi sita kwa mujibu wa katiba.

7.102. Ili kupata kiasi cha fedha kinachohitajika kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 7.101, kiasi cha fedha kinachohitajika kitagawanywa sawa kwa Wanaumoja wachange.

7.103. Mwanaumoja atakaye shindwa kuchanga mchango wa kutunisha kwa mujibu wa kanuni atasimamishwa kupokea huduma za umoja na hatua nyingine kufuatia kwa mujibu wa Katiba ya Umoja.

7.104. Mweka hazina wa mkoa ,mweka hazina wa wilaya, mwekahazina wa kata na wa kituo na kamati za kikatiba kwa kushirikiana na kamati ya Fedha na Uchumi watabuni namna bora ya ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha mfuko wa umoja unakua kifedha.

## Usimamizi wa Uwekezaji wa Umoja uboma Saccos

7.105. Kwa asili ya majukumu yake, Mweka Hazina atakuwa msimamizi wa kila siku wa uwekezaji wa Umoja kwenye Uboma SACCOS na mahali pengine Umoja utakapoamua kuwekeza.

7.106 Kwa asili ya majukumu yake, Mwenyekiti ni mwakilishi wa Umoja kwenye mialiko yote ya nje, hivyo yeye au mwanaumoja aliyemteua kumwakilisha atahudhuria Mikutano yote ya SACCOS au sehemu nyingine ambayo Uboma ina uwekezaji au maslahi na kusimamia maslahi ya Umoja yanayohusu uwekezaji wake.

7.107. Kazi kubwa ya mwakilishi wa Umoja kwenye Mkutano wa Uboma SACCOS au sehemu nyingine yenye uwekezaji au maslahi ya Umoja ni kupiga kura na kuamua mstakabali wa maslahi ya Umoja kwa niaba ya Wanaumoja wote.

7.108. Mwakilishi huyu kwa wadhifa wake atasimama kama Umoja wa bodaboda mkoa wa Arusha mahala ambapo uboma ina uwekezaji au maslahi mengine.

7.109. Ijulikane kuwa Mwakilishi wa umoja wa bodaboda mkoa wa Arusha sehemu Umoja ulipowekeza ni kujitolea kwa maslai mapana ya umoja na atalipwa Tsh 20,000/- tu kutoka kwenye mfuko wa Umoja kwa kila siku

atakayowakilisha Umoja kama kifuta jasho. Mkutano Mkuu unao uhuru wa kumuuliza chochote kuhusu mustakabali wa uwekezaji wa Umoja.

# Faini na Adhabu Mbalimbali:

7.110. Muda wote viongozi wa umoja ngazi zote wachukue jukumu la kutoa elimu na kumsaidia mwanaumoja kuelewa kuwa kwa tabia anazoonyesha anavunja katiba na anaenda kinyume na maelekezo ya kanuni za umoja.

7.111. Mwanaumoja aliyefikishwa mbele ya kamati ya Nidhamu na Maadili na akakutwa na hatia ya kuvunja katiba au kwenda kinyume na kanuni za umoja ataadhibiwa. Kamati itamwamuru kulipa gharama za umoja zilizotumika wakati wa kushughulikia shauri hilo na kumwamuru kulipa faini ambayo Kamati itaona inafaa baada ya kuzingatia uzito wa makosa na mwenendo wa Mwanaumoja.

7.112. Kwa minajili ya kupanua wigo wa mapato, faini zote zitakazotozwa kwenye mkoa, wilaya Kata na kituo na Kamati za Kikatiba, Kamati Kuu, Halmshahauri na Mkutano Mkuu au kwa masuala mengine yasiyokuwa na uhusiano na vikao vilivyotajwa zitalipwa kwenye mifuko ya umoja kila ngazi kwa utaratibu wa malipo ya Umoja.

7.113. Kiongozi au Mwanaumoja atakayetozwa adhabu ya kutohudhuria au kuchelewa kikao cha Kituo, kata, wilaya na mkoa na Kamati ya kikatiba, Kamati Kuu, Halmashauri au Mkutano Mkuu adhabu hiyo atailipa siku hiyo hiyo kupitia utaratibu wa malipo kuweka fedha kwenye akaunti.

7.114. Adhabu ya Kutohudhuria kikao chochote halali cha Umoja, kila ngazi ya kituo, kata,au wilaya na mkoa bila ruhusa kwa mujibu wa katiba ni Tshs 5,000/=

7.115. Adhabu ya makosa yote yaliyoainishwa chini ya kifungu 6.1.15 na 6.1.16 cha katiba ya Umoja na endapo mwanachama atathibika kuyatenda atatozwa faini kama ifuatavyo-:

a) Ngazi ya kituo itakuwa shilingi elfu kumi (10,000/=) tu

b) Ngazi ya kata itakuwa shilingi elfu ishilini (20,000/=) tu

c) Ngazi ya wilaya itakuwa ni shilingi elfu thelathini (30,000/=) na

d) Ngazi ya mkoa ni shilingi elfu arobaini (40,000)

# Taarifa ya madeni ya Wanaumoja:

7.117. Pamoja na taarifa ya michango ya kila mwezi, Mwekahazina wa mkoa, mwekahazina wa wilaya, mwekahazina wa kata na kituo atawasomea wanaumoja wote kwenye mkoa,wilaya,kata na kituo taarifa ya wanaodaiwa madeni mbalimbali ya umoja.

7.118. Taarifa ya madeni kwa wanaumoja itatolewa kila mwezi.

7.119. Ni wajibu wa Kamati kuu kuandaa taarifa ya madeni ya kila kata ili kila Mwekahazina wa Kata aichukue na kuisoma kwenye kikao cha Kata.

## Upigaji Kura Mkutano Mkuu

7.120. Maamuzi ya Umoja yatakayohitaji kufikiwa kwa kupiga kura, yatatambuliwa kuwa halali kutokana na kura halali tu zitakazopigwa.

7.121. Kura halali ni kura ambayo itapigwa na mwanaumoja aliyeoa au kuolewa. Itakuwa kinyume cha Katiba ya umoja kwa mgeni au mtegemezi kupiga kura.

7.122. Kura zitachukuliwa halali iwapo idadi iliyopigwa ni sawa na wanaumoja waliohudhuria mkutano husika.

7.123. Kila mkutano lazima uwe na akidi inayotakiwa na kanuni hizi.

## Utaratibu wa kumfukuza mwanammoja

7.124. Iwapo Kamati Kuu itaona mwanachama yeyote amekiuka katiba au kanuni hizi na anatakiwa kufukuzwa uanachama itapitisha azimio la lengo la kumfukuza mwanachama katika Umoja.

7.125. Azimio ni lazima litaje kosa analotuhumiwa nalo na kwa kiasi gani kosa hilo adhabu pekee ni kufukuzwa uanachama.

7.126. Nakala ya Azimio hilo atapewa mwanachama na Katibu wa Kata.

7.127. Baada ya azimio kupitishwa na Kamati Kuu, Katibu Mkuu ataliwasilisha kwenye Kikao cha Halmashauri kuu ambayo itamwalika Mwanachama husika kwa ajili ya kusikiliza utetezi wake

7.128. Nukuu yoyote ya maelezo inayoandikwa na katibu wa Kikao cha Halmashauri wakati wa kusikiliza shauri lazima mhusika asomewe na kama anakubali ndicho alichokitamka atie sahihi yake kila ukurasa wa nukuu hizo.

7.129. Halmashauri itapokea nyaraka zote za maandishi na kuziambatisha na nukuu za maelezo ya Mwanaumoja ili kujiridhisha na uzito wa makosa.

7.130. Baada ya kumsikiliza, Halmashauri, ikimkuta mwanachama anayetuhumiwa ana hatia inaweza:

a) Kutoa masharti ya Mwanaumoja kujirekebisha na kurejea kwenye utaratibu wa Umoja ndani ya muda itakao ona unafaa;

b) Kumuweka chini ya kipindi cha uangalizi.

c) Kumfukuza kwa mujibu wa Katiba ya Umoja.

7.131. Bila kuathiri masharti ya Katiba ya Umoja, mwanaumoja asiporidhika na uamuzi wa Halmashauri, ndani ya siku 28 tangu kupokea barua ya kufukuzwa anaweza-:

7.132. Kuwasilisha maombi kwa Halmashauri akiomba irejee uamuzi wake.

7.133. Kukata rufaa kwenye kamati ya rufaa

7.134. Baada ya kupokea rufaa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 7.133, Katibu Mkuu atalazimika kuiweka kwenye agenda za Mkutano Mkuu wowote utakaoitishwa mapema tangu kupokea maelezo ya mkata rufaa.

7.135. Iwapo Mwanaumoja hakutii wito wa kufika mbele ya Halmashauri kujitetea atawajibika kuueleza na kutoa ushahidi wa kuridhisha mbele ya Mkutano Mkuu kwamba alikuwa na sababu za msingi zilizo mfanya ashindwe kutii wito wa kufika mbele ya Halmashauri kusikilizwa.

7.136. Iwapo atashindwa kuonyesha kwa ushahidi kwamba sababu zilizotajwa zenye uzito sawa na hizo zilimfanya ashindwe kutii wito rufaa yake itatupiliwa mbali.

7.137. Iwapo rufaa haitakataliwa mwenye kukata rufaa, ili afaulu katika rufaa, sharti kuuridhisha Mkutano Mkuu kwa kuainisha makosa ambayo Halmashauri ilifanya na ambayo kama yasingekuwepo uamuzi wa kumfukuza usingefikiwa.

## Uchaguzi kwenye Umoja:

7.138. Kutakuwepo na Kamati ya Uchaguzi kwa mujibu wa Katiba ya Umoja.

7.139. Wajumbe wa Kamati ya uchaguzi watapendekezwa na uongozi wa juu ili kupata wasimamizi

7.140. Kwa muda unaofaa kabla ya Uchaguzi Kamati Kuu itaitisha kikao cha Pamoja kitakachojumu wajumbe wa kamati hiyo kuwaweka maswala sawa na kupitia vifungu vya Katiba vinavyohusu uchaguzi.

7.142. Baada ya Kamati Uchaguzi kupata viongozi kikao cha pamoja kitapitia vifungu vya Katiba na Kanuni ili Kamati ya Uchaguzi itoke na uelewa wa mchakato wa Uchaguzi.

7.143. Uchaguzi wa Viongozi wa Umoja utaitishwa kwa mujibu wa katiba.

7.144. Iwapo uchaguzi utashindikana kufanyika kwa sababu zozote zile baada ya uongozi kujiuzulu kwa mujibu wa katiba ya Umoja, kamati ya uchaguzi itatangaza kuwarudisha viongozi hao waliojiudhulu nafasi zao kuendelea kuongoza umoja mpaka uchaguzi utakapoitishwa tena.

7.145. Uongozi wa Umoja kwa mujibu wa Kanuni hii kanuni ndogo ya utajulikana kama uongozi wa mpito.

7.146. Bila kujali masharti Kwenye kipindi cha uongozi wa mpito, Wanaumoja wataendelea kulipa madeni kwa kuweka fedha benki na kukabidhi Bank Deposit Slip kwa Mweka Hazina wa Kata.

7.147. Bila kujali masharti ya Katiba ya Umoja, kwenye kipindi cha uongozi wa mpito, Mwanaumoja akikabidhi Deposit Slip kwa Mwekahazina wa umoja atahesabika kuwa amelipa.

7.152. Mweka Hazina wa umoja ataandika upande wa nyuma wa Deposit Slip tarehe ya kuipokea na atasaini.

7.153. Iwapo ni lazima kuna uhitaji wa fedha, uongozi wa mpito lazima upitishe matumizi hayo kwa asilimia 80 ya Wajumbe wote.

## Marekebisho ya Kanuni

7.154. Kanuni hizi zipitishwe na kura zaidi ya asilimia 75% ya wajumbe wote wa Halmashauri.

7.155. Halmshauri inaweza kubadilisha na/au kurekebisha, kanuni hizi muda wowote iwapo itaona kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Mabadiliko yoyote ya kanuni hizi kwa mjibu wa kanuni hii yatafanyika baada ya kupata kura 75% au zaidi ya wajumbe wote wa Halmashauri.

7.156. Katika kujadili kanuni Halmashauri itapiga kura kupitisha kanuni moja baada ya nyingine. Asilimia 51 ya kura za wajumbe waliohudhuria kikao zitapitisha Kanuni moja moja

7.157. Iwapo kura zinazohitajika kuamua kupitisha marekebisho kwenye kanuni hizi baada ya kupitisha kanuni moja moja hazitapatikana kwenye upigaji kura wa kwanza kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 1, Wajumbe wa Halmashauri watarudia kupiga kura hadi mara tatu.

7.158. Kura zisipotosha baada ya kupiga kura mara ya tatu, Mwenyekiti atatoa rai ya kuahirisha kikao mpaka siku nyingine ya karibu ambayo kikao kingine kitaitishwa.

7.159. Iwapo kwenye kikao kilichoitishwa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 5 kura zitapigwa na 75% ya kura zisipatikane baada ya kupiga kura mara tatu, kura zitapigwa mara ya nne ambapo Kanuni zitapitishwa kwa asilimia 60 ya kura zote.

7.160. Iwapo asilimia 60 ya kura zote haitapatikana kupitisha mabadiliko ya Kanuni hizi kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 6, Halmashauri itarejea kwenye kanuni zilizosababisha kanuni kukataliwa na vitarekebishwa kulingana na maoni ya walio wengi ilimradi marekebisho hayo hayalengi kutunga kanuni zinazopingana na Katiba.

## Kupitisha na Kuanza kutumika kwa Kanuni:

Kanuni hizi zimepitishwa na asilimia 95 ya wajumbe wa Kikao cha Halmshahuri siku ya ………………………ya mwezi wa ……………………, mwaka …………………… katika ukumbi wa ……………………………na kusainiwa na katibu na mwenyekiti wa Umoja ili zianze kutumika kuanzia tarehe …………………………….

Mwenyekiti Mkoa Sahihi……………………………………

KatibuMkoa Sahihi…………………………………….